

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Tatu – Tarehe 8 Aprili, 2022

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa tukae. Katibu!

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali; tutaanza na Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, Mbunge wa Arusha Mjini sasa aulize swalii lake.

Na. 21

**Idadi ya Wamachinga Halmashauri ya
Jiji la Arusha**

MHE. MRISHO M. GAMBO aliuliza:-

Je, Jiji la Arusha lina wamachinga wangapi, wapo maeneo gani na wangapi wamepatiwa vitambulisho hadi kufikia mwezi Februari, 2022?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange majibu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, Mbunge wa Jimbo la Arusha Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Februari, 2022 Jiji la Arusha lilikuwa na wamachinga 5,426 ambao walikuwa wamepangwa katika maeneo mbalimbali kama ifuatavyo; soko la Samunge, Kiwanja Na. 68 Soko la Kilombero, eneo la Ulezzi Mianzini, Machame Luxuary na Kilombero eneo la Daladala.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuratibu usajili na utoaji vitambulisho vya wamachinga, ambapo kwa Halmashauri ya Jiji la Arusha jumla ya wamachinga 1,187 sawa na asilimia 22 wamepatiwa Vitambulisho.

SPIKA: Mheshimiwa Mrisho Gambo, swali la nyongeza

MHE. MRISHO M. GAMBO: Mheshimiwa Spika, kwanza taarifa iliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri nina mashaka nayo, kwa sababu wako wamachinga wengi Jiji la Arusha ambao wamekosa maeneo ya kufanya baishara.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia taarifa ya Mheshimiwa Naibu Waziri ametuambia kwamba kwa sasa wao wamewatambua wamachinga 5,426 na kati ya hao wametoa vitambulisho kwa wamachinga 1187, je ni kwa nini wamachinga waliobaki mpaka sasa hivi hawajapata vitambulisho na wanaendelea kuchajiwa ushuru na Halmashauri ya Jiji la Arusha?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa mgambo ambao wanatumwa na Halmashauri ya Jiji la Arusha kuititia Mkurugenzi wa Jiji wamekuwa wanapora vitu vya watu vinakwenda kuwekwa kule depo vinaoza pia wanachukua

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

fedha za watu nje ya utaratibu kiasi cha kuleta manyanyaso na kufanya hali ya kisiasa...

SPIKA: Mheshimiwa Gambo sasa hapo unachangia, Mheshimiwa Gambo ulishauliza maswali.

Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo Mbunge wa Jimbo la Arusha Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba taarifa hizi zimetoka ndani ya Halmashauri ya Jiji la Arusha kwa watendaji wa Serikali ambao wamejiridhisha idadi ya wamachinga walioko pale na idadi ya wamachinga ambao wamepewa vitambulisho. Pamoja na kwamba Serikali na Jiji la Arusha lilikuwa katika utaratibu wa kuwapanga wamachinga lakini utaratibuwa kutoa vitambulisho ulikuwa unaendelea sambamba na kuwapanga wamachinga; kwa hiyo nikutoe shaka katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na kwa nini baadhi ya hawa wamachinga hawajapata vitambulisho; suala hili ni suala la kutoa elimu, kuhamasisha wale wamachinga wenye sifa waweze kutoa kwa hiari yao ili waweze kupata vitambulisho vile na kazi hii inaendelea kuelimisha ili hawa wallobaki nao wapate vitambulisho.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mgambo kuvamia na kupokea fedha na kumwaga bidhaa za wananchi, Serikali ilishatoa tamko, kwamba katika shughuli za kuwapanga wamachinga nchini kote mgambo hawahusiki na hawatakiwa kuhusika kuleta bugudha yoyote kwa wafanyabiashara. Kwa hiyo nitoe maelekezo kwa Jiji la Arusha

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kusimamia maelekezo ya Serikali ili wafanyabiashara hawa wasibughudhiwe na mgambo sehemu yoyote. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Aysharose Ndongholi Mattembe Mbunge wa Viti Maalum swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Ritta Kabati.

Na. 22

Hitaji la Gari la Wagonjwa – Hospitali ya Wilaya Mkalama

MHE. DKT. RITTA E. KABATI K.n.y. MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka gari la kubebea Wagonjwa katika Hospitali ya Wilaya ya Mkalama?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aysharose Ndoggoli Mattembe Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali kupitia Mpango wa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO-19 itanunua magari 195 ya kubebea wagonjwa ambayo yatagawiwa kwa Halmashauri zote 184. Kupitia utaratibu huu kila Halmashauri itapatiwa gari moja la kubebea wagonjwa, ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa magari ya kubebea Wagonjwa ili kuboresha na kuimarisha hali ya utoaji huduma za afya nchini kote.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Mheshimiwa Ritta Kabati, swali la nyongeza.

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, ahsante, na ninamshukuru Mhehsimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri naomba niulize maswali madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; ni lini Serikali itapeleka magari ya wagonjwa kwa Hospitali ya Iliongelo na Hospitali ya Wilaya ya Manyoni iliyopo Singida?

Mheshimiwa Spika, swali la pili vituo vya afya vya Ngome na Ipogolo vimekuwa vikitumia magari ya abiria katika kusafirisha wajawazito kwenda kujifungu. Ni lini sasa Serikali itaona umuhimu pia wa kutupatia magari katika hospitali yetu ya Wilaya ya Iringa Manispaa na katika vituo hivyo vya Afya vya Iringa Mjini?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ritta Kabati Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimetangulia kujibu kwenye jibu langu la msingi, kwamba Serikali itanunua magari ya wagonjwa 195 kwa ajili ya Halmashauri zetu zote 184 nchini kote. Kwa hivyo Kituo cha Afya na Hospitali ya Iliongelo na Manyoni zitanufaika kwa magari hayo lakini bado tutaedelea kutenga fedha kwa awamu ili vituo vingine vyote vipate magari ya wagonjwa, kwa maana ya kuboresha huduma za rufaa.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Kituo cha Afya cha Ngumi, Ipogolo na Hospitali ya Manispaa ya Iringa ni kweli ina changamoto ya gari la wagonjwa; na Manispaa ya Iringa nayo itanufaika na magari haya. Kwa hiyo changamoto hiyo

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kwa sehemu itakuwa imetatuliwa, lakini tutaendelea kutafuta magari zaidi.

Mheshimiwa Spika, tarehe 06 juzi Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan amezindua mpango mkakati wa M-mama ambao utawezesha rufaa za dharura katika mikoa 12 kwa kushirikisha wadau, wakiwemo Vodacom. Kwa hiyo pamoja na jitihada za Serikali lakini bado jitihada za *private sector* kama *Vodacom* tutakwenda kuondoa kabisa changamoto ya rufaa kwa wagonjwa wetu, asante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Saashisha Mafuwe swalii la nyongeza.

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Spika, asante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swalii la nyongeza, nikilwa na hakika kabisa kwenye magari na Wilaya ya Hai itapata.

Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza ni lini Serikali sasa itatuletea vifaa tiba kwenye kituo chetu cha afya cha Longoi ambacho kimekamilika, ili kiweze kuanza kazi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais - TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Saashisha Mafuwe Mbunge wa Hai kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali yetu imeendelea kutenga fedha za ununuzi wa vifaa tiba kwa awamu. Kwa sasa tayari imeshatenga kwa ajili ya Hospitali zile 67 za awamu ya kwanza lakini tutakwenda Hospitali zile 28 za awamu ya pili na vituo vya afya vitatengewa fedha baada ya kukamilika kwa hizi 67 na 28 kikiwemo Kituo hiki cha Afya katika Halmashauri ya Hai. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hicho ni kipaumbele cha Serikali na kadri

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ya upatikanaji wa fedha tutapeleka fedha na vifaa tiba katika Kituo cha Afya cha Hai.

SPIKA: Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, swali la nyongeza.

MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU: Mheshimiwa Spika, asante kwa kunipa nafasi. Naomba kujua Serikali ilitumia utaratibu gani kutoa fedha kwa ajili ya kujenga maeneo ya machinga kwa kutoa kwenye miji mingine na kwenye miji mingine kuacha hasa kama Mji wa Iringa?

SPIKA: Mheshimiwa Jesca hilo swali la machinga lilikuwa limeshapita, hili swali linalojibiwa hapa sasa hivi ni la kuhusu wagonjwa. Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako.

Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge tutaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina Mbunge wa Kisesa sasa aulize swali lake.

Na. 23

Wafugaji Kurejeshewa Mifugo yao Iliyokamatwa na TAWA na TFS - Kisesa

MHE. LUHAGA J. MPINA aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itarejesha kwa wafugaji mifugo iliyokamatwa na *TAWA*, *TFS* na *WMA* ambapo Mahakama ilitoa hukumu irejeshwe?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Masanja majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mbunge wa Kisesa, kama ifuatavyo:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Uhifadhi Wanyamapor Na. 5 ya mwaka 2009 ni kosa kuingiza na kuchunga mifugo ndani ya Hifadhi. Serikali ina jukumu la kulinda Rasilimali na Maliasili za Taifa, ikiwa ni pamoja na kuzuia uharibifu unaosababishwa na uvamizi wa mifugo ndani ya maeneo ya Hifadhi.

Mheshimiwa Spika, wafugaji wanapokamatwa na mifugo ndani ya hifadhi kesi zao hupelekwa Mahakamani ambapo hukumu hutegemea na maamuzi ya Mahakama. Hukumu inaweza kuwa kulipa faini na kurejeshewa mifugo au kutaifishwa. Endapo kuna wananchi ambao mifugo yao ilikamatwa na Mahakama kuamuru kurejeshewa mifugo yao na hawajarejeshewa, wawasilishe malalamiko yao Wizarani ili yashughulikiwe.

Mheshimiwa Spika, ili kuepukana na migogoro ya wafugaji, Serikali inawaomba wananchi hususani wafugaji kujiepusha kuingiza mifugo kwenye maeneo ya Hifadhi.

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Luhaga Mpina swali la nyongeza.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza suala la kuvunja sheria hapa halipo kwa sababu tayari hawa wananchi wameshashinda kesi mahakamani na Mahakama ikawapa ushindi na ikaamuru mifugo yao warejeshewe.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; Waziri wa Maliasili na Utalii wakati anahitimisha bajeti yake alisema mifugo hiyo itarudishwa mara moja; na Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokutana na kikao cha wafugaji wote nchini aliagiza mifugo hiyo wairejeshwe lakini sasa hivi...

SPIKA: Uliza swali Mheshimiwa Mpina ulishatoa maelezo marefu sana

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Spika, la kwanza kwamba Waziri anasema mpaka sasa hivi hajapata

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

orodha ya wananchi ambao wanadai mifugo lakini Waziri wa Mifugo ametembea...

SPIKA: Mheshimiwa Mpina tusikilizane. Sasa ni kipindi cha maswali na majibu; uliza swali

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Spika, swali la kwanza mifugo hawa.

SPIKA: Uliza swali.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Spika, si ndiyo nauliza sasa?

SPIKA: Hapana, unaanza na maelezo ambayo umeshaeleza kwa kirefu tuelewane vizuri, uliza swali.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Spika, swali ninaloliuliza hapa orodha ipo Wizarani na Waziri anayo orodha kwa nini anakwepa hapa kuwalipa hao wafugaji wanyonge ambao wameshashinda kesi mahakamani na kutudanganya hapa kwamba hiyo orodha hana?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mbunge wa Kisesa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi ni kwamba mpaka sasa hatujapata orodha ya wafugaji ambao wanalamika hawajarejeshewa mifugo yao. Kma ambavyo nimeeleza kwamba kesi inapopelekwa mahakamani sisi tunapeleka vielelezo tu lakini kesi inabaki kuwa ni chini ya hakimu, *DPP* na sisi tunakuwa kama mashahidi, kwamba tumekamata mifugo hii, baada yah apo hakimu ndio anayetoa hukumu. Aidha, hukumu inakuwa ni kurejeshewa hiyo mifugo kwa faini au mifugo kutaifishwa.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Nimesema endapo kama kuna mfugaji ambaye ana kesi ambayo inatudai sisi Wizara ya Maliasili na Utalii basi waje wizarani tutakaa pamoja tuichambue hiyo kesi na tutaweza kutekeleza kama Serikali.

SPIKA: Mheshimiwa Festo Sanga swali la nyongeza

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Spika, asante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Swali langu pale Makete tuna pori la Mpanga Kipengele ambalo linazunguka vijiji vya Ibaga, Ikovo, Kiimani na Kigala. Pori hili limegeuka ni mwiba kwa wananchi wa Makete kwa sababu mifugo yao imekuwa ikiingia na watu wanakamata lakini bikoni zimebekwa kwenye maeneo ya wananchi; na nililalamika hapa Bungeni na ukaniahidhi Mheshimiwa Waziri utakuja.

Je, ni lini Serikali itekwenda kuweka bikoni ili wananchi wangu wawe salama katika eneo hili?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, ahsante naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sanga Mbunge wa Makete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimtaarifu tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tulikuwa kwenye ziara ya Mawaziri nane ambao wanatatua changamoto hizi za migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie tu kwamba nitafika kama sio mimi basi ni Mheshimiwa Waziri kuhakikisha kwamba tunafafanua wapi mipaka ilipo ili wananchi waweze kuelewa na hatimaye tuendelee kushirikiana kulinda maeneo ya hifadhi.

SPIKA: Mheshimiwa Esther Midimu, swali la nyongeza.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. ESTHER L. MIDIMU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa vile Serikali inasema itawarudishia ng'ombe wao je, itakaporudisha itawalipa na fidia?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swal la nyongeza la Mheshimiwa Esther Midimu Mbunge wa Simiyu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, naomba nifafanue hapa nimesema hapa kwamba tunapokamata mifugo kesi zao tunazipeleka Mahakamani hukumu inakuwa kati ya Hakimu na sisi tunasimama pale kama mashahidi tu ambao tunaonyesha vielelezo. Kwa hiyo suala la kwamba tutarejesha mifugo ni pale ambapo Serikali itajiridhisha kwamba hawa wahalifu watakaoingiza mifugo yao kwenye hifadhi wanastahili kurejeshewa hiyo mifugo na tunapopeleka kesi Mahakamani tunakabidhi vielelezo vyote, kwa hiyo sisi hatukai na mifugo. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Hamis Mwagao Tabasam, swal la nyongeza.

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kule Sengerema katika Kisiwa cha Juma kuna ngedere wengi zaidi ya binadamu na wanavamia maeneo ya wananchi. Ni nini mstakabali wa kuondoa wale ngedere katika kisiwa cha Juma?

SPIKA: Mheshimiwa Tabasam hilo ni swal la msingi kabisa na ulipeleke ili aje alete majibu mahsus kwa swal lako muhimu sana hilo. Mheshimiwa Nicodemas Maganga.

MHE. NICODEMAS H. MAGANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuulizwa swal.

Naomba nimuulize Waziri wa Maliasili, kule Mbogwe kumekuwa na tabia ya Maliasili wanakamata watu

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wanapiga na kuua; je, miongozo inaruhusu kumkamata mtu kwenye Hifadhi na kumuua? Naoma nipate majibu ya Serikali. (*Makof/Vicheko*)

SPIKA: Mheshimiwa Maganga hilo nalo ni swali la msingi na umesema mambo mazito hapa kwamba watu wanaauawa huko peleka swali la msingi ili yaletwe majibu ya mahsus hapa, kwa sababu hatutaki kusikia hizo Habari za watu wanaauawa kwenye Hifadhi, peleka swali la msingi.

Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako. Tunaenda Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje Mbunge wa Viti Maalum sasa uliza swali lako.

Na. 24

Kuzuia ukatili na utumikishwaji wa watoto wakati wa ujenzi wa Bomba la Mafuta Hoima – Tanga

MHE. NUSRAT S. HANJE aliuliza:-

Je? Serikali ina mkakati gani wa kuzuia ukatali wa kijinsia na utumikishwaji wa watoto katika makambi yanayotarajiwu kujengwa ili kuwezesha ujenzi wa Bomba la Mafuta Hoima Tanga?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri *sorry*, nilikuwa sijakuona hapo. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha vitendo vya ukatili wa kijinsia na utumikishaji wa watoto vinakomeshwa katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo mradi wa bomba

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

la mafuta Hoima Tanga, kuititia MTAKUWWA Wizara yangu imejipanga kuimarisha na kuzijengea uwezo Kamati za Ulinzi na Usalama kwa watoto kwa vile Serikali itaendelea kutumia vyombo vyta dola kuhakikisha wale wote wanaotumikisha watoto na kufanya vitendo vyta ukatili wanachukuliwa hatua za kisheria. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Nusrat Hanje, swali la nyongeza.

MHE. NUSRAT S. HANJE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi nami niulize maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri alisema kuna ngazi mbalimbali ambazo zinashughulika na hayo, lakini wanaonaje sasa wakati huu wasianzishe jeshi la jamii kama lilivyo Jeshi USU kwa upande wa Maliasili, kwa ajili ya kuhakikisha kwamba jamii inalinda watoto wetu dhidi ya ukatili pamoja na wanawake? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili: Ni kwa nini sasa Serikali isiende kwenye shule zetu kwa ajili ya kuanzisha klubu za stadi za maisha na majukwaa ya stadi za maisha kwa ajili ya kuwajengea watoto wetu uwezo wa kujilinda wenyewe? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Nusrat kama ifuatavyo. Swali lake la kwanza kuhusu Jeshi Jamii; Wizara imejipanga na mpango kazi wa Taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto (MTAKUWWA) ili kuhakikisha kwamba wanakuwa na usalama. Mpango huu umejielekeza kuanzia ngazi ya vijiji hadi mkoa na kuhusisha vyombo vyta ulinzi na usalama katika kila eneo.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kuhusu jukwaa la watoto; Wizara yetu ina majukwaa ya watoto ambayo yanahimiza ulinzi na usalama. Pia yapo mabaraza na clubs

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

za watoto kuanzia shule za msingi, sekondari hadi Vyuo. Klabu hizi zinawafunza watoto na kuwaelimisha waweze kujitambua, kujielewa, kujiamini na kujieleza wakati wowote katika kujikinga na ukatili dhidi ya watoto. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Yustina Rahhi, swali la nyongeza.

MHE. YUSTINA A. RAHHI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Mkoa wa Manyara umeonekana kuwa ni mbili mbili katika ukatili wa jinsia na sababu kubwa ni kwamba waathirika bado hawana elimu ya kutosha kuhusu hatua za kuchukua:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutokomeza ukatili wa jinsia katika Mkoa wa Manyara? Ahsante. (*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

kuhusu swali la ukatili wa jinsia kwa watoto katika mkoa wako, Wizara kama nilivyoeleza imejipanga katika mpango wa Taifa kutokomeza ukatili wa jinsia (MTAKUWWA). Mpango huu unahusisha vijiji hadi mkoa.

Kwa hiyo, kuna Kamati katika kila mkoa ambazo zinahusisha usalama wa watoto na wanawake katika kuhakikisha tunatokomeza ukatili kwa watoto na tunapingga ukatili wa jinsia kwa wanawake na wananchi.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali hayo. Sasa tunaenda Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Fautine Engelbert Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni, sasa aulize swali lake.

Na. 25

Kupitia Gharama za Leseni kwa Wabunifu wa Apps za Huduma za Kifedha

MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapitia gharama za leseni kwa Wabunifu wa Apps za huduma za kifedha na kuwawezesha kutumia mifumo iliyopo?

SPIKA: Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Chande, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mifumo ya Malipo ya mwaka 2015 inazitaka kampuni zinazotaka kuendesha huduma za malipo kuwa na leseni ya kutoa huduma inayosimamiwa na sheria hiyo. Leseni hii hutolewa na Benki Kuu ya Tanzania mara baada ya kampuni kukamilisha taratibu zote za kupata leseni. Kampuni ikikamilisha taratibu zote, hutakiwa kufanya malipo ya leseni ambayo ni shilingi milioni 12 na hufanyika mara moja kila baada ya miaka mitano. Aidha, Sheria ya Mifumo ya Malipo inakataa kutoa huduma za malipo bila leseni na adhabu zake zimeainishwa kwenye vifungu vya sheria husika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mwenendo wa maombi ya leseni kutoka kampuni mbalimbali za huduma za malipo na kiwango cha uwekezaji wa kampuni hizo, ni maoni ya Serikali kuwa gharama za leseni kwa wabunifu wa App za huduma za kifedha zinaendana na mahitaji ya soko. Naomba kuwasilisha. (*Makof*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, swali la nyongeza.

MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE: Mheshimiwa Spika, nianze kwa ushauri mdogo kwamba Serikali iende ikaziangalie hizi gharama, bado ni kubwa sana na zinadumaza ubunifu. Maswali mawili yangu ya nyongeza; vijana wengi wamejajiri kuititia ubunifu na wengi wanafanyakazi na taasisi za nje, changamoto imekuwa ni malipo.

Je, ni lini sasa Serikali itaruhusu mfumo wa *pay poll* ili vijana hawa ambao wamejajiri na kufanya kazi za *consultancy* huko nje ya nchi waweze kupata malipo yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swalilangu la pili; tuna vijana wengi wabunifu ambao wanaandaa mifumo ya *software*. *Software* ambazo tunazinunua *online* hazitozwi *VAT*, lakini zile ambazo zinatengenezwa nchini, zinatozwa *VAT*. Ni lini sasa Serikali itafanya mapitio ili kuhakikisha kwamba wabunifu wa ndani ya nchi wanapata nafuu katika mifumo ambayo wanaitengeneza hapa nchini? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ndugulile kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kumpungeza sana Mheshimiwa Ndugulile kwa kiasi ambacho anapigania wananchi wa Jimbo la Kigamboni na Watanzania kwa jumla. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mfumo wa *Paypal* bado haujazuiliwa na unaendelea kutumika nchini. Mwaka 2016 wawakilishi wa *Paypal* walifika Benki Kuu ya Tanzania ili kupata taratibu zinazotakiwa katika kutekeleza huduma hiyo. Hata hivyo, Serikali ipo tayari kupokea maombi ya leseni kwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

sababu hawawezi kuendesha huduma hiyo bila kuwa na leseni. Serikali iko tayari kupokea leseni hizo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, swalı lake la pili, ni kweli kabisa. Naomba nikiri kwamba ni kweli huduma hii ya *software* au huduma za mtandao hulipiwa *VAT* ni suala la kweli kabisa kwamba lazima ilipiwe *VAT* na ni tofauti, yaani *VAT* ambayo inalipiwa kwa *software* ambazo zinatengenezwa nchini, zinakuwa na ongezeko hilo la thamani tofauti na ambazo wanana nua ndani ya mtandao *online*.

Mheshimiwa Spika, suala hili tayari utafiti umeshafanyika kwa kina na mapendekezo yake tayari. Nalihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba mapendekezo hayo yatawasilishwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023 mwaka huu. Ahsante. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Tarimo, swalı la nyongeza.

MHE. PRISCUS J. TARIMO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Makampuni mbalimbali ya simu yanatoa huduma za mikopo kupitia mitandao na riba zake ziko juu sana:-

Je, Benki Kuu inafanya nini kuhakikisha inasimamia huduma hizi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swalı dogo la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Benki Kuu ya Tanzania inapitia maombi yote ambayo yanaletwa na makampuni mbalimbali. Itakapo jiridhisha, basi itatoa leseni kwa kampuni yoyote ikizingatia masharti kwamba lazima waambatane au washirikiane na kampuni au taasisi ambayo ipo ndani ya nchi yetu. (*Makof*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 26

Sensa ya Mwaka 2022 Kusaidia Kupata Takwimu za Watu Wenye Ulemavu

MHE. KADIJA S. TAYA aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Sensa ya Watu na Makazi inajumuisha takwimu za watu wenye ulemavu na aina ya ulemavu?

SPIKA: Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibuu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, dodoso la sensa ya watu na makazi itakayofanyika nchini mwezi Agosti, 2022 limejumuisha maswali 10 yanayohusu hali ya ulemavu. Maswali hayo yataulizwa kwa watu wote ikijumuisha umri, jinsi na ulemavu na hivyo kutoa takwimu za hali ya ulemavu nchini. Kupitia sensa hiyo, ni matarajio yetu kuwa Serikali itapata takwimu rasmi za hali ya ulemavu nchini kwa maeneo ya kiutawala, jinsi, hali ya ndoa, kiwango cha elimu, ajira na viashiria vingine muhimu vilivyoainishwa katika dodoso la sensa.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuungana na Serikali kuwashimiza wananchi kushiriki kikamlifu katika Sensa ya Watu na Makazi itakayofanyika Agosti, 2022 - Sensa kwa Maendeleo, jiandae kuhesabiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya, swali la nyongeza.

MHE. KHADIJA S. TAYA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali na kuonyesha namna gani Serikali imejipanga kwa kutumia hizi takwimu.

Mheshimiwa Spika, kwa kutumia takwimu zilizopita, za 2010 na sasa hivi tuko 2022/2023 kwenye maandalizi ya bajeti ya Mpango wa mwaka 2022/2023.

Je, Serikali imejipangaje kupitia Wizara yake hii ya Fedha na Mipango kuondoa matatizo ya watu wenye ulemavu; kwa sababu hii Wizara ndiyo ambayo ina bajeti Kuu ya Serikali? Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilisha Sensa yetu tukapata takwimu sahihi na kuweza kujua idadi ya watu wenye ulamavu na aina ya ulemavu ambayo ipo nchini, tutaandaa mipango rasmi na kutoa vipaumbele ambavyo vinaweza kuingizwa hadi katika bajeti yetu kwa maslahi ya wananchi wote.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mama Samia Suluhu Hassan haiko tayari kuacha kundi lolote nyuma, makundi yote yataainishwa katika vipaumbele vya nchi hii na kwa maslahi ya umma. Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo, tunakushukuru. Tunaelekea Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, Mbunge wa Ngara, sasa aulize swali lake.

Na. 27

**Serikali Kukamilisha Vituo vya Polisi vya Nyamagana,
Keza na Djululigwa**

MHE. NDAISABA G. RUHORO aliuiliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Vituo vya Polisi vya Nyamagana, Keza na Djululigwa vilivyojengwa na wananchi?

SPIKA: Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Jumanne Sagini, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, Mbunge wa Ngara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua na kuthamini jitihada na michango ya wananchi katika kujenga vituo vya Polisi nchini. Vituo vidogo vya Polisi vya Nyamagana, Keza na Djululigwa ambavyo viko Wilaya ya Ngara, ni vituo vilivyojengwa kwa nguvu za wananchi. Tathmini imefanyika na kubalni kuwa kiasi cha shilingi 125,000,000 kitahitajika ili kugharamia uwekaji wa mfumo wa umeme na maji, kupiga plasta, kuweka sakafu, dari, milango, madirisha, samani na kupaka rangi. Serikali kuititia Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na wadau inatafuta fedha ili kuweza kumalizia kazi ya ujenzi huo.

SPIKA: Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, swalii la nyongeza.

MHE. NDAISABA G. RUHORO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwa kuwa maeneo yote aliyoyataja hayana vituo vya Polisi: Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yupo tayari kutupatia gari liendelee kuimarisha ulinzi eneo hilo huku

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

tukiwa tunasubiri kujengwa kwa vituo hivyo? Hilo ni namba moja.

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa eneo la Ngara liko mpakani na changamoto ya ulinzi na usalama ni kubwa, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kuambatana nami tukaone changamoto hizo sambamba na kutatua mgogoro wa Rusumo Magereza na wananchi wa kijiji cha Magereza? Ahsante sana.

SPIKA: Sasa Mheshimiwa mbona umeunganisha mambo mawili? Hapo unataka akujibu hilo la tatu au aishie la pili? Kwamba ataongozana na wewe, halafu mtajua huko mnakokwenda maana umeongeza na cha tatu hapo. Maswali unaruhusiwa mawili tu.

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu kwa maswali mawili kati ya hayo matatu aliyouliza.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:
Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ruhoro kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu kusaidia gari kwa ajili ya kuimarisha usalama na ulinzi wa raia na mali zao, kama ilivyojibwa siku tatu zilizopita na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi hapa, Wizara kweli itapata magari 78 mwishoni mwa mwezi huu ambapo tathmini itafanyika kuona Halmashauri yenye changamoto kubwa iweze kuzingatiwa ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Ngara na hasa ukizingatia iko mpakani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuambatana naye, niko tayari kuongozana naye wakati wowote nafasi itakapopatikana hususan baada ya Bunge hili ili kuweza kuona changamoto zake na kuzifanya kazi. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, swali la nyongeza.

MHE. STANSLAUS H. NYONGO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Wilaya ya Maswa hasa katika Mji wa Maswa hatujawahi kujengewa Kituo cha Polisi toka tumepata uhuru mwaka 1961:-

Je, ni lini Serikali itajenga kituo chake katika Wilaya ya Maswa na nyumba za maaskari?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Stanslaus Nyongo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba kweli ziko wilaya hasa Wilaya kongwe kama Maswa hazina vituo vya polisi kwa maana ya ngazi ya *OCD*. Wizara ina mpango wa kuzijengea vituo vya polisi vya ngazi ya wilaya, wilaya zote ambazo hazina vituo hivyo kwa kutegemea upatikanaji wa fedha. Nami nafahamu wilaya hii kwa sababu pia ina mapori kule na hifadhi, wanahitaji kituo hiki, hivyo tutaipa kipaumbele katika mpango huo. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Florent Kyombo, swali la nyongeza.

MHE. FLORENT L. KYOMBO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi. Wananchi wa Kata Kakunyu, Wilaya ya Misenyi ambapo ni mpakani mwa nchi yetu na Uganda, wamejenga kituo cha polisi mpaka kuezeka.

Je, ni lini sasa Serikali itawaunga mkono kumalizia kituo hicho wapate huduma za kipolisi? Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kyombo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema, wananchi wamejenga kituo, wanahitaji msaada wa kumalizia. Hatua watakayoanza ni kutathmini kiwango gani cha fedha kinatakiwa ili kukamilisha kituo hicho ili kuona kama tunaweza tukatumia sehemu ya fedha ya tuzo na tozo kwa ajili ya ku-support vituo hivi ambavyo viko mpakani. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Tarimba Abbas, swali la nyongeza.

MHE. TARIMBA G. ABBAS: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa Jimbo la Kinondoni lina watu wengi sana na mahitaji ya usalama wa watu hao pamoja na mali zao ni mkubwa, hasa ikitiliwa maanani nyumba ziko karibu karibu sana:-

Je, Serikali haioni kwamba sasa ni wakati muafaka kuruhusu vituo vidogo vya Polisi vinavyofungwa saa 12 vifanye kazi masaa 24 ili kuweza kusaidia usalama katika maeneo hayo? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Abbas kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunatambua wingi wa watu kwa wananchi wa Kinondoni na umuhimu wa kuwa na vituo vidogo vya Polisi katika maeneo mbalimbali. Tutatathmini kwa sababu ili Kituo Kidogo cha Polisi kiweze kufanyakazi saa 24, vinahitaji rasilimaliwatu; na muundo wa kituo kile kuweza kuhifadhi silaha na mambo kama hayo. Kwa hiyo, tutatathmini kuona mahitaji, tutashauriana na Mheshimiwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Abbas kuona namna gani tuvifanye viweze kutoa huduma saa 24. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Mwanaisha Ulenge, swali la nyongeza.

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi ya swali la nyongeza. Kwa kuwa Jiji la Tanga limetanuka na lina makazi mapya mengi, sasa ni lini Serikali itajenga vituo vya Polisi katika maeneo ya Kange Uzunguni, Kange Mbugani, Mwahako na Mwakidila? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Mwanaisha hilo ni swali la nyongeza unataka akujibie kata zote hizo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Nailbu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwanaisha Ulenge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunatambua ukubwa wa Jiji la Tanga na kwa kweli limepanuka sana na umuhimu wa kuimarisha ulinzi na usalama katika maeneo hayo ni mkubwa, kwa hiyo tutashauriana na uongozi wa Polisi wa Mkoa ili kuwajumuisha wadau akiwemo Mheshimiwa Ulenge na wengine wadau wema kuanza kujenga Vituo vya Polisi kwenye maeneo haya yaliyopanuka ili kuimarisha ulinzi kwenye maeneo hayo. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Assa Makanika swali la nyongeza.

MHE. ASSA N. MAKANIKA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Tuna Kituo cha Polisi katika Wilaya yetu ya Kigoma DC, Kituo cha Polisi cha Mkuti, ukiangalia matukio mengi sana ya kihalifu yanafanyika katika eneo lile.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Je, ni lini Serikali itaweba kumalizia Kituo kile cha Polisi katika hali iliyopo? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:
Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Makanika, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nipo tayari kufuatana na Mheshimiwa Makanika baada ya Bunge hili ili kuona mahitaji ya kituo hicho kwa maana ya kufanya tathmini, kuona fedha zinazohitajika ziweze kutengwa katika bajeti zetu zinazofuata. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Michael Mwakamo, swali la nyongeza.

MHE. MICHAEL C. MWAKAMO: Mheshimiwa Spika, Mji wa Mlandizi unakua kwa kasi na pale Mlandizi kuna majengo kwenye Kituo cha Polisi yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi. Je, ni lini Serikali itaweka nguvu za Serikali kusaidia nguvu za wananchi kumaliza nyumba zile? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:
Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Michael, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tutaomba uongozi wa Polisi wa Mkoa ilipo Wilaya ya Mheshimiwa ili iweze kufanya tathmini kujua kiwango cha fedha zinazohitajika kwa ajili kukamilisha ili tuweze kuingiza kwenye mpango na hatimaye kiweze kumalizwa. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba, swali la nyongeza.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Katika Jimbo la Shinyanga mjini Kituo Kikuu cha Polisi kilikuwa na hali mbaya jambo ambalo uongozi wa Polisi waliamua kujenga kwa fedha zao za ndani, lakini kituo hicho kipywa kilichojengwa bado hakijakamilika. Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza fedha katika kituo hicho ili kiweze kukamilika? Nashukuru. (*Makof!*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salome Makamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchakavu wa Kituo cha Polisi Shinyanga Mjini kinachohitaji ukarabati, tutafanya tathmini ili kuona kiwango cha fedha zinazohitajika kuwezesha ukarabati huo kufanyika, tuingize kwenye mpango wa bajeti katika miaka inayofuata.

SPIKA: Mheshimiwa Pallangyo, swali la nyongeza.

MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO: Mheshimiwa Spika, nakushuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Kituo cha Polisi katika Kata ya King'ori na kukarabati Kituo cha Polisi kilichopo Ngarenanyuki katika ...

SPIKA: Hayo ni maswali mawili, Mheshimiwa.

MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

SPIKA: Hayo ni maswali mawili. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, jibu swali moja.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Pallangyo, kama ifuatavyo:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, tupo tayari kushirikiana na Mbunge na wadau wengine wa Kata ya King'ori kuona kiwango cha ujenzi kinachotakiwa kumaliziwa ili tuweze kutengea fedha kituo hicho kiweze kukamilishwa. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Mohamed Said Issa, Mbunge wa Konde.

Na. 28

Ukarabati wa Kituo cha Polisi – Konde

MHE. MOHAMED SAID ISSA aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya ukarabati wa Kituo cha Polisi cha Konde katika Wilaya ya Micheweni?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Saidi Issa, Mbunge wa Konde, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uchakavu wa Kituo cha Polisi cha Konde ambacho jengo lake lilijengwa wakati wa ukoloni. Tathmini kwa ajili ya ukarabati wa kituo hicho imefanyika na kubaini kwamba kiasi cha fedha Sh.42,000,000/= kinahitajika ili kugharamia ubadilishaji paa, kubadilisha mfumo wa umeme, maji safi na maji taka, kuziba nyufa, kubadilisha dari na kupaka rangi. Ukarabati huo utafanyika kulingana na upatikanaji wa fedha. Aidha, Serikali inawahamasisha wadau walio tayari kushirikiana na Makamanda wa Polisi wa Mikoa na Wilaya katika kuboresha vituo vya Polisi vilivyo kwenye maeneo yao.

SPIKA: Mheshimiwa Mohamed Said Issa, swali la nyongeza.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. MOHAMED SAID ISSA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwanza, niishukuru Wizara kwa kuweza kutenga fedha kwa ajili ya matengenezo ya Kituo cha Konde, lakini swali langu la nyongeza ni kwamba katika Kituo cha Polisi cha Konde pia kuna nyumba za askari ambazo wanatumikia katika kituo kile. Je, Serikali ina mpango gani wa kuweza kuzikarabati?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, pia katika maeneo ya Konde mbele kuna Kituo cha Polisi kinaitwa Matangatuani ambacho ni kituo muhimu sana kinatumika kwa ajili ya ulinzi wa mali, lakini pia na uhalifu kwa sababu Jimbo la Konde ni la mpakani, Je Serikali ina mpango gani wa kuweza kukikarabati Kituo hicho cha Matangatuani?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mohamed Saidi Issa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu kukarabati nyumba za askari zilizo kwenye kituo hicho, hili ni jambo muafaka kabisa tunapokuwa tunafanya tathmini hizi gharama zinazohitajika kwa ajili ya ukarabati wa kituo tutazingatia nyumba hizo ili ziweze kuingizwa katika mpango wa ukarabati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili la kuboresha kituo cha polisi kilicho mpakani, jina sijalipata vizuri Matanga...

MHE. MOHAMED SAID ISSA: Mheshimiwa Spika, Matangatuani

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, hivyo hivyo Matangatuani, tutakifanyika tathmini kituo hicho ili kuona kiwango cha fedha

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

zinazohitajika kwa ajili ya ukarabati wake, tuweze kukiingiza katika mpango wetu wa ukarabati. Nashukuru. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Kuchauka, swali la nyongeza.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Wilaya ya Liwale haina Kituo cha Polisi na kwa kuliona tatizo hilo nimetoa fedha shilingi 10,000,000 kutoka kwenye Mfuko wa Jimbo kwa ajili ya kuanza ujenzi. Je, Serikali inatusaidiaje ili kuimarisha kituo cha Polisi cha Wilaya ya Liwale? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kuchauka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge Kuchauka kwa kuchangia shilingi 10,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi Liwale, naomba nitoe ahadi kama nilivyosema katika swali lililopita kwamba maeneo yote ya Wilaya ambayo hayana Vituo vya Polisi ni mpango wa Serikali kuona kwamba Wilaya hizo zinapata Vituo vya Polisi, hivyo tutafanya tathmini kuona kiwango cha fedha kinachohitajika ili kushirikiana nae tuweze kukamilisha Kituo cha Polisi Liwale. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mussa Sima, swali la nyongeza.

MHE. MUSSA R. SIMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Singida Mjini ni Mji ambao unakuwa kwa kasi sana na maeneo mengi hayana vituo vya Polisi hali inayopelekea askari wetu kusafiri kwa umbali mrefu. Je, Serikali haioni haja sasa umefika wakati wa kuwaongezea walau fedha ya mafuta ili waweze kufanya kazi yao vizuri ya usalama wa raia?

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Mussa Sima, Mbunge wa Singida Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba Makao Makuu ya Mikoa yetu mingi kwa kweli yanapanuka sana na kuhitaji huduma za kipolisi kwa maana ya kuwa na magari, kuelekea kwenye maeneo hayo kuwahudumia wananchi. Niseme kama itakavyokuja kusomwa bajeti yetu hapa mwaka huu Rais wa Awamu ya Sita, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, ameongeza fedha kwenye majeshi yetu ikiwemo Jeshi la Polisi ili kuimarishe shughuli za kiulinzi ikiwemo doria na mambo kama hayo. Kwa hiyo Wilaya ya Singida na Manispaa ya Singida ni moja ya Wilaya zitakazonufaika na ongezeko hilo la Bajeti. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Charles Kajege, swalii la nyongeza.

MHE. CHARLES M. KAJEGE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nina swalii moja; kwa vile Vituo vya Polisi vya Kibara, Bulamba na Kisorya vinatumia nyumba za wenyeji kufanya kazi zake. Je, ni lini Serikali itajenga vituo hivyo? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Kajege, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Kajege kwa juhudini zake za kuimarishe huduma za ulinzi wa wananchi ikiwemo kuhamasisha wananchi kushiriki kujenga vituo vya Polisi vya

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Bulamba na Kisorya. Napenda kumuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba tutafanya tathmini ya kiwango cha fedha zinazohitajika kukamilisha vituo hivyo ili viweze kuingizwa katika mpango na bajeti itakayosomwa siku zijazo. Nashukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, swali la nyongeza.

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya ukarabati mkubwa katika Kituo cha *Central*/kilichopo Jimbo la Tabora Mjini? (*Makof!*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Vituo Vikuu vya Polisi vya Mikoa kama anavyosema *Central* Tabora vinahitaji kufanyiwa tathmini kwa ajili ya kuona mahitaji ya fedha yanayohitaji kwa ajili ya kuwezesha ukarabati huo kufanyika. Naomba nimuhidi Mheshimiwa Mwaifunga na bahati nzuri Tabora ni eneo nililoanza kazi, tutashirikiana na Mheshimiwa Mbunge na Mbunge wa Jimbo ili kufanya tathmini ya kiwango cha fedha zinazohitajika ili ukarabati huo uweze kufanywa. (*Makof!*)

SPIKA: Mheshimiwa Twaha Mpembenwe, swali la nyongeza.

MHE. TWAHA A. MPEMBENWE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili kuuliza swali la nyongeza. Wilaya ya Kibiti inafahamika maarufu sana kwa jina la Kanda Maalum, sasa ni upi mpango wa Serikali kujenga Kituo cha Polisi ambacho kina hadhi ya Kanda Maalum katika Wilaya ya Kibiti? Ahsante. (*Makof!*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:
Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Twaha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunatambua ulianzishwa Mkao wa kipolisi Kanda Maalum ya Kibiti, ukaanza kwa utaratibu wa dharura kwa kutumia ofisi ya *OCD* zilizokuwepo miongoni mwa Mikoa mipyä ya kipolisi ambayo itajengewa majengo yake ni pamoja na Mkao huu wa Kanda Maalum ya Kibiti. Kwa hivyo Mheshimwia Mbunge asubiri kadri tutakapokuwa tunapata fedha, Kibiti itapewa msisitizo maalum. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. (*Makofi*)

Sasa tunaelekea Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 29

Ujenzi wa Barabara ya Igawa hadi Tunduma

MHE. SUMA I. FYANDOMO aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Igawa hadi Tunduma kwa kiwango cha lami?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa *Engineer Msongwe*, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Suma

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Ikenda Fyandomo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Igawa hadi Tunduma yenyе urefu wa kilometra 218 ikiwa ni maandalizi ya kufanya ukarabati kwa kiwango cha lami. Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ilikamilika mwezi Agosti, 2021. Aidha, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umejumuisha barabara ya mchepuo katika Jiji la Mbeya kipande cha Uyole – Songwe *Bypass* yenyе urefu wa kilometra 48.9.

Mheshimiwa Spika, Serikali itafanya ukarabati na upanuzi wa Barabara ya Igawa hadi Tunduma kwa awamu, ambapo awamu ya kwanza itahusisha upanuzi wa barabara kutoka njia mbili kuwa njia nne kwa sehemu ya Uyole – Ifisi yenyе urefu wa kilometra 29 ili kupunguza msongamano katika Jiji la Mbeya. Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi zinaendelea na inatarajiwa kazi itaanza mapema katika mwaka wa fedha 2022/2023.

Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ukarabati wa sehemu iliyobaki pamoja na kujenga Barabara ya Mchepuo ya Uyole – *Songwe bypass*. Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, swalı la nyongeza.

MHE. SUMA I. FYANDOMO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pia nashukuru kwa majibu ya Serikali kwamba imejiandaa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa *bypass*, hata hivyo nina maswali ya nyonge. La kwanza, je, ni lini wananchi ambaao wanakaa Uyole mpaka Ifisi watalipwa fidia zao ili kupisha ujenzi wa barabara hiyo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swalı langu la pili, naomba kwa uzito wake, kuanzia Uyole mpaka Mbeya Mjini mpaka kufika *airportile* barabara haina hata *service road* kwa maana hiyo

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mabasi, bajaji, maguta, malori pamoja na *ambulance* ambazo zinapeleka wagonjwa wa rufaa Mbeya, lakini usiombe kama unakwenda *airport*...

SPIKA: Uliza swali Mheshimiwa.

MHE. SUMA I FYANDOMO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kama unakwenda *Airport* unaweza ukapaki gari pembeni ukapanda bajaji ama bodaboda ili kuwahi kule inakuwa shughuli...

SPIKA: Mheshimiwa, uliza swali.

Mheshimiwa Spika, sasa je, ni lini Serikali itatafuta Mkandarasi kwa haraka ili kuweza kuepusha ajali zinazotokea mara kwa mara kwa ufinyu wa barabara kutoka Igawa mpaka...

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Mbeya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nianze na suala la fidia kabla ya kuanza ujenzi wa barabara hii, fidia italipwa kwa wananchi ambao watapisha ujenzi huu. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jiji la Mbeya kwamba Serikali italipa fidia kabla ya kuanza ujenzi wa barabara hii.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge lakini pia na Mheshimiwa Spika ambaye najua hili jiji ni jiji lako kwamba, ni kweli barabara hii ambayo Serikali imeamua kuchukua hatua za haraka sana kulingana na ukweli kwamba msongamano ni mkubwa.

Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba hatuna barabara hizi za kupaki bajaji na pikipiki lakini pia tunatambua

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kwamba barabara hii ndio inayopitisha mizigo karibu asilimia zaidi ya 50 ya mizigo inayotoka Bandari ya Dar es Salaam kwenda DRC, Zambia na Malawi na ndio maana Serikali imechukua jitihada na hatua za haraka kuhakikisha kwamba barabara hii inapanuliwa na wakati inafanya *design* ni pamoja na kutengeneza hayo maeneo ambayo yatakuwa ni ya kupaki malori, mabasi na bajaji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kazi hii itafanyika na tayari tupo kwenye hatua za manunuzi ili tunavyoanza tu Julai kazi ianze ya ujenzi huu pamoja na hizo *parking* ambazo Mheshimiwa Mbunge amezisema. Kwa hiyo naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Mbunge hivyo. Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, siku ya Jumanne Iiliulizwa swalii la nyongeza la kuhusu hii barabara na majibu yako yalisema, ujenzi unaanza mwaka huu wa fedha ambao ni 2021/2022, majibu ya msingi hapa yanaonesha kwamba katika mwaka wa fedha 2022/2023, Sasa kwa sababu hapa umenitaja nimeona uliweke vizuri hilo tuwe tunajua 2021/2022 au 2022/2023. (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba niliweke vizuri suala hili. Kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, tutaanza ujenzi kwa maana ya kupeleka mkandarasi *site* mara tunapoanza mwezi Julai, utekelezaji wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, lakini kwenye jibu la msingi tunasema taratibu za manunuzi zimeshaanza kwa maana ya kutafuta Mkandarasi, kusaini zabuni na kuanza kufanya tathmini. Kwa hiyo, ujenzi tunasema tayari tumeshaanza kwa sababu hizo hatua zimeanza na kwamba tutakapoanza tu mwaka mpya Mkandarasi anakuwa yupo *site*. Lakini taratibu za manunuzi zimeshaanza na tayari tumeshatangaza. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Catherine Magige swalii la nyongeza.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. CATHERINE V. MAGIGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa barabara ya Kona ya Kiseriani ambayo inaungana na barabara ya Arusha *bypass* imekuwa kero kubwa sana na kusababisha msongamano wa magari katika Jiji la Arusha. Tumeona Mkandarasi amepatikana na muda wa kujienda umekwisha.

Je, ni lini sasa mkandarasi ataanza kazi ya kujenga barabara hii katika Jiji la Arusha?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, sijamsikia vizuri barabara aliyotaja Mheshimiwa Mbunge, ningeomba arudie.

SPIKA: Mheshimiwa Catherine Magige ni barabara gani uliyotaja?

MHE. CATHERINE V. MAGIGE: Mheshimiwa Spika, barabara ya Kiseriani katika Jiji la Arusha ambayo inaungana na barabara ya *Arusha bypass*.

SPIKA: Haya ahsante sana.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Catherine Magige Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara zote za *bypass* lakini barabara zote za Mji wa Arusha, ziko kwenye mpango wa kujengwa. Kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ziko kwenye taratibu mbalimbali za manunuzi ikiwa ni pamoja na barabara ya Arusha kwenda Kisongo, Arusha kwenda Usa River, lakini pia na barabara ambayo inaunganisha barabara ya *Bypass* ya Arusha Kusini ambayo inaunganisha Tengeru kwenda Usa River. Kwa hiyo,

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba taratibu zinaendelea za kuzijenga hizo barabara. Ahsante. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Hamis Shabani Taletale swali la nyongeze.

MHE. HAMISI S. TALETALE: Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza Serikali ni lini itaanza kujenga barabara yetu ya Bigwa – Kisaki?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Taletale Mbunge wa Morogoro Vijiji, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara ya Bigwa – Kisaki ni kati ya barabara 22 ambazo ziko kwenye taratibu mbalimbali za manunuzi ili ujenzi wa barabara hii muhimu ya kutoka Bigwa – Kisaki, kwenda Bwawa la Nyerere uanze. Kwa hiyo, muda wowote taratibu zikikamilika, barabara hii itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Daniel Sillo Baran swali la nyongeza.

MHE. DANIEL B. SILLO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali moja. Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Babati, Galapo hadi Orkesumet kwa kiwango cha lami?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Sillo, Mbunge wa Babati Vijiji, kama ifuatavyo: -

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, barabara hii ni barabara muhimu ambayo tayari imeshakamilishwa kufanyiwa usanifu wa kina na Serikali inaendelea kutafuta fedha ili barabara hii ianze kujengwa kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, mara Serikali itakapopata fedha, barabara hii itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Mariam Nyoka, swali la nyongeza.

MHE. MARIAM M. NYOKA: Mheshimiwa Spika, nashukuru.

Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya Majengo, Ruvuma, Subira kwenda Mpitimbi kwa kiwango cha lami?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa...

SPIKA: Mheshimiwa Mariam Nyoka!

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, Mariam Nyoka, barabara ya.....!

Mheshimiwa Spika, sikumsikia barabara aliyoitaja. (*Makofi*)

SPIKA: Haya Mheshimiwa Mariam Nyoka mtajie barabara ya Ruvuma hiyo.

MHE. MARIAM M. NYOKA: Mheshimiwa Spika, nashukuru ni barabara ya Majengo, Ruvuma, Subira kwenda Mpitimbi kwa kiwango cha lami.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Mariam Nyoka, Mbunge wa Viti Maalum Mkao wa Ruvuma, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, barabara hii Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kufanya kazi ya usanifu wa kina ili ianze kujengwa kwa kiwango cha lami.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwenda tutaenda sasa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, Mbunge wa Momba, sasa aulize swalii lake.

Na. 30

Migogoro ya Mikataba ya Minara ya Simu Kata ya Kapele

MHE. CONDESTER M. SICHALWE aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itatatua migogoro ya mikataba ya minara ya simu kati ya kampuni za simu na Kijiji cha Namuchinka Kata ya Kapele?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, majibu.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI aliibuu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, Mbunge wa Momba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Namchinka kina minara miwili iliyojengwa na Kampuni ya Tigo na Halotel. Minara

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

hiyo imesimikwa katika ardhi inayomilikiwa na watu binafsi na siyo kijiji. Hivyo, watoa huduma hulipa malipo ya pango la ardhi kwa wamiliki hao kulingana na makubalino katika mikataba waliyoingia.

Mheshimiwa Spika, kuititia Bunge lako Tukufu nitoe maelekezo kwa watoa huduma wote kuhakikisha kuwa wanashirikisha Serikali ya Wilaya na Kijiji wanapotaka kujenga minara ya mawasiliano katika Kijiji husika ili kuepuka migogoro inayoweza kujitokeza ya namna hii. Vilevile, watoa huduma wahakikishe waingie mikataba ya ulinzi wa minara na Serikali za Vijiji ili kuwa na ulinzi wa uhakika katika minara ya mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, nitoe rai kwa wananchi kuwa wazalendo na kutoa ushirikiano kwa watoa huduma wakati wa ujenzi na ulinzi wa mlundombini ya mawasiliano ili kuhakikisha huduma za mawasiliano zinakuwa endelevu kwenye maeneo yetu.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, swali la nyonge.

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, nimepokea majibu ya Serikali na ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa ufanuzi. Swali langu la kwanza lipo katika mfumo wa ombi, je, Naibu Waziri anaonaje kama atatafuta siku ya *weekend* katikati ya Bunge hili la Bajeti aongozane nami kwenda Jimboni Momba, kunisaidia kutoa ufanuzi kwa wananchi wa Kijiji cha Namchinga ili waweze kuelewa?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, je, Serikali inaonaje kama itatoa mwongozo kwa makampuni haya ya simu ili kuhakikisha wanapolipa pango la ardhi kwa Mmiliki lakini watoe na *percent* kwenye Serikali ya Mamlaka husika, aidha, Serikali ya Mtaa au Kijiji ili kutoa mgongano wa maslahi kwenye jamii.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri nisikilize kwanza, hili la kwanza mimi nakulinda hapa maana amesema *weekend*, maana yake lazima iwe ndani kipindi hiki, kwa hiyo hilo nakulinda. Kwa hiyo wewe unaweza kufanya kipindi hiki kama unao muda au baada ya Bunge, kwa sababu mimi mwenyewe nakutaka hapa Dodoma. Sasa usije ukasema nimetumwa huko na Mbunge nilimjibu Bungeni. Kwa hiyo, hilo una uhuru wa kutoa jibu kama una nafasi kipindi hiki au utakwenda baada ya Bunge kuahirishwa. Majibu kwa maswali hayo.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, Mbunge wa Mombasa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa anayoifanya. Siku mbili tatu hizi tumekuwa tukiongea na Wenyeviti wa Vijiji, Wenyeviti wa Mtaa na Mwenyekiti wa Kata katika Kijiji hiki cha Namchinga. Kwa kweli anafanya kazi kubwa sana na hakika Jimbo la Mombasa wamepata Mbunge kwelikweli.

Mheshimiwa Spika, vilevile kuhusu suala la kwenda kutoa elimu, naomba nilipokee na tutakaa tutajadili kadri nafasi itakavyoweza kupatikana tutaweza kufanya hivyo. Nakuhakikisha Mheshimiwa Mbunge tutafanya kulinganana na nafasi itakayopatikana.

Mheshimiwa Spika, jambo jingine kuhusu suala la kutoa *percent* kwa wananchi wetu na dhana kubwa ambayo inasababisha kwamba wananchi wanahitaji kupewa *percent* kuna dhana imejengeka kwamba minara hii iliyopo katika maeneo ya wananchi ina mionzi ambayo inawaathiri sana wananchi kiasi kwamba wanataka hii *percent* kama fidia.

Mheshimiwa Spika, Wabunge na wananchi wote, nikuhakikishie kwamba minara hii kiwango ambacho kimewekwa katika minara yetu, kiwango cha chini ni *Volt*

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Saba *per meter*, lakini minara yetu nchi nzima iko chini ya Volt Saba maana yake ipo kati ya Tatu mpaka Nne. Kwa hiyo, suala la mionzi naomba huu mtazamo tuutolee elimu ya kutosha ili wananchi wafahamu.

Mheshimiwa Spika, vilevile kwa Sheria ya Mwaka 2009, iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2020 inasema kabisa kwamba makampuni ya simu yatatoa asilimia 0.3 kwenye Halmashauri kulingana na minara inayotumika katika Halmashauri husika. Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu hayo unaweza kurejea kwenye kiti chako.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nilete matangazo kwenu kwanza ni tangazo la kukaimu nafasi ya Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni, nimeletewa taarifa hapa kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu hayupo Dodoma, hivyo hayuko pia Bungeni na kwa hivyo, amempa hiyo nafasi kukaimu Mheshimiwa Dkt. Dotto Mashaka Biteko, ahsante sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, pia tunao wageni mbalimbali ambao wako hapa Bungeni siku ya leo. Kwanza ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge, tunae mgeni wa Mheshimiwa Patrobass Katambi, ambaye ni Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Ndugu Diana Paul Chando, huyu ni kijana Mtanzania ambaye ni Balozi wa Vijana Umoja wa Afrika, Kitengo cha Siasa, Ulinzi na Usalama anayewakilisha nchi 14 upande wa Afrika Mashariki, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Christine Mnzava, ambao ni rafiki zake kutoka Mkoani Shinyanga, hawa ndugu Richard Raphael Masele na Ndugu Ally Nassor Khalfan. Karibuni sana. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Neema Mwandabila ambao ni ndugu zake kutoka Jijini Mbeya, na hawa ndugu Emmeliana Mwandabila, ndugu Judith Mzumbwe na ndugu Naomi Mwandabila. Karibuni sana. Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Cosato Chumi ambao ni wataalam wa ardhi kutoka *AFROTAI Group Company Limited* kutoka Jiji Dar es Salaam na hawa ni Ndugu Anold Ignatus Makeka na Ndugu Joseph Ngoja. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Kwanza ni wageni 141 ambao ni washereheshaji kisima cha mafanikio kutoka Mikoa mbalimbali nchini wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Ester Kimweri, karibuni sana. (*Makofi*)

Hawa Washereheshaji inaonekana wamejipanga, mambo yao ni mazuri sana, karibu sana Wabunge wenu wako hapa wanawawakilisha vizuri. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni wawili kutoka kampuni ya *Gml and Eddy's Ltd.* ya Jiji Dodoma na hawa ni Ndugu Dativa Herman na Ndugu Bahati Shirima, karibuni sana.

Tunao wanafunzi 100 na walimu wa *St. Gasper Primary School* toka Jijini Dodoma wakiongozwa na Mwalimu Mkuu wa shule hiyo Mwalimu Abel Misanga. Karibu sana Bungeni. Tunao wanafunzi 50 na walimu saba kutoka *St. John Bosco Primary School* ya Mkoani Mara, karibuni sana Bungeni, karibuni sana Dodoma. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matangazo niliyokuwa nayo hapa mbele tunaendelea na ratiba yetu.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mwongozo wa Spika.

MHE. MRISHO M. GAMBO: Mheshimiwa Spika, jambo la dharura.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ni nani aliyesema jambo la dharura?

MHE. MRISHO M. GAMBO: Meshimiwa Spika, ni mimi.

SPIKA: Mheshimiwa Mrisho Gambo.

MHE. MRISHO M. GAMBO: Mheshimiwa Spika, nasimama kwa Kanuni ya 54(1) ambayo inasema baada ya muda wa maswali kuisha, Mbunge yeoyote anaweza kutoa hoja kwa Shughuli za Bunge kama ilivyooneshwu kwenye orodha za shughuli ziahirishwe ili Bunge lijadili jambo halisi la dharura...

SPIKA: Mheshimiwa Gambo, huna haja ya kusoma Kanuni kila mtu anayo. Kwa hiyo, wewe nenda kwenye hoja yako halafu tuitazame.

MHE. MRISHO M. GAMBO: Mheshimiwa Spika, sote tunafahamu kwamba sasa hivi bei za bidhaa zimepanda sana nchi nzima, bidhaa kama za mafuta ya kula, *diesel*, *petrol*, vifaa vya ujenzi, kama saruji, nondo na mabati lakini pia vyakula kama nyama, unga wa ngano na viungo vimepanda sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, haya mambo ni mambo ya msingi sana kwa maisha ya binadamu ya kila siku. Tumemsikia Mheshimiwa Rais ametoa maelekezo kwamba Waheshimiwa Wabunge tunatakiwa tuende kwenye Majimbo yetu tukaelezeed jambo hili.

Kwa hiyo, ili tuweze kupata uwezo na weledi wa kuelezea jambo hili, naomba kutoa hoja ya kuahirishwa Shughuli za Bunge ili tujadili jambo hili la dharura ambalo lina maslahi ya Taifa.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, Waheshimiwa Wabunge, tuskilizane, namuona Mbunge mmoja kule nyuma amesimama huko nyuma. Kanuni ya 54 imempa fursa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, kusimama na kusema jambo ambalo ye ye anaona ni la dharura na kwamba lijadiliwe.

Sasa masharti ya Kanuni yetu ya 54 na pia ukisoma pamoja na Kanuni ya 55, Kanuni ya 55 inaeleza masharti ya jumla kuhusu jambo la dharura, kwa hiyo, jambo linaloweza kujadiliwa hapa ndani lazima liwe limekidhi vigezo vilivyowekwa kwenye Kanuni ya 55. Sasa Kanuni ya 55 inaanza kwa kusomwa hiyo ya 54 na Fasili ya (4) inaeleza kwamba ikiwa Spika ataridhika na hayo maelezo yaliyotolewa na jambo hilo lililoelezwa, likiwa ni la dharura. (*Makofi*)

Sasa kwa masharti ya Kanuni 55 inataka jambo ambalo litahesabiwa ni la dharura ni lile ambalo utaratibu wa kawaida wa kufanya kazi haliwezi kushughulikiwa, ndio linaitwa la dharura ili sasa Bunge liweze kupata nafasi ya kulijadili na kupata fursa ya kushauri yule anayetakiwa kufanya maamuzi fulani au wakati mwingine Bunge litaishia kuazimia jambo fulani na kwa hivyo Serikali itatakiwa kutekeleza kwa sababu hakuna utaratibu wa kawaida wa kufanya hivyo.

Kwa hiyo, fasili ya 54(4) mimi sijaridhika kama hilo jambo ni la dharura, kwa hiyo utaratibu wa kawaida wa kushughulikia kupanda kwa bei za vitu ufuatwe na Kaimu Kiongozi wa Shughuli za Serikali upo hapa, Serikali mchukue hoja hiyo aliyoisema Mheshimiwa Gambo ya kupanda kwa bidhaa mbalimbali ambazo wananchi wanazitumia kila siku basi muangalie namna ya kulishughulikia hilo jambo kama ambavyo huwa mnashughulikia mambo mengine ambayo bei huwa zinapanda mnatafuta namna ya kughulika nayo, hili nalo mlisughulikie kwa utaratibu wenu wa kawaida.

Waheshimiwa Wabunge alisimama pia Mheshimiwa Timotheo Mzanva akisema kuwa anaomba mwongozo maana yake kuna jambo ambalo limetokea hapa Bungeni mapema na anataka Kiti kimpe mwongozo.

Mheshimiwa Timotheo Mnzava.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 76.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kipindi cha maswali na majibu, wakati Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii akijibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Sanga aliahidi kwamba mgogoro ule utashughulikiwa wakati Kamati nane itakapokwenda kwenye eneo hilo kutoa taarifa.

Mheshimiwa Spika, nimesimama kuomba mwongozo wako, kwamba tangu 2019, Bunge la Kumi na Moja, Bunge hili limekuwa likisubiri kwa hamu na kwa muda mrefu, taarifa ya Kamati ya Mawaziri nane, kuhusu migogoro ya ardhi, kati ya vijiji na hifadhi. Na mwaka jana Kamati yako illiomba Serikali ipeleke taarifa ya Kamati hiyo, Waziri wa ardhi aliyekuwepo aliahidi atapeleka Kamati ikasubiri kwa masaa mawili baadaye wakasema kuna mambo bado hayajakaa sawa. Lakini sasa hivi tunawaona Mawaziri wanaenda mikoani; wameenda Morogoro, wameenda Tanga na humu ndani mara kadhaa inarudiwa kwamba Kamati ya maridhiano inafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, ningependa kupata mwongozo wako, je, ni sahihi kuendelea kuahidiwa kwamba migogoro inayoshughulikiwa kati ya Mawaziri nane, ilhali Bunge lako halina taarifa hiyo, wala Kamati ya Kisekta inayoshughulikia ardhi haina taarifa hiyo, hatuoni kwamba ni sahihi Bunge au kupitia Kamati ya Kisekta tupate taarifa hii ili tuishauri Serikali kabla ya kwenda kwenye vijiji kupeleka taarifa ambazo zinapelekwa kule kwa wananchi wetu. Nakushukuru. (*Makofii*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Timotheo Mzanva kwa mujibu wa kanuni 76 akitaka nitoe mwongozo kuhusu jambo ambalo limetokea mapema hapa Bunge wakati Mheshimiwa Naibu Waziri Mary Masanja, Naibu Waziri Maliasili na Utalii akijibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Festo Sanga, ambalo lilikuwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

linauliza kuhusu mgogoro ambao upo huko kwenye Jimbo Lake la Makete.

Mheshimiwa Naibu Waziri wakati akijibu swalii hilo alisema kwamba mgogoro utatatuliwa punde kwa sababu Kamati ya Mawaziri nane, inayo majibu ya huo mgogoro na itakapopata fursa ya kwenda huko basi huo mgogoro utakuwa umetatuliwa.

Sasa mheshimiwa Timotheo Mzanva, anataka kujua kama hilo jambo linaruhusiwa ama haliruhusiwi, kwa sababu ndiyo kanuni inachosema. Lakini ametoa maelezo kwa kirefu kidogo kuashiria kwamba hiyo taarifa ambayo huwa inapelekwa huko kwenye maeneo mbalimbali, mikoa mbalimbali, majimbo mbalimbali na hao Waheshimiwa Mawaziri, Kamati inayohusika ya Bunge hailifahamu jambo hilo. (*Makof!*)

Sasa kwa sababu yeye ameomba mwongozo wangu ili niseme kama inaruhusiwa au hairuhusiwi, kwa sababu Mheshimiwa Naibu Waziri yeye alikuwa anajibu swalii liliolizwa. Kwa hiyo, inaruhusiwa kwamba anajua taarifa ipo na anajua majibu na hivyo amejibu; kwa hiyo kwa mwongozo inaruhusiwa. Sasa kwa jambo la ziada kwamba ambalo kimsingi halijatokea hapa lakini Mheshimiwa Timotheo Mzanva ameeleza jambo la msingi kabisa kwamba Mawaziri hawa huko nyuma walishaambiwa walete hiyo taarifa na hiyo taarifa haikuja kwenye Kamati inayohusika.

Sasa Mheshimiwa Kaimu Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, taarifa hiyo kabla hamjaipeleka huko na mmeshaipeleka maeneo mengi, na nia njema, kwamba mnataka kutatua migogoro ya ardhi kati ya wananchi na TANAPA, maeneo mengine ni kati ya wananchi na taasisi nyingine za Serikali, yote mnayafanya. Kwa sababu hiyo kazi mmeshaifanya na hayo maamuzi tayari mmeshayachukua, na mnaenda sehemu mbalimbali kuyapeleka hayo maamuzi ya Serikali, basi ni jambo jema kabisa sisi Wabunge kwa maana ya Kamati inayohusika ipate hiyo taarifa. (*Makof!*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ufanye utaratibu ule wa kawaia kabisa ambao huwa tunawasiliana, kwa maana ya ofisi ya Waziri Mkuu ambayo wewe unakaimu hapa leo kama kiongozi lakini na ofisi yetu ya Bunge kwa kufuata zile taratibu za kawaida kabisa, tupate zile taarifa ambazo hazina siri yoyote. Kwa sababu mkishaenda kule mnazitoa hizo taarifa kwa hiyo hata Wabunge hapa kwa maana ya Kamati hii ya Ardhi, Maliasili na Utalii hakuna siri ambayo itakuwa inatolewa hapo. (*Makofii*)

Kwa hiyo, hilo limekuja kwako mahususi na nadhani mtalifanyia kazi kwa wakati ili Kamati ipate fursa ya kufahamu hiyo taarifa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hayo mambo mawili yaliyojitokeza hapa tutaendelea na ratibu iliyo mbele yetu. Katibu!

NDG. HUSSEIN ATHUMAN, *ndc* – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu
kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023**

(Majadiliano Yanaendelea)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na majadiliano ya hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, na hapa nimeshaletewa orodha ya wachangiaji wengi ambao wangependa kuchangia siku ya leo. Tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Joseph Kasheku Musukuma, atafuata Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo ajiandae.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niwe mchangiaji wa kwanza katika hoja ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza sana
Mehshimiwa Rais, Mama Samia kwa kazi kubwa na nzuri
aliyofanya kwenye majimbo na katika nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri Wabunge tutakubaliana kwamba kazi imefanyika, tumetoka kukagua miradi mikubwa na midogo hakuna mahali ambapo tumekuta mradi haujapelekewa fedha; hii ni hongera kubwa sana kwa mama na imedhihirisha kweli kwamba kinamama mkiwezeshwa mnaweza wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu, mimi ninatoka Kanda ya Ziwa, tulikuwa na miradi mikubwa sana kule mradi wa Daraja la Busisi, Hospitali ya Kanda ya Chato, Hospitali ya Musoma...

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Musukuma kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Matiko.

T A A R I F A

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Musukuma, kwamba tunashukuru anapo-*appreciate* kuhusu uongozi wa kinamama lakini najua wanawake tunaweza bila kuwezeshwa. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Musukuma nadhani alikuwa ananyoosha pale mwanzo, naamini ulikusudia kusema hiki ambacho amekisema Mheshimiwa Esther Matiko.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, akina mama ni mama zangu walionilea, siwezi kubishana nao. Ni kama alivyosema, na iwe hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, miradi yote hii mikubwa nilioitaja, imepelekewa fedha na inafanyika na inaendelea

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kukamilishwa. Hongera sana kwa Mama Samia na aendelea kuchapa kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa ushauri. Njua Mheshimiwa Rais, ana majukumu mengi sana na ndiyo maana tukawa na mawaziri na Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, mnapopeleka fedha nyingi kwenye majimbo yetu, inahitaji ufuatiliaji wa karibu wa watu wenye maamuzi; namaanisha mawaziri. Sasa kumekuwa tabia ambazo nilizungumza hata juzi, ile kwamba Waziri anataka kutembelea halmashauri tano mpaka sita kwa siku, hii haina ufanisi mzuri katika kutusaidia kwenye fedha mnazozipeleka kwenye majimbo yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni vizuri mkaenda *specifically* kwenye halmashauri moja mkasikiliza siku nzima, mkaona miradi na kusikiliza matatizo ambayo yako kwenye ile halmashauri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba kumshauri Waziri Mkuu, ule utaratibu wake wa kupelekewa kero na kwenda kutatua moja kwa moja kwenye halmashauri, ningeomba aendelee nao. Ukipikiliza Wabunge wengi humu hawawezi tu kutamka moja kwa moja, kila Mbunge ana matatizo kwenye halmashauri yake, na ukileta Mawaziri unaambiwa mchakato unaendelea, tunaunda Tume, tume hazitoi majibu. Inakuwa kama tunapeleka fedha halafu kama hatuwezi kuzisimamia; bado Watanzania hawatatuelewa.

Mheshimiwa Spika, nimeona mtandaoni tangu jana au juzi, kuna *clip* inazunguka ya Mheshimiwa Mpina; na ninayezungumza ni mimi usiingie kwenye kumi na nane. Na ile *clip* imechukua sehemu ambayo imeashiria mimi nimezungumza kwenye mchango wangu, halafu imeunganishwa ikawepo kwenye hotuba ya Mheshimiwa Mpina.

Mheshimiwa Spika, mimi kweli nililalamika sana kuhusiana na Bwawa la Mwalimu Nyerere kulingana na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

taarifa ilioletwa na Waziri wa Nishati, na ni mjumbe wa Kamati. Baada ya yale majibu sikukata tamaa nilifuata utaratibu kwenda kwa Mwenyekiti, na Mwenyekiti na Wajumbe tukakubaliana tukakuomba kibali cha kwenda kuukagua mradi.

Mheshimiwa Spika, mimi ni balozi, naweza kusema ule mradi umeenda mara mbili ya ulivyokuwa umeachwa na Hayati Dkt. Magufuli, nimeenda kukagua mara nne. Kwa hiyo, tuisitengenezeane ajali. Na sisi kama Kamati kwenye taarifa yetu mtaisikiliza mtaiona. Matatizo tuliyoyagundua si mradi, ni wataalam walimdanganya Waziri.

Mheshimiwa Spika, sasa nikisema mimi naomba ninukuliwe mimi, na mtu akitaka kutumia hansard yangu nina haki yangu kama Mbunge nisichukuliwe kwenda kutengeneza uzuri mtu.

Mheshimiwa Spika, mimi ni muathirika mkubwa sana wa Mheshimiwa Mpina. Nikimuangalia Mheshimiwa Mpina na hotuba aliyoitao; mimi basi yangu mimi Mheshimiwa Mpina amei-cease mpaka leo inaozea kituoni, ilikutwa na Samaki watatu, hebu angalia samaki tatu... (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Musukuma hebu subiri kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, hoja iliyoko mezani, ndio kanuni zetu zinavyosema, sasa Mheshimiwa Musukuma usitupeleke mahali ambapo kila mtu atakuwa analeta hapa hoja za mambo ambayo yametokea kati yake ye ye binafsi na mtu mwengine kwa sababu ninyi wote ni Wabunge. Kama ulivyosema hapa lingkuwa hilo jambo limetokea hapa ndani ningeshughulika nalo kwa sababu kanuni zetu zina utaratibu hapa ndani. Lakini sasa ukisema hivyo maana yake naye Mheshimiwa Mpina asimame aanze kukujibu, aaa, sio utaratibu wetu (*Makofi*)

Kwa hiyo, jiekeleze kwenye hoja iliyoko mezani kama kuna tofauti iliyo tokea kwenye *clip* ambayo hajatokea hapa ndani huo utaratibu mwengine kwa sababu kanuni zetu

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

zitakuwa hazitupeleki huko, tuende kwenye hoja iliyoko mezani.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: *Message delivered.*
[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]

SPIKA: Sasa Mheshimiwa Musukuma, Taarifa zetu Rasmi za Bunge lazima zikae vizuri, futa hayo maneno yako ya *message delivered*.

MHE. DKT. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, naya futa.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa najaribu kuielea Serikali, kwamba mambo haya ni vizuri tukayaangalia vizuri, kwa sababu sisi Wabunge tunapokuwa tunalalamika, huwa wanaona wenzetu kule chini kama tunawaonea. Lakini unavyowatendea wenzio ukitendewa na wewe uvumilie msumari uingie.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba kushauri. Kama alivyozungumza Mbunge wa Arusha, Mheshimiwa Gambo, kwamba kuna mfumuko mkubwa wa bei. Hili ningeomba kutoa ushauri wangu kwenye Serikali kwamba ukiangalia leo bei ya mafuta tunanunua mpaka 3,000 huko Kijiji.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba Serikali ichukue suala hili kama suala la dharura, tuone namna, hata kama ni kupitisha bajeti ya dharura. Serikali yetu kwa sasa inakopesheka, tumefanya hivyo mara nyngi, ilishuka bei ya korosho Serikali tukakaa hapa tukaipitishia tukaenda kurescue suala la korosho, sasa kuna mfumuko wa bei ya mafuta (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, najua kuna fedha ambazo tuliweka kwa ajili ya miradi ya maji, tuliweka kwa ajili ya miradi ya barabara, tunaweza tukaona namna kama ni kiasi gani kimebakia tukaziondoa hata tukaenda kukopa ili tufidie.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, kwa hali ya kawaida, mafuta shilingi 3000, na tunakoelekea yatapanda mpaka 3200 Serikali isikae kimya, kazi ya Serikali ni kuwalinda watu wake. Sasa hili lionwe kama suala la dharura ili kama kuna uwezekano, walete *agenda* yoyote ya dharura hapa tuweze kutafuta fedha yoyote tuweze kushuka mfumuko wa bei hasa kwenye mafuta.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la *TARURA*, kila Mbunge anaitegemea *TARURA* hapa. Ukienda ofisi ya *TARURA* hapa Makao Makuu utapishana na Wabunge 10, 20 kwa siku. Lakini kumekuwa na shida sana kwenye *TARURA*, ukisikiliza Waziri alienda pale wakasema wanaunda Tume hakuna mwelekeo.

Mheshimiwa Spila, leo sisi tunakuwa Wabunge wengine wawilli kwenye halmashauri moja. wameondoa meneja wa kila halmashauri wameweka meneja wa Wilaya. Lakini unamuondoa yule uliyemshusha unambakisha pale pale na cheo ni kimoja, na wote walikuwa ni mameneja; kazihazienda wilayani huko.

Mheshimiwa Spika, na ukiangalia, *TARURA* ndilo tegemeo letu kila mtu hapa ndani; tunatoa fedha nyngi; na leo Rais kawaongeza zaidi ya bilioni 900 lakini fedha walikuwa nazo, hata kipindi mwaka wa kwanza wamebakira na bilioni 72, mwaka wa pili bilioni 100, mwaka wa tatu bilioni 130, hizi ni ripoti *CAG*. Kwanini sasa tusione namna ya kuiboresha *TARURA* ikakaa vizuri ili hizi fedha zisibaki kama bakaa zitumike kwa sababu ukihoji humu kila mtu ana barabara mbovu. Lakini fedha zinabaki na bado tunaendelea kuwaongeza.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu wa mwisho, naomba sana; Mhesimiwa Shabiby alizungumza juzi hapa, suala la mafuta kuagiza kwa *bulk procurement*, hili suala hata kama tungeongeza hela bado mafuta hayawezi kushuka. Biashara huria ndio muarobaini wa hili suala, aruhusiwe kila mtu alete mafuta, kazi yetu Serikali tukusanye kodi, kazi yetu Serikali ipime TBS mafuta ni mazuri. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, mafuta yako mengi sana huko ya njia za panya yanini tungeshusha bei za mafuta. Sisi hatuna sababu ya kuanza kusimamia mafuta ya warabu, sisi tunachotaka ni mafuta yashuke bei. Tukiruhusu kila mtu alete mafuta watu wataunga na mitaji, wataleta mafuta ya wanavyojua wenyewe, sisi tutakusanya kodi na tutasimamia suala viwango, mafuta yatashuka bei. Nashukuru. (*Makof!*)

SPIKA: Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo, Mheshimiwa Jumanne Kibera Kishimba ajiandae.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika hotuba iliyoko mbele ya Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze napongezi kwa ofisi ya Waziri Mkuu kwa kazi nzuri sana ambayo wameifanya. Tumeona utekelezaji wa miradi mbalimbali ambayo hivi punde tumetoka kuikagua katika maeneo tofauti tofauti katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kipekee kupitia hotuba yangu ningependa pia nitoe mchango katika eneo la ukusanyaji wa mapato, nikitoa pongezi kubwa sana kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) kwa namna ambavyo wameendelea na zoezi zuri kabisa la kukusanya mapato bila kutumia mitutu ya bunduki wala bila kufunga biashara za watu. Hii inaonyesha wazi dhamira ya Mheshimiwa Rais, kwamba yeye ana *mentality* ya kibashara na ana amini kwamba kupitia biashara ndivyo tunaweza kupata kodi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, ningependa kuchangia eneo la mfumuko wa bei lakini nikigusia eneo zima la mafuta. Kama ambavyo mzungumzaji wa mwisho ametoka kusema, ni kweli mafuta yanapopanda bei, maana yake kila kitu kitakwenda kupanda bei; kwa sababu gharama za usafiri, usafirishaji mitambo na kadhalika kwenye maeneo yote ya udhalishaji inategemea nishati ya mafuta.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, sasa ni nini muarobaini wa hili jambo? Kwa sasa kwa hali tuliyokuwa nayo ambayo imetokana na vita, baina ya Ukraine na Russia, namna pekee ambayo inaweza kutusaidia ni Serikali kuweka ruzuku katika eneo zima hili la uagizaji wa mafuta ili angalau sasa kuweza *ku-stabilize* bei.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mfumo wa uagizaji mafuta kwa pamoja, eneo hili ningeomba sana kwa ridhaa yako uwasiliana ikiwezekana na Wizara ya Nishati, angalau tupate semina ya uelewa wa pamoja. Hatuwezi tukakwepa mfumo wa *bulk procurement system* ambao ndio unaotufanya leo tunatamba kuwa na *storage* ya mafuta ya siku 36. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kama tungeruhusu kila mmoja aagize mafuta kwa wakati wake, tusingeweza kuwa na *control* hii ambayo leo tunayo na mfumo huu umeanzishwa mwaka 2011 kupitia Bunge lako Tukufu likiwa ni sehemu la mwanzo wa mfumo huu.

Mheshimiwa Spika, mfumo huu umetusaidia sana kudhibiti baadhi ya mambo. Maana yake nini; kwenye mfumo huu wa uagizaji wa pamoja wafanyabiashara wa mafuta wanakutana na viwanda ambavyo vinasambaza mafuta kwa maana ya *refineries*; tunaangalia bei shindani, na kwenye mamfuta vitu vitatu ni muhimu sana kuzingatia; kwanza *reliability, availability, na affordability*, hivi ndivyo vitu vitatu vya msingi vya kuangalia wakati wa kuagiza mafuta. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunapokwenda kupata sasa *tonnage* watu wote tunapeleka oda zetu kwa yule ambaye ameshinda tenda na anasafirisha mzigo wote kwa wakati mmoja. Anaposafirisha mzigo kwa wakati mmoja maana yake hata *shipping cost* zinakuwa zimeshuka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, zamani wakati kila mmoja alipokuwa anaagiza kutoka kwenye kila kichochoro chake maana yake hata *demurrage pale* bandarini ilikuwa

inaongezeka kwa sababu unashubiri mafuta yako katika meli kumi tofauti tofauti. Lakini leo tunaagiza mzigo katika meli moja kubwa inaleta, hata kama ni *metric ton* 600,000 zinatua kwa pamoja; *demurrage* imeshuka kutoka dola 30 hadi 45 kwa siku, sasa hivi dola moja mpaka tatu kwa siku. Kwa hiyo, haya ni mapinduzi makubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa mfumo huu ili tuelewe, ndiyo maana nasema lazima tupate semina ya kuelewa hili jambo vizuri. Leo nchi zote zinazotuzunguka hapa zimejunga katika mfumo wa *bulk procurement system*. Uganda wamo, Burundi wamo, Rwanda wamo, Malawi wamo, Zambia wamo na DR Congo wimeingia. Hata nchi Mauritius imekuja kujifunza namna bora ya kuingia katika mfumo huu wa manunuvi ya pamoja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema, makampuni yanayozalisha mafuta duniani yanafahamika. Kwa hapa kwetu tuna *Trafigura* au *DAX Energy*; ya kizawa, tuna *GBP* ambapo mmiliki ni mwenyeji kutoka Kigoma, anashusha katika Bandari ya Tanga. Kuna *Hans Energy*, mwenyeji wa Mara, wakati mwagine anashusha katika Bandari ya Dar es Salaam, wanapata hizi tenda. Kwa hiyo, hakuna shida ya kuwa na wasiwasi kwamba eti kuna meli sijui zimepaki Bandarini huko kwenye bahari zina mafuta. Huko ndiko tulikotoka wakati ule tulipokuwa tunaletewa mafuta machafu, ambayo yalikuwa hata ukiweka kwenye magari, kila siku magari yanakufa pampu barabarani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tumetoka huko, hakuna *businessman* mzuri, *smart* akaweka meli kwenye bahari. Biashara yote inafanyika kwenye mtandao na hii ni kama zilivyo kwenye *Bureau De Change*, bei ya mafuta kila siku ukiingia kwenye mtandao unaiona. Nasi *source* yetu ni *Arab Gulf* ndiko tunakochukulia mafuta zaidi. Ukiangalia kwenye mtandao pale unaona bei ya mafuta kila siku kama ilivyo kwenye *stock exchange*, hakuna namna kwamba eti utakuta meli imekaa kwenye *deep sea* huko ambayo siyo ya wizi au siyo ya maharamia iletwe kwenye nchi ambayo ni ya kistaarabu kama Tanzania. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, ninachoshauri, Serikali iwe na mpango mkakati madhubuti wa kuongeza *storage facility* katika *TIPER*. Sasa hivi *TIPER* tunapokea mafuta lakini bado kwa hali hii ambayo tunayo, ni lazima tuongeze *storage capacity* ili tuweze kuwa na ujazo wa kuwa na mafuta hata wa miezi mitatu mpaka minne. Ila katika mfumo mzima wa kodi, mfumo huu ndiyo unaotusaidia zaidi. Kwa sababu gani? Pale ambapo makampuni haya ya mafuta yanapotoa *order zao*, tayari *TRA* anajua kabisa kwamba kampuni 'X' itaingiza *metric ton* kiasi fulani na kodi yetu tutakusanya kiasi fulani. Hata kama yatapita kwenye mita, lakini tayari mchakato wa awali wa kujua kwamba Serikali inapata kodi kiasi gani unajulikana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, niwaambie, mafuta ndiyo bidhaa pekee ambayo inalipiwa kodi zote kabla hata hayajaanza kutumika. Inapoanza kuwa *discharged* kutoka kwenye meli kwenda kwenye matenki yale ya kuhifadhia, tayari pale kodi zote za Serikali zinakuwa zimelipwa. Kwa hiyo, huo mfumo umetusaidia sana kama Taifa na ningeomba sana wala tusiuguse. Kama kuna maboresho yanaweza kufanyika, lakini kwa tunavyokwenda mpaka sasa uko vizuri sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningetaka kuchangia ni *MSD*. Bohari ya Madawa haifanyi kazi vile inavyopaswa. Tuna shida kubwa sana katika Bohari ya Madawa kwa maana kwamba Halmashauri nydingi tumeweka fedha pale ili tuletewe vifaatiba na vitendanishi, lakini hivi tunavyozungumza ni zaidi ya miezi sita hakuna vifaa ambavyo vinapatikana katika hospitali zetu. Sasa jukumu la Bunge ni kusimamia na kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Spika, tunaombwa Bunge lako Tukufu lielekeze Serikali kama *MSD* kazi imewashinda, basi atafutwe mtu ambaye anaweza kwenda kusimamia ile kazi vizuri. Huko nyuma tumeona walikuwa na mpango mzuri sana. Walikuwa na mpango mzuri kiasi kwamba waliwahi kupata *tender* ya kusambaza dawa katika nchi zote za *SADC*, lakini nadhani kwa haya yaliyotokea hapa nyuma na kushindwa kufanya

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kazi zao kwa ufanisi, hata ile kazi ambayo ingeweza kuingizia Taifa kipato sasa imekwenda kwenye eneo likinge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo, nakushukuru sana. Ahsante sana kwa nafasi hii. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, atafuatiwa na Mheshimiwa Jomanne Kibera Kishimba na Mheshimiwa Cosato David Chumi, ajandae.

MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO: Mheshimiwa Spika, nami nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri sana alioitoa jana hasa kwa matumizi yake ya picha na video ambayo yalionesha wazi kwamba kazi kubwa inaendelea katika sehemu mbalimbali hapa nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, bahari mbaya Mheshimiwa Waziri Mkuu jana alisahau au aliamua kuacha kwa makusudi tu, moja ya mafanikio muhimu sana alipokuwa anazungumzia eneo la utamaduni, sanaa na michezo. Ukweli wenyewe ni kwamba, kwa hakika mwaka huu tena Yanga itachukua ubingwa wa Ligi Kuu ya NBC. Kwa hiyo, alitaja pale mengi lakini hili akaliachaka, sasa nimeona nilitaje. (*Makofii/ Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, mwaka huu na mwezi huu wa Aprili, nchi yetu inaadhimisha miaka 100 ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Kama angekuwa hai, mwezi huu angefikisha miaka 100. Ni fursa nzuri kwa nchi yetu kuendelea kutafakari mchango wa Mwalimu, lakini pia ni fursa nzuri kuendelea kutafakari historia ya nchi yetu; miaka 60 ya Uhuru wa Tanganyika na miaka 58 ya Muungano wetu wa Tanganyika na Zanzibar. Siku ya Jumatatu tarehe 29 Julai, mwaka 1985, Mwalimu alitoa hotuba yake ya mwisho katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwa Rais. Katika hotuba ile alitumia nafasi ile kuipitisha nchi katika mafanikio yaliyopatikana katika uongozi wake na katika changamoto ambazo zilijitokeza. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, moja ya jambo zuri sana katika hotuba ile, ni ukweli kwamba Mwalimu alikuwa muwazi na mkweli kwa makosa ambayo aliyafanya katika uongozi wake. Alitaja mengi, lakini muhimu yanajitokeza wazi. Moja, alikiri na alitumia neno la Kiingereza, alisema: “*it was a major error* kufuta Mamlaka za Serikali za Mitaa.” Kosa la pili ambalo aliliita: “*the other most serious mistake,*” ilikuwa ni kufuta Vyama vya Ushirika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kosa la kwanza tuliiyahisha yeye mwenyewe akiwemo mwaka 1982 kwa Bunge hili kutunga Sheria ya Kurejesha Mamlaka ya Serikali za Mitaa na tukaingiza kwenye Katiba ibara 145 na 146. Pia tumefanya marekebisho makubwa tangu wakati huo hasa mwaka 1996 - 1998 pale ambapo tuliamua kuanza kutekeleza *Policyya D By D (Decentralization by Devolution)* maarufu kama Sera ya Ugatuaji wa Madaraka Mikoani.

Mheshimiwa Spika, sera hii ina mambo makubwa mawili. Kwanza ni kuhamisha majukumu ya kusimamia matumizi ya fedha za maendeleo na watumishi kutoka Serikali Kuu kwenda Serikali za Mitaa. La pili, tuliona kabisa kwamba huduma za jamii ili ziweze kuwa endelevu; zingekuwa tu endelevu kama wananchi wangeshiriki kikamilifu katika kubuni kwa maana ya kuibua miradi, kushiriki kwenye utekelezaji wake na kusimamia pale ambapo imeshakamilika.

Mheshimiwa Spika, kwa maoni yangu, tuna mambo matatu ya kusahihisha katika eneo hili la *Local Government*. Kwanza ni kuhusu mahusiano kati ya Serikali Kuu na Serikali ya Mitaa. Uksoma ile *document*, mahusiano yanayotarajiwu kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa ni mahusiano ya kiuishauri na kiuwezeshaji; kwamba Serikali Kuu itaishauri na kiuwezesha *Local Government*.

Mheshimiwa Spika, zimetoka tathmini za wataalam, tena *report* imetoka juzi tu ya wataalam wetu hapa nchini, wanatueleza; na uhalisia Wabunge wanafahamu. Uhustiano uliopo kati ya *Local Government* zetu na Serikali Kuu hasa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI ni wa kimaelekezo; kwamba kazi kubwa ya Serikali Kuu ni kuelekeza mamlaka zile na mamlaka kutekeleza. Kwa hiyo, siyo ushauri. Hivyo, ile dhana ya kwanza ya kuipa mamlaka Serikali za Mitaa inapotea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo ni muhimu, ni kiwango kidogo cha ushirikishwaji wa wananchi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Tulisema wananchi washiriki kwenye kuibua na kutekeleza miradi ya maendeleo. Kwa sasa kwa kweli ukifuatilia kwa karibu, na tathmini zinaonesha hivyo, wananchi wengi wamekuwa wapokeaji na washangilaji wa mafanikio ya miradi ya maendeleo. Ushiriki unazidi kupungua.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu ni lile ambalo pia kwenye hotuba ya Mwallimu amellzungumza. Kwa wakati wake aliona kwamba changamoto na sifa zote zilikwa zinaelekezwa kwake. Ni kwamba changamoto zote ni kwake na zikitokea sifa za mafanikio zinaelekezwa kwake. Jambo hili halikumpendeza na akalikemea. Naomba ninukuu maneno yake aliyojasema. Alisema kwa Kiingereza: "*our President is important, but he is not Tanzania. The Vice President and the President of Zanzibar are important, but they are not Tanzania. We; all of our people organized together, are Tanzania.*" (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nasisitiza kwamba ni muhimu kwa wananchi kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa miradi ya maendeleo na mafanikio yanayopatikana. Pia pale ambapo mafanikio yanapatikana ni muhimu sana wananchi waonekane kwamba ni sehemu ya mafanikio. Ni muhimu sana Halmashauri zetu zionekane kwamba ni sehemu ya mafanikio.

Mheshimiwa Spika, haiwezekani mradi wa maendeleo utekelezwe Kakonko halafu sifa zote ziende Serikali Kuu, sifa zote ziende kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, sifa zote ziende kwa Waziri Mkuu, sifa zote ziende kwa Mheshimiwa Rais, siyo sahihi. Lazima utukufu wa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mafanikio pia ugawanywe ili ile *sense of ownership* iwepo miongoni mwa wananchi. Kwa sababu wanapoona kuwa miradi tumetekeleza, tumesifiwa sisi, mafanikio ni yetu, ile *sense of ownership* inakuwepo. Vilevile changamoto zikitokea, haiwezekani changamoto zote zimetokea, tumwelekeze mtu mmoja au watu wawili. Lazima tuwe na *sense of ownership* ya changamoto na mafanikio. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu la kurekebisha ni lile ambalo limejitokeza. Tumesema tunatekeleza Sera ya Ugatuaji, lakini ukweli ni kwamba hii inaitwa *devolution*. Wataalam wa *Local Government* sasa wanasema kinachoendelea siyo *devolution*, isipokuwa ni *deconcentration*, kwa maana umemega madaraka kidogo yakashuka kule chini. Nami naita ile ni ugutuaji, siyo ugatuaji ni ugutuaji. Turudi kwenye sera yetu ya msingi ya ugatuaji. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, eneo la mwisho ambalo nataka kuchangia kwa sababu kengele ya kwanza imegonga, ni eneo hili ambalo Mheshimiwa Waziri Mkuu amelieleza kwenye hotuba yake ukurasa wa 78 mpaka 83. Ni hoja kuhusu upandaji wa bei za bidhaa na hatua ambazo Serikali inazichukua; nami naunga mkono zile hatua ambazo amezieleza pale ikiwemo kudhibiti wafanyabiashara wasipandishe bei holela. Pia ameeleza vizuri sababu za mfumuko wa bei na bei ya mafuta kupanda.

Mheshimiwa Spika, maelezo ni mazuri, lakini maelezo peke yake hayatoshi. Muhimu sana kwa Serikali ni kwamba Serikali inachukua hatua gani kuwapunguzia wananchi makali ya maisha kutokana na kupanda kwa bei? Hili ni jambo la msingi. Sote tunajua bei zimepanda katika hali ambayo siyo ya kawaida. Chukua mfano, kati ya Aprili mwaka 2020/2021 bei ya mafuta ilipanda kwa wastani wa shilingi 36, lakini Aprili, 2021/2022 hii ya juzi, imepanda kwa shilingi 738. Siyo kiwango cha kawaida cha upandaji wa bei ya mafuta. Sote tunatambua kwamba siyo kwa sababu yetu au Serikali, lakini hoja ya msingi kwa Serikali ni kwamba, inachukua hatua gani kuwapunguzia wananchi makali?

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Waingereza wana msemo unaosema, *desperate times calls for desperate measures.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, maoni yangu ni kwamba tuko katika kipindi ambacho siyo cha kawaida na Serikali lazima ichukue hatua ambazo siyo za kawaida. Ushauri wangu hapo ni kwamba Waziri wa Fedha na Mipango na Kamati yetu ya bajeti, haraka iwezekanavyo wakae waangalie katika bajeti yetu ni wapi tunaweza kuchukua hatua za kusaidia?

Mheshimiwa Spika, mapendekezo yangu ni kwamba katika zile *levy*, shilingi 792 ambazo zinakusanya moja kwa moja kama *Levy* kwenye mafuta, Kamati ya Bajeti inaweza ikashauri tukachukua shilingi 300/= mpaka shilingi 400/=, tukaondoa kwa muda mfupi kwa miezi mitatu au minne tukitarajia kwamba mwezi Julai mpaka Agosti, kwa jinsi wataalam wanavyosema, hali itarudi kama kawaida. Tukifanya hivyo, tutakuwa tumempunguzia mwananchi ukali wa maisha. Hizo fedha ambazo zinapungua kwenye miradi ya maendeleo, sasa hivi Serikari yetu bahati nzuri inakopesheka, ikope ili miradi ya maendeleo isisimame. Hayo ndiyo mapendekezo yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, narudia tena, *desperate times calls for desperate measures.* Hatupo katika hali ya kawaida, lazima Bunge lako lichukue hatua ambazo siyo za kawaida. Inapofika wakati wananchi wanaumia, msemajji wao mkubwa katika nchi ni Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Bunge hili haliwezi kukaa kimya; haliwezi kuridhika tu na maelezo ya Serikali kwamba maelezo bei zimepanda kwa sababu moja, mbili, tatu; haitoshi. Muhimu sana tunachukua hatua gani kupunguza makali ya maisha kwa wananchi? Hili ndilo jambo la msingi, na Serikali hii ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa jinsi alivyoonesha upendo mkubwa kwa wananchi wake, naamini tukimshauri atachukua hatua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Jumanne Kibera Kishimba atafuatiwa na Mheshimiwa Cosato David Chumi na Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah ajiandae. (*Makofi*)

MHE. JUMANNE K. KISHIMBA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nami niungane na Wabunge wenzangu kuchangia Wizara hii ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rais, Waziri Mkuu na wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika kwa kuchaguliwa kuwa Spika wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kitila Mkumbo na Mheshimiwa Gambo wamejaribu kuliongea vizuri suala hili la kupanda vitu, lakini mimi bado nina wazo. Sisi Waislamu tumeambiwa tukatafute elimu mpaka China ila tusije tukachukua dini ya Wachina. Pia Biblia imesema, "watu wangu wataangamia kwa kukosa maarifa." Mwenyezi Mungu hakusema wataangamia kwa kutojua kusoma na kuandika, hapana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakisema ukachukue elimu mpaka China, walichomaanisha ni kwamba tukachukue mawazo ya Wachina na siyo maandishi ya Wachina; ila kama una wasiwası utasahau, unaweza ukajifunza Kichina kidogo ukaandika ili uje ukumbuke huku. Wataalam wetu, wasomi wetu wa Tanzania asilimia 90 wanajua kusoma na kuandika siyo maarifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi niko kwenye Kamati ya Viwanda na Biashara. Hapa tunapolia mabati, Serikali inakataa mabati kuanzia *gauge* 33 mpaka *gauge* 40, kwa nini? Je, imepiga marufuku nyumba za nyasi? Imepiga marufuku nyumba za tembe? Sasa wewe una shida nyumbani kwako, huna hela ya kuweza kula ugali mweupe, si unasaga dona? Si ndiyo maana yake? Sasa wakati huu wa shida, wewe unakataa watu wasiezekee mabati ya *gauge* 40 wakati hujatukataza sisi kutumia nyasi. (*Makofi/ Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, hii elimu ya kwenu ndiyo iliyotutoa sisi kwenye nyasi ikatupeleka kwenye bati. Ninyi mlikuja mkatuambia kwamba nyumba za nyasi ni mbaya, anzeni kutumia mabati. Leo mabati yamepanda, mnatuwekea sheria tena tusitumie ya *gauge* 40, kwa sababu gani? Tunamwomba Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara atoe hiyo dharura maana bati la *gauge* 40 ni shilingi 8,000/=, unamkatazaje mwananchi? Leo nyasi hazipo na hawa *new generation* hawawezi kuezeka nyumba ya nyasi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia viwanda vya *cement* kwenye Kamati vime-*confirm* vinayo *cement* ya shingili 5,000. Mheshimiwa Waziri anakataa, anasema wataalam wamemwambia kwamba maghorofa yataanguka. Wananchi wanajenga maghorofa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nimesema kwamba wataalam wetu asilimia 90 wanajua kusoma na kuandika, hawana maarifa. Wananchi kule vijijini wanatulalamikia mno kwamba hivi nyie kweli, ndiyo mmesoma, unanikataza mimi, lakini juu nimeweka turubai navujiwa; umenikatalia bati la *gauge* 40, inakuja kweli kwenye akili? Haiwezekani! Hata kama mnasema tukaiambie Serikari ipunguze, itapunguzaje sasa? Itafanyaje kupunguza? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, leo tulipewa hela hapa za Mheshimiwa Mama Samia shilingi trillioni moja na kitu, zote tumempa Dangote, mmekataa matofali ya kuchoma. Hela si wangebakiza kwa wananchi? Shule za matofali ya kuchoma leo zina miaka 150 na Makanisa yapo. Sasa Dangote kachukua hela, ALAFwamechukua hela ambao ni Wachina, sisi ndiyo tutalipa deni. Kwanini hela nytingine isingeenda kwenye matofali ya kuchoma, wananchi wetu wakapata hela na ndiyo walipaji wa lile deni? kwa hiyo, najaribu kuleta hili wazo ambalo wenzetu wataalam lazima tukubaliane kwamba tuna watu wa hali ya chini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, juzi hapa kama sikosei, ni miezi miwili au mitatu kuna gazeti la Busara lilitoa mwelekeo kwamba taasisi inayoongoza kwa kufanya vizuri sasa hivi, ni

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Jeshi la Wananchi wa Tanzania ikifuatiwa na wananchi wale wenye mila za kienyeji. Sisi Bunge ni taasisi ya saba kwa kuva vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa ombi langu, sisi kule Kanda ya Ziwa asilimia 75 ya watu wetu wana dini za mila. Kwa nini Serikali isiruhusu wafundishe na wao dini yao mle kwenye shule? Serikari ipitie vile vitabu vyao, linapokuja somo la dini wana pofundishwa Wakristo na Waislamu, na wao wafundishe. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu, hawa watu wako asilimia 75, lakini dini yao ni nzuri mno. Wao wanachofundisha ni kusalimia umepiga magoti kwa mtu mzima, siku ya harusi wanafanya harusi kwenye mti, wala hamna kadi wala hamna nini; kwenye mazishi mnaleta chakula toka kwa jirani. Je, ni kosa utaratibu huo ukifundishwa; ili siku wakija kufika sasa wenye dini, wakute watu hao ni wastaarabu. Ila sasa hivi, mnachofanya nyie, mnawapelekea kamari na *disco*. Sasa ipi bora? Wafundishwe utaratibu wao waishi vizuri kwa utaratibu ili siku nyie mkifika na dini zenu, basi wanaweza wakaungana, kuliko sasa hivi tukiwaacha hivyo hivyo na kila mtu anawasakama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunamwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni alifikirie, maana yake Mheshimiwa Rais sasa hivi mnafahamu ndiyo Kiongozi wa Machifu, sasa Machifu gani kama hawatakuwa na kitabu cha kufundishia wale watu wao? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia tu, ni suala hili la mtihani. Siku ya mtihani wanakuja polisi, kuna kuwa na vurugu pale shulenii, najaribu kujiuliza hivi kweli mtu toka darasa la kwanza huwa anakuwa wa kwanza mpaka darasa la saba mpaka *form one*, wewe hofu yako nini mpaka unaleta polisi siku hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa nini kama matokeo yatakuja tofauti wewe unayemtilia shaka ni yule ambaye huwa wa mwisho, kama wa mwisho amefaulu si uangalie kwenye

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

notice zake tu za kila siku toka darasa la kwanza, kwa nini we leo umefaulu. Kwani akili ya binadamu ni bando kwamba wewe uliweka bando leo siku ya mtihani. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, sioni sababu maana wale watoto wanakuwa na hofu, wanaona polisi, kunakuwa na hekaheka, ni ya nini, toka darasa la kwanza rekodi zote zipo, kama atafaulu ambaye hafaulu basi, ni kwa nini unafuta mtihani wa shule nzima. Kwa nini usichukue tu wale ambaou unaona huwa hawana akili leo wamefaulu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo najaribu tu kuona kwamba wataalam wetu wajaribu kufikiria maisha ya wananchi, wasiwe *rigid*, kuna mabati ya *asbestos*, yalipigwa marufuku hapa miaka 40 iliyopita, sababu ilisemwa ni kansa, tunamuuliza Mheshimiwa Waziri miaka 40 iliyopita sababu hizo zipo, wataalam tunao kwa nini wasifanye *research* tena, maana yake bati la *asbestos* linatengenezwa kwa mkono, leo nani angelia mabati na unatumia katani na *cement* linakuwa batimbona sie tunaezekeea matope na nyasi? Ndio tunataka elimu iwe hivyo hatutaki elimu ya kiingereza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunataka elimu ikawasakiie wananchi hasa wakati huu wa matatizo, hata wakisema tumbane Mheshimiwa Rais, wataweza kupunguza bei ya vitu duniani, kwa nini wanakataa tusirudi huko ambako kuna *solution* ya dakika moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunaomba Waziri atangaze kwamba kuanzia kesho kwa dharura hii tumeruhusu sasa hivi unaweza kutumia mabati ya *gauge* 40.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huo, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Jumanne Kibera Kishimba.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Waheshimiwa Wabunge huwa Mheshimiwa Kishimba akichangia wote mnanyamaza humu ndani kusikiliza profesa akiwa anazungumza. Ila sasa hapa ametoa takwimu za asilimia 90 kujua kusoma na kuandika, halafu bila maarifa na humu ndani kumejawa wasomi, natafakari. Asilimia 90 ya wasomi humu ndani, hii inaweza kuwa mtihani kidogo, akini kwa sababu ni profesa aliyetoa hizo takwimu basi twende naye kwa namna hiyo. Mheshimiwa Cosato David Chumi atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, Mheshimiwa Erick James Shigongo ajiandae.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Napongeza maandalizi yote ya Ofisi ya Waziri Mkuu katika hotuba hii ya bajeti utekelezaji na makadirio ya mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuanza kwa nukuu ya baba wa Taifa Mwalimu Nyerere aliyeitoa katika *speech* yake, ilikuwa kwenye Kiingereza ikisema *the situation and challenges of education in Tanzania* tarehe 22 Oktoba, 1984. Katika nukuu hii alisema; *not being selected to enter form one does not imply that they have failed yaani hao wanafunzi it is result of the very few form one places which exist.*

Mheshimiwa Spika, hii maana yake ni nini? Nataka nitumie nafasi hii kuipongeza Serikali kwamba nyakati hizo tulikuwa tunakosa nafasi za kwenda kidato cha kwanza, sio sababu labda tulifeli, ni kwa sababu nafasi zilikuwa chache. Sasa napongeza Serikali kwa sababu tumejionea mwaka huu fedha tulizopata ambazo ni mkopo ambao *of course* tutalipa sisi wenyewe Watanzania, jinsi mgawanyo umeelekeza hadi kugusa maeneo ya elimu na hivyo watoto wetu kujunga na kidato cha kwanza katika awamu moja bila kusubiri *second or third selection*. Napenda kupongeza sana Serikali katika jambo hili.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kupongeza Serikali kwa shughuli ambazo zinaendelea katika majimbo mbalimbali ikiwemo Jimbo la Mafinga Mjini ambapo napongeza pia utaratibu wa kutujulisha Wabunge, hapa nina

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

barua kutoka TAMISEMI ikinieleza kuhusu milioni 500 za ujenzi wa barabara katika Jimbo la Mafinga Mjini na kazi inayoendelea. Kwa hiyo sisi watu wa Mafinga tunaona pamoja na changamoto zingine zote, kazi iendelee tunaiona kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nijielekeze katika jambo hili ambalo hata mwaka jana nilisema. Kama Taifa, viko vitu lazima tujitosheleze ndani, nilisema kuhusu sukari, mafuta ya kula, bidhaa mbalimbali ambazo katika nyakati ngumu kama hizi ambazo zinazoendelea huko kwa wenzetu, maana yake kama tunajitosheleza hata kama ni kupanda kwa bei hakuwezi kupanda kwa bei kama unavyotegemea kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kazi ya Bunge mojawapo ni kushauri, sasa nashauri. Ukienda katika ukurasa wa 57 wa kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu anazungumza ambavyo Jeshi la Kujenga Taifa linafanya kazi nzuri ya ujenzi, kandarasi mbalimbali, nataka nishauri wakati wa amani duniani kote, wakati wa utulivu majeshi ya ulinzi kazi yake ni uzalishaji. Kwa hiyo nataka kushauri tuwape JKT hii kazi, nilikwenda na Kamati Chita nimejionea kazi nzuri inayofanywa na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, tuna maeneo mengi yana rutuba, tuthubutu, *for two years* hatutaagiza mafuta kutoka nje, *unless tutake wenyewe*. Tulime alizeti za kutosha, tuwape kazi ya kutafiti mbegu zinazotakiwa, tulime ufuta, tutaondokana na kutumia mabilioni ya fedha kuagiza hizi bidhaa nje na bei kupanda. Tukifanya hivi, tutawapa wananchi wetu unafuu mkubwa sana katika Maisha. Kwa hiyo naomba na nashauri jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, ukienda pia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukurasa wa 80 unatoa msisitizo wa mambo muhimu katika mwaka wa fedha tunaoelekea, ni kutoa msukumo katika kutekeleza vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na vipaumbele hivyo vinajumuisha kuchochaea uchumi shindani na shirikishi.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Pia kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma, kukuza biashara na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ninapozungumza hapa watu wa Mufindi, Mafinga, Njombe na Kilolo tuko katika hali ya taharuki baada ya kuambiwa kwamba Serikali sasa ina mpango wa kuanza kuagiza nguzo kutoka nje. Sasa sijajua kama kuagiza nguzo kutoka nje ina-reflect Mpango wetu wa Maendeleo wa Taifa kama ambavyo hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu inaeleza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa miaka sita saba Serikali imetuamini tume-supply nguzo katika miradi ya REA, TANESCO. Hapa napenda nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa January Makamba, tulipopata taarifa hii nilimwendea na *immediately* akaitisha kikao baina ya wazalishaji, TANESCO na yeye, kutaka kujua ni sababu gani zinaifanya TANESCO ifikirie kuanza kuagiza nguzo kutoka nje, wakati hapa tunasema kwamba vipaumbele vyta mpango wetu ni kuchochaea uchumi shirikishi. Huu ni ushirikishwaji gani, nguzo tunazo unaagiza nguzo kutoka nje, ni kwa sababu gani.

Mheshimiwa Spika, katika kikao kile TANESCO wanasema kwamba ni suala la uwezo. Kwa mwaka uzalishaji wa nguzo ni zaidi ya milioni tatu, *consumption* ni milioni moja unawezaje kusema kwamba ni uwezo. Pili wanawema ubora, narejea hotuba ya Waziri Mkuu kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani, sasa kama ni suala la ubora uki-supply nguzo laki moja ukakuta nguzo 500 hazina ubora ni jambo la kawaida, hata viwandani soda kuna nyingine unakuta ziko *flat*. Kwa hiyo kama tuko *serious* kupunguza makali ya wananchi wetu, yako mambo ni lazima tuyasimamie kwa nia ya ile dhana tunayosema *local content*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hivi ninapozungumza, kwa mfano, katika nguzo kuna *chain* kubwa ya uchumi. Yuko mtu ambaye anazalisha, ana shamba, yuko mtu anakuja kununua kwa mwenye shamba, yuko mtu atapewa kibarua cha kuangusha nguzo na kuzimenya, yuko mtu atapakia kwenye fuso, yuko mtu atasafirisha kwenda kiwandani, yuko

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mwenye kiwanda ata-treat atanunua dawa, yuko mwenye *semi-trailer* atasafirisha kwenda Mwanza, Kigoma na kadhalika. Hawa wote katika utendaji wao wa kazi pako sehemu wanununa mafuta. Wakinunua mafuta Serikali inapata *fuel levy*. Sasa *chain* yote hiyo all over sudden tunataka tuiondoe.

MHE. JUSTIN L. NYAMOGA: Mheshimiwa Spika, taarifa

MHE. COSATO D. CHUMI: Je, tunaondokana na hili jambo la kujenga uchumi shirkishi na shindani?

Mheshimiwa Spika, naomba...

SPIKA: Simwoni anayesema taarifa.

MHE. JUSTIN L. NYAMOGA: Mheshimiwa Spika, nkoo hapa

SPIKA: Sawa, Mheshimiwa wa Kilolo.

MHE. JUSTIN L. NYAMOGA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nataka tu kumtaarifu Mheshimiwa Cosato anapoendelea kuchangia kwamba katika Wilaya ya Kilolo tu peke yake kuna kiwanda cha nguzo kikubwa na kina wawekezaji wanatoka nje ya nchi, ambazo hizo hizo ndio nchi ambazo zinatarajiwaa kuagizwa hizo nguzo na wanatumia mashine kama hizo hizo zilizoko kwenye hizo nchi. Kwa hiyo afahamu tu kwamba na wana nguzo za kutosha, hata hivi tunapozungumza ambazo hazijachukuliwa na Serikali. Nilitaka tu kumfahamisha hilo. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa David Cosato Chumi, unaipokea taarifa hiyo?

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa hii na naongeza, Halmashauri zetu asilimia 60 ya *own source* zinategemea mazao ya misitu. Ninaposema mazao ya misitu ni nguzo, mirunda, mbaa na mazao mengine kama *plywood*. Nguzo tu peke yake zina-

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

make one third ya mapato yetu. Kwa mfano sisi Mafinga mapato ya ndani ni karibu bilioni 4.5. Maana yake unapoanza kuagiza nguzo kutoka nje unatuondolea mapato ya bilioni 1.5, ndio maana narejea hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, je, huku ndio kuchochaea uchumi shirikishi na shindani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninachotaka nikiseme, kuwajengea wananchi wetu uwezo ni pamoja na *local content* kuifanya kwa vitendo, lakini kinyume chake huku kama tunavyosema, bei za mafuta zinapanda, bei za sukari zinapanda, lakini tena yale mazingira machache yanayowaongezea kipato nayo tunataka tuwanyang' anye, je tutajenga uchumi shindani na shirikishi? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, katika ukurasa wa 62 mpaka 63 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, najua kengele imepiga lakini nilipewa taarifa, kuna dakika zangu zilienda nadhani....

SPIKA: Taarifa unapewa kwenye muda wako ndio maana unauliza kama unaikubali au unaikataa. Sasa maadam umeikubali maana yake umekubali achangie kwenye sehemu yako.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Spika, basi itoshe tu kusema kwamba jambo hili Serikali ijitafakari na iliangulari mara mbili.

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Spika naomba kuwasilisha.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, atafuatiwa na Mheshimiwa Erick James Shigongo na Mheshimiwa Ferista Deogratius Njau ajiandae.

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii. Ninayo mengi kidogo, lakini nitajaribu kuzungumza machache. Niseme na najiunga

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

na wenzangu kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais wetu kwa mafanikio mengi tunayoyaona na ambayo yameorodhesha vizuri kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Pia nimpongeze Rais wa Zanzibar Dkt. Hussein Mwinyi na Makamu wa Rais wetu Philip Mpango na wewe pia Mheshimiwa Spika nikupongeze jinsi unavyofanya kazi yako.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, naomba niseme, tumesikia mengi yametekelawa kwenye uchumi wetu, miradi mikubwa sana, lakini naomba Serikali ielewe kwamba, wakati unapofanya makubwa usahau kwamba kuna vikero vidogo vidogo ambavyo ukiviondoa vitakupa amani na kutekeleza yale makubwa.

Mheshimiwa Spika, ukiingia kwenye mtihani usianze na maswali magumu, anza na yale madogo na yale rahisi ambayo utayamaliza mara moja, halafu uende kwenye makubwa. Hasa ukienda kwenye halmashauri zetu kwa mfano, kuna vijikero kama kwa mfano kule Vunjo, barabara ya kilometra saba toka Mji Mdogo wa Himo kwenda Lotima, kitu ambacho unaweza ukakimaliza kwa fedha utakayoita ni chenji tu.

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye barabara tunayoita ni ya Mandaka - Mkirema kilometra saba ni pesa kidogo, ukienda Uchila – Kisomanji - Kikolarii ni kilometra saba au nane, kwa hiyo unaweza ukaviondoa na mimi nisije tena hapa nikiwa naomba kuuliza maswali hapa na pale, nitawaachia na wengine wakiuliza maswali kwa sababu vile vidogo vimetoka, mimi nina amani na Serikali *ina-implement* vitu vizito itaweba kui-*implement* bila kusema kule Vunjo kuna matatizo gani mbona huyu jamaa anasimama kila siku. Naomba Serikali ichukulie hilo na iweze kuvikamilisha vile vidogo.

Mheshimiwa Spika, tunaipongeza sana Serikali kwa miradi mikubwa iliyotekelawa na tunasema kwamba hii miradi ina maana kubwa sana hasa hii tunayoizungumza ya huduma za jamii, mashule na hospitali na kadhalika. Nafikiri

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

tuangalie vizuri kwamba je, *the current costs implications* zake zikoje. Unapojenga shule ufikirie *OC* na mishahara itakayotosheleza ile shule, iende ifanyi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, nafikiri kwamba hilo jambo ambalo kila saa nikiangalia najisikia na-*shrinks* sana. Hivi itakuja kufika mahali kwa mfano leo naamini kama tungenesema mahitaji yote ya Walimu, watoa huduma za afya na wafanyakazi wengine wa Serikali ambao wanatakiwa kwenye Wizara ambao hawapo kama wote wangepewaa, tungepewaa ile ikama kama inavyoombwa, naamini kwamba bajeti nzima isingetosheleza kukidhi mahitaji yale.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naamini kwamba ni lazima tuangalie vizuri na tufanye uchambuzi vizuri, tusije tukaishia kukopa ili tule. Nakubaliana na mambo haya mnayosema *inflation*, kwani hii *inflation* niseme na ni lazima tujue, leo hii mfumuko wa bei Marekani na nchi za kanda za ulaya imefikia asilimia 7.5 kwa wastani.

Mheshimiwa Spika, ni mfumuko mkubwa kuliko wakati wote kuanzia mwaka 1982. Kwa hiyo hili ni suala la kidunia ni *structural* na kitu ambacho hatuwezi kuki-*address* kusema kwamba tunaenda kuomba pesa, ni kufanya nini, ni kukaza mikanda, *this is the time to belt tighten*, ni wakati kusema kwamba *there is no way* tutaepuka makali haya, kama ulikuwa unaenda jimboni kila siku nenda mara mbili, mara tatu kwa sababu hela utakayokuwa nayo haitatosheleza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka kusema kwamba hilo ni jambo ambalo tuliangalie, sio kwamba ni letu na sio jambo la kufanya haraka haraka na sio kitu ambacho Benki Kuu inaweza ikashughulikia mara moja, haiwezi *it is not monetary policy* ya hapa ndani itafanya hicho kitu kwa sababu kinakuwa given na *imported inflation*.

Mheshimiwa Spika, sasa turudi hapa, ambacho nimepongeza kwenye hii miradi mikubwa, kuna kwa mfano hili suala la Vyuo vya VETE, naishukuru sana Serikali imeanza

kutoa vipaumbele stahiki kwa *VETA*, vyuo hivi ambavyo vinatupa *study* na ufundi. Hata hivyo, naambiwa kwa takwimu ambazo sio rasmi, *VETA* ina upungufu wa Walimu 1400 na ni kabla havijaongezwa hivi vyuo vingine ambavyo vinakamiliika kwenye mwezi huu wa Juni na mwaka unaokuja wanaweka vyuo vingine thelathini.

Mheshimiwa Spika, ukiweka pengine upungufu utakuja kuwa ni mkubwa sana wa watu, lakini sio tu upungufu wa Walimu, lakini ni upungufu pia wa vitendea kazi, vifaa vile vya kufundishia. Watu wanataka kujifunza cherehani, wanahitaji kushona kwa sababu sasa hivi tunavaa nguo zimeshonwa hapa, kwa hiyo lazima wawe na *basic equipments* kwenye hivi vyuo. Kwa hiyo, ni lazima tufikirie tunafanyaje pesa inatoka wapi ili tuweze kuhakikisha kwamba wanajenga ndiyo tusije tukajenga magofu, yaani kuwa na majengo tu *it doesn't help*, hiltasaidia.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu mkubwa nilitaka kuingiza kwenye uwekezaji ambao Mheshimiwa Rais wetu ameufanya kazi sana na naamini utanza kuona miradi mingi inasajiliwa. Wamesajili miradi 294 kutokana na hotuba tuliyopewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu na kweli kama miradi hii yenye kubeba thamani ya Dola Bilioni Nane itatekelezwa ajira zitaongezeka, kipato cha Taifa kitaongezeka, tutabakia kwenye kundi lile la watu walioendelea vizuri kipato cha katni pengine tutaenda juu, lakini miradi hiyo inatakiwa kutekelezwa, tutafanyaje mimi nataka nishauri mambo matatu, manne.

Mheshimiwa Spika, kwanza nataka uwekezaji huu wenzetu majirani zetu wameanza kupunguza kodi ya makampuni, kwa sababu tunashindania wawekezaji hawa, wanapunguza kodi ya makampuni kutoka 30 kuja asilimia 25. Hiyo ni kivutio ambacho hatuwezi kukibisha hata tungesema tunafanya nini. Pili; kuna *perception* kwamba gharama za kuanzisha mradi hapa ni kubwa sana kumbe wala si kubwa sana ukilinganisha na kwingine, tatizo la watu kuona gharama hizi za uanzishaji miradi kubwa ni uititiri wa mamlaka zinazotoza tozo hizi. (*Makof*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, utakuta kwamba kama tungeweka *lamp sum* tukasema kuanzisha kitu hiki ni Shilingi Milioni Moja unaenda kulipa kama ni *TRA* au mahali pengine lakini mamlaka nyingine zikagawiwa na huyo anayekusanya inakuwa ni rahisi mtu anajua kabisa *ok*, nataka kuanzisha kampuni ya simu ni Shilingi Milioni Tano basi *its transparent and open and no need ushauri wa mtu*. Kwa hiyo, mimi naomba hilo lifanyiwe kazi ili tuweze kupata wawekezaji hawa waje upesi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tatu; ni suala zima nitalizungumza tena kwa bahati mbaya suala la riba ambalo najua mamlaka imeshatoa amri imeshatoa *directive* kwamba lishughulikiwe, lakini hatuwezi kupata wawekezaji ambao hawawezi kukopa ndani kwa sababu utakuja na mtaji wako ndiyo mashine na nini, lakini ule mtaji wa *working capital/lazima utoke kwenye mabenki ya ndani*. Hasa huwezi kukopa kwa asilimia 16 wakati kule nje mtu anayezalisha kama huyo anakopa kwa asilimia tano uende ukashindane naye kwenye mauzo ya nje *it is impossible! What you need ni kwamba lazima kweli au tuweke special windows* na tunajua kwamba kuna watu wanataka kuongeza uzalishaji wao hapa kwa mfano kule *NIDA* tulikwenda, lakini hawawezi kukopa hapa ndani kwa sababu hiyo tu kwamba riba ni kubwa na wakipeleka kuuza vile vitu nje hawataweza kushindana kwa hiyo inakuwa matatizo, naomba hicho kifanyiwe kazi na tusichukue tu mzaha mzaha kwamba basi tu tuna njia ya kupunguza hizo riba, tunajua zipo! (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niongeze kingine ni kwamba mimi naamini pia kwamba miradi mingine kwa mfano Bagamoyo *Port*, sijui Mchuchuma – Liganga, tunasema kwamba tatizo lililopo ni kwamba wanajadili vitu ambavyo hatuna, wanajadiliana maslahi ya Taifa letu tuyalinde lakini tuangalie maslahi mapana yanatokana au faida nzima zinazotokana na mradi ule kwa muda mrefu, tuangalie tuisiangalie kesho utakosa ushuru wa kiasi hiki na hiki, kwa sababu huo ushuru huna *anyway haupo* kama ile kampuni haitaanzishwa wewe hutapata huo ushuru. Kama Bagamoyo *port* haitaanzishwa ianze kufanya kazi hutapata hicho kitu,

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kwa hiyo afadhali tukubali tuangalie tuwe na *long term view* ya *issues* badala ya kuwa na *short term issues*.

Mheshimiwa Spika, lakini niseme kwamba...

SPIKA: Ahsante sana muda wako umeshaisha Mheshimiwa.

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Eric James Shigongo atafuatiwa na Mheshimiwa Felista Deogratius Njau, Mheshimiwa Francis Isack Mttinga ajiandae.

MHE. ERIC J. SHIGONGO: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu Subhana Wataallah kunipa nafasi ya kusimama ndani ya Bunge lako Tukufu, nimshukuru sana Jehova kwa upendeleo alionipa kuwa mmoja wa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana wewe kunipa nafasi ya kusimama lakini niwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Buchosa kwa kunituma hapa Bungeni kuwawakilisha, nataka niendelee kuwaahidi ya kwamba nitakuwa mwakilishi bora nitakaye wawakilisha wao hapa Bungeni na sitajiwakilisha mwenyewe hata siku moja. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kabla sijaenda mbele sana naomba kwanza niunge mkono hoja, lakini niongee mambo matatu au manne hivi kabla sijazungumza hasa jambo nataka kuchangia.

Mheshimiwa Spika, kwanza; nataka nizungumze suala la uvezeshaji wa wazawa kiuchumi, nimezungumza hili suala mara kadhaa nataka nilizungumze tena leo. Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 8 (1)(b) jukumu kubwa la Serikali ya Jamhuri ya

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Muungano wa Tanzania itakuwa ni kusimamia ustawi wa watu wake. Mwaka 2004 tukatunga sheria katika Bunge hili ya kuwawezesha wazawa wa nchi hii kushikilia uchumi wa nchi yao baada ya kuona kwamba uchumi ulikuwa mikononi mwa wageni, sheria hiyo ilisainiwa na Rais Mkapa Marehemu mwaka 2005 na ikaunda Baraza la Uwezeshaji wa Wazawa Kiuchumi ambalo lipo mpaka leo.

Mheshimiwa Spika, naomba sana bajeti tunayopitisha mwaka huu ya zaidi ya shilingi trillioni 40 hivi naomba iweze ku-*consider* sana wazawa wa nchi hii. Wazawa wa nchi hii wamechoka kuona sehemu ya bajeti kubwa kama hiyo inaishia kwenda nje na wao wanabaki na umaskini. Kwa hiyo, naomba hilo lizingatiwe kabla sijaenda mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili; nchi hii ina vijana wengi sana wabunifu. Nchi hii ina watu wengi sana wenye uwezo mkubwa wa kubuni *solutions* mbalimbali, lakini wengi wanaenda nazo kaburini kwa sababu ya ukosefu wa uwezo wa kuzalisha bidhaa au kuendelea mbele na ubunifu wao. Naionba sana bajeti hii izingatie suala zima la kuanzisha *National Innovation Fund*, Mfuko wa kuwawezesha vijana wabunifu wa nchi hii waweze kwenda mbele na ubunifu wao na kutengeneza bidhaa. Hii ninaongea ni kama mara ya tatu ya nne hapa Bungeni kwa sababu wapo watu wengi sana wana ubunifu upo ndani ya kabati lakini hawana mtaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, huko duniani kuna kitu kinaitwa *Global Innovation Fund* ambayo huwa inatoa fedha nydingi sana kwa mataifa mbalimbali kusaidia wabunifu wao. Ethiopia mwaka jana wamepewa *Euro Milioni Sita* na hizi zinakuja siyo mkopo zinatolewa kama *grant* kwa wabunifu wetu wanaotoka vyuo vikuu ambaa hawana mtaji na hawakopesheki na benki zetu.

Mheshimiwa Spika, ninawaomba watalaaam wetu, *PhD* ambazo tunazo katika nchi hii ziandike maandiko ili tuweze kupata sehemu ya fedha hizo ziwasaidie watu wetu.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu; nataka kukumbusha kabla sijaenda mbele ni suala zima la kuipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mkataba au makubaliano ambayo iliingia na nchi za Uarabuni kuhusu mafuta. Waliingia makubaliano ya kwamba nchi za Uarabuni zitakuja hapa zitawekeza kwenye mafuta zitaweka matenki makubwa ili mafuta yawe yanawekwa hapa Tanzania igeuke kama Dubai au *Gulfx* Afrika Mashariki na Kati. Naomba Serikali yangu itekeleza jambo hili mapema hizi *deal* na urasimu huu uondolewe ili jambo hili lingekuwa limeshafanyika mapema hakika tusingekuwa pengine tunapata changamoto tunayoipata leo. Kwa hiyo, naomba hilo lifanyike mapema sana.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho na ninaomba niungane na Profesa Kitila Mkumbo ya kwamba *ex-ordinary times require ex-ordinary decisions*. Nchi yetu inapita kwenye wakati mgumu sana hivi sasa na siyo Tanzania peke yake ni dunia nzima inapita kwenye wakati usiokuwa wa kawaida, ninaiomba Serikali yangu Tukufu ifanye maamuzi magumu kwenye kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1979 baada ya vita ya Uganda nakumbuka Rais wetu Hayati Baba wa Taifa alisema tufunge mkanda kwa miezi 18, watanzania tunatakiwa kufunga mkanda kipindi hiki kwa sababu ni wakati mgumu kabisa na yafanyike maamuzi ambayo yatasaidia wananchi wawe na unafuu wa maisha. Huko vijijini kwa watu wa chini kabisa achana na sisi huku juu, ukienda watu wana malalamiko makubwa sana. Kila kitu kimepanda bei, mafuta ya kupikia, mafuta ya *petrol*, kila kitu kipo juu na wananchi wanashindwa hata ku-afford Maisha. Kwa hiyo, tufanye maamuzi ambayo yatakuwa na maslahi kwa Taifa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nizungumzie suala la umaskini wa Taifa hili. Mwaka jana tumesherehekeea uhuru wa nchi yetu mwezi wa 12, ni kweli Taifa hili limepiga hatua kubwa sana na mimi nakubali, lakini umaskini bado upo na umaskini unawasumbua sana watu wa nchi hii. Sisi wote hapa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

tunatoka vijjini na wengi wetu hapa tunatoka katika familia maskini tunaelewa madhara ya umaskini.

Mheshimiwa Spika, Taifa hili umaskini mkubwa unawakabili wakulima wa nchi yetu. Nchi hii wakulima wanapata shida na ndiyo mafukara namba moja, kilimo kimeajiri asilimia 65 ya watu. Naomba nizungumzie suala la kilimo kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, ili nchi hii iondoke kwenye umaskini unaotukabili ni lazima tuwekeze sana kwenye kilimo chetu, hatuvekezi vyta kutosha kwenye kilimo. Nchi hii wakulima wanazidi kuwa maskini kila siku, tumeshakuja na mipango mingi sana, siasa ni kilimo, kilimo cha kufa na kupona, kilimo kwanza, mambo mengi tuna-*fail* wakati umefika tuijulize ni kwa nini tuna-*fail*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Taifa hili lina ardhi kubwa sana *square kilometer* Laki Tisa hivi, na ardhi ambayo inaweza kulimwa ni kama *square kilometer* za miraba Laki Nne hivi. Lakini nchi ya Malawi ni ndogo, ardhi yao ambayo inaweza ikalimwa ni *square kilometer* kama 50,000 hivi, lakini wanazalisha *soya bean* tani 230 kwa mwaka sisi tunazalisha tani 6,000 mpaka 20,000 kwa mwaka na ukubwa wa hekta tunao na mchango wa kilimo kwenye pato la Taifa ni asilimia 26% lakini Malawi ina 42 % *what is wrong with us.* (*makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka tuijulize kama Taifa nini shida yetu katika kilimo? Naomba uwekezaji kwenye kilimo ufanyike kwa nguvu kubwa sana kuwasaidia wakulima wanchi hii. Mazao ya nchi hii wakulima wetu wanalima lakini mwisho wa siku mazao yanaishia kuharibika, *post-harvest loss* kwenye Taifa hili ni asilimia 40, tafsiri yake ni kwamba unalima mazao lakini asilimia 40 yanaharibika.

Mheshimiwa Spika, miwa katika Taifa hili tunavuna tani Milioni Nane kwa mwaka, lakini tunatumia tani Milioni Nne peke yake na tani Milioni Nne zinaharibika. Naambiwa na wataalam wa kilimo kwamba tani Milioni Nne zinazoharibika zingeweza kuchakatwa kuwa sukari

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

tusingeagiza sukari, hivyo, *forexyetu tungeweza kuiokoa!* Kwa nini hatuwekezi kwenye utengenezaji wa mitambo ya kuchakata sukari? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, *TEMDO* taasisi yetu ya Tanzania *Engineering Manufacturing Development Organization* wanatengeneza mitambo, wametengeneza mitambo, mimi ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda na Biashara wametengeneza mtambo wa kuchakata sukari ambao unaweza kusaidia wakulima wadogo wadogo wakikopeshwa na *SIDO*, *SIDO* kuna kitu wanaita *NEDF* wanakopeshwa wakawa wanatengeneza sukari hii miwa tutaiokoa. Kwa nini hatuwekezi sasa kwenye *TEMDO*?

Mheshimiwa Spika, kazi ya Mheshimiwa Bashe ni kulima, kazi ya Mheshimiwa Bashe siyo kuuza, kazi ya kuuza ni ya Mheshimiwa Dada yangu Dkt. Ashatu Kijaji, Wizara ya Viwanda na Biashara. Sasa najiuliza tunaweka bajeti kubwa kwenye kilimo lakini kwa nini hatuweki bajeti humu ya kutafuta masoko?

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mwenyekiti ninakuambia *TANTRADE*hawana pesa watatafutaje masoko? Mheshimiwa Bashe atalima atauza wapi? Matokeo yake tatalima lakini mazao yataoza. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba sana tubadilishe mtazamo wetu kwenye kilimo, ni kilimo peke yake kitaitoa nchi hii hapa ilipo kwenda mbele.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja tena. Ahsante. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Felista Deogratius Njau, atafuatiwa na Mheshimiwa Francis Isack Mttinga, Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara ajiandae.

MHE. FELISTA D. NJAU: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia katika hotuba ya Waziri Mkuu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, najikita kwenye ukurasa 33 ambapo ameainisha kwamba Serikali imeendelea kutekeza miradi ya ujenzi wa Mahakama mbalimbali nchini. Tuna kero kubwa ambayo ni kwikwi katika Taifa ni mlundikano wa mahabusu ndani ya Mahakama na wafungwa, hii ni kero kubwa kwa Taifa na inasababisha athari kubwa.

Mheshimiwa Spika, mpaka hapa tunapoongea mahabusu na Mahakama ndani ya nchi yetu wako zaidi ya 30,000 hawa zaidi ya 30,000 ni kiwango cha juu kabisa tumeshazidi yaani Mahakama zetu zimekosa uwezo na Magereza wa kuweza kumudu hawa watu.

Mheshimiwa Spika, nilijua mkakati utakuja madhubuti katika kutekeleza hili ili tuweze kupambana na adha hili, kwa sababu ndani ya Magereza kuna vitu vingi. Kuna kesi ambazo ni kesi za ajabu, yaani unakwenda Magereza unaenda kutembelea wafungwa unakutana na msichana amepoteza 10,000 ya bosi wake, yuko pale miezi nane, ni kesi ngumu.

Mheshimiwa Spika, ninapendekeza kwa sababu wale wakiwa kule tayari wana-*adopt* tabia ngumu na mbalimbali mbaya ambazo kwenye jamii hazikubaliki, ni bora tungekuwa na sera maalum au utaratibu wa kuweza kuchukua haya makosa madogo madogo na kuwafunga vifungo vyatya. Tukifanya hivi tunaweza kusaidia kupunguza adha ya mlundikano wa Magereza zetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kingine kikubwa Magereza yetu pia yamejaza katika hao 30,000 kuna wakimbizi ndani yake ambao hapa nchini kwetu wanapita tu au hii ni njia. Kwa hiyo, hapa wanatokea Nairobi, wanakuwa-*charged* hela wanapita, hapa sisi tunaenda kuwekeza pesa tunajenga *self-house* tunawaweka, wanakula pesa za Watanzania, pesa za walipa kodi, halafu kifungo kikiisha wanaangalia tu kama kawaida. Kwa hiyo, tunapoteza fedha nyingi kutumia kwa hao watu. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa tuna takwimu ya wakimbizi 5,756 wako Tanzania na kwa siku mtu mmoja anakula shilingi 2,500 mara idadi hiyo, kwa siku wanakula zaidi ya shilingi milioni 14, ukihesabu kwa mwaka ni zaidi ya shilingi bilioni tano. (*Makofii*)

SPIKA: Sawa. Mheshimiwa Felista Njau tusaidie jambo moja, hawa ni Wakimbizi au wahamiaji haramu?

MHE. FELISTA D. NJAU: Mheshimiwa Spika, ni wahamiaji haramu.

SPIKA: Eeh! Ni lazima taarifa yako iwe inawasema hivyo kwa sababu Wakimbizi kuwekwa ndani tena inakuwa kidogo siyo sahihi.

MHE. FELISTA D. NJAU: Mheshimiwa Spika, sawa. Hao wahamiaji haramu ambao wanaopita, kwa hiyo wanatumia shilingi zaidi ya bilioni tano milioni mia moja kumi na moja ambazo ni pesa za walipa kodi ya Watanzania. Ukikaa ukafikiria unaweza ukaona labda, halafu hakuna mtu anayeshtuka wala hakuna hatua, kikubwa ingewezekana wakifika hapa wachukuliwe na *escort* mpaka mpakani wanapoelekea ili tuokoe hii pesa ya Watanzania ambayo inachukuliwa bure na hawa watu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wakati tunazungumza haya ziko hospitali hazina dawa, wakati tunazungumza haya ziko barabara mbovu, pesa hii ingeweza kuelekezwa kule na ikaleta tija. Ukjumlisha hii pesa kwa pesa ya Tanzania kwa darasa moja la Shilingi Milioni 20 unajenga madarasa 250, kitu ambacho hili tungelichukua kama *special case* tukaenda nalo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine gumu wahamiaji hawa haramu wapo walotumikia kifungo chao, wamemaliza kifungo na wapo nchini 2,200 wanakula pesa za walipa kodi, wanakula pesa za Watanzania, wahamiaji haramu 2,200 wapo tu wamemaliza kifungo, hawapelekwi kwao, hawako

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ndani wako tu pale wanambwela wanakula hela za Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba hatua zichukuliwe Uhamiaji, Mambo ya Ndani na Polisi washirikiane katika hili ili kuokoa pesa nyingi za walipa kodi zinazopotea. Tunalia adha ya umaskini, tunalia janga, sasa hivi tuko kwenye umaskini mkubwa huko nje kila mtu ana kilio, lakini pesa hii ingeweza kuwezesha hata vikundi vyta akina mama ambao leo wanatembea wana adha kubwa, hili tulichukue kwa unyeti wake ili liletetija kwa Taifa letu. (*Makofi*)

MHE. ALI HASSAN OMAR KING: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

SPIKA: Mtoa taarifa yuko wapi? Aah! Mheshimiwa Felista Njau kuna taarifa, kwanza kabisa hutakiwi kukaa kabla sijamruhusu yeye, nikimruhusu ndiyo unakaa.

Mheshimiwa Mbunge wa Jang'ombe.

TAARIFA

MHE. ALI HASSAN OMAR KING: Mheshimiwa Spika, nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Felista Njau, kati ya hawa Wahamiaji Haramu ambao wamemaliza kifungo chao wamekuja jamaa zao kuwataka wasafirishwe, basi bado kuna ugumu wa kuwatoa na bado tumewashikilia. Nataka nimuongzee hiyo taarifa. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Felista Njau unaipokea taarifa hiyo.

MHE. FELISTA D. NJAU: Mheshimiwa Spika, naipokea kwa mikono miwili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika suala hili niombe Wizara ziungane ili kulitatua kwa wakati na kwa muda ili kuokoa pesa hizi zinazopotea.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ninataka nilichangie kwa ufupi ni kwamba kuna kipande cha barabara inayotoka Morogoro kuja Dodoma, hiki kipande ni kama vile watu hawaoni, lakini ni kipande kigumu ambacho kina mabonde, ukisafiri usiku unaweza ukafikiri haupo Tanzania, lakini kwenye barabara hiyo kwa siku unakutana na malori manne, matano yamedondoka yako chini, hakuna *effort* zozote zinazochukuliwa katika kurekebisha barabara hii ambayo umuhimu wake mkubwa kwanza ni barabara inakuja Makao Makuu ya nchi.

Mheshimiwa Spika, pili, barabara hii inaunganisha nchi za jirani kwa maana ya Uganda, kwa maana ya Congo, kwa maana ya Rwanda, kwa maana ya Burundi. Barabara hii ni ya msingi kwa maana ya diplomansia yetu ya kiuchumi, inasafirisha malori yanayosafirisha bidhaa kuelekea nchi mbalimbali, lakini imesahaulika kabisa.

Mheshimwia Spika, lakini kwenye barabara hiyo kwa siku unakutana na malori manne mpaka Matano yamedondoka, na hakuna *efforts* zozote zinazochukuliwa katika kurekebisha barabara hii ambayo umuhimu wake ni mkubwa. Kwanza inakuja makao makuu ya nchi, pili, barabara hii inaunganisha nchi za Jirani za Uganda, Congo, Rwanda pamoja na Burundi. Kwa hiyo, barabara hii ni ya msingi, kwa maana ya diplomasia yetu ya uchumi kwa sababu malori yanatasafirisha bidhaa kuelekea nchi mbalimbali, lakini imesahaulika kabisa.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana, nafikiri ni Oktoba, Msemaji wa Serikali alisema tayari upembuzi yakinifu umefanyika tunatafuta Mkandarasi, lakini naona kuna ukimya mkubwa katika barabara hii. Naomba tulichukulie kipaumbele kwa sababu Wabunge wanapita hii barabara na watakuwa ni mashahidi wangu, barabara ni mbovu kwa kiwango cha tofauti. Naomba hilo lichukuliwe kama ushauri wangu. Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Felista Njau kwa mchango huo. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Francis Isack

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mtinga atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava ajiandae.

MHE. FRANCIS I. MTINGA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika Hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumpongeza Rais wangu Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuiongoza nchi kwa weledi mkubwa, na pia kuijaza jumbo langu fedha nydingi katika sekta zote. Leo hii tunajenga Vituo vya Afya, Gumanga pamoja na tunajenga Ilunda. vilevile leo hii tunajenga shule ya thamani ya milioni mia nne sabini katika Kata ya Ilunda, tumepeata fedha za barabara na tunaunganisha kata zetu; yote haya yanatokana na Uongozi wake mzuri, nampongeza sana kwa hili.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, niiombe Serikali iunganishe haya mazuri kwa kutupatia kilomita arobaini na mbili za lami kutoka makao makuu ya wilaya kwenda makao makuu ya mkoa, ili wananchi wafaidi matunda hayo kwa kwenda vizuri katika mkoa wao na makao makuu ya wilaya yao.

Mheshimiwa Spika, niende sasa kwenye mchango wangu. Mimi ningependa kuongelea nia njema ya Serikali katika kulitizama upya suala la kilimo katika nchi hii. Nimeona nia njema ya Serikali sasa ya kupeleka fedha nydingi, na ushahidi tu ni juzi, Rais wetu amekabidhi takribani pikipiki 9,000 na vifaa vya kupima udongo kwa lengo la kuinua kilimo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo ninapata hofu kama nia hii njema itafanikiwa vizuri kutokana na kitendo cha kuzingunisha Idara zetu mbili katika Halmashauri, Idara ya Kilimo na Idara ya Mifugo kuwa Idara moja. Hizi Idara ni kubwa sana. Sote tunatambua umuhimu na ukubwa wa Idara ya Mifugo katika kuchangia pato la nchi hii na pia tunafahamu Idara ya Kilimo ilivyo muhimu. Kama ambavyo zipo Wizara mbili tofauti, Wizara ya Mifugo na Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, sijui ni busara gani imetumika katika kuunganisha Idara hizi katika ngazi ya Halmashauri kuwa Idara moja. Tunafahamu Mkuu wa Idara atakuwa mmoja na kwa vyovoyote lazima atabobeia aidha, kwenye kilimo au kwenye mifugo; na kwa vyovoyote utendaji wake utaendana zaidi na ubobezi wake. Sasa jambo hili la kuunganisha Idara hii kuwa moja wakati Mawaziri ni wawili na Idara zenyewe ni kubwa na zinapelekewa fedha sasa kwenda kuinua uchumi wa nchi, naona kama ni jambo ambalo tume-overlook kama Serikali.

Mheshimiwa Spika, mimi ningependa kuishauri Serikali, kwamba idara hizi zibaki kuwa idara mbili tofauti ili fedha nyigi hizi zinazopelekwa kwenye kilimo na kwenye mifugo ziweze kusimamiwa vizuri na wataalam katika kuleta tija katika nchi yetu. Kama kweli lengo ilikuwa ni kubana matumizzi, sidhani, kwa sababu kwa kuunganisha Idara hizi bado tumeongeza idara nytingine. Zilikuwa kama 19, sasa hivi ukiangalia idara na vitengo zinakaribia 23. Kwa hiyo mimi ningecomba niishauri Serikali yangu iliangularie upya suala hili la kufanya Idara hizi zisiwe moja ziwe Idara mbili tofauti kama ambavyo Wizara zipo tofauti, ili lengo jema hili hili la kuinua kilimo na mifugo iweze kufanikiwa vizuri katika Idara zetu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, ningependa kuishauri Serikali yangu kuhusiana na suala la mipaka ya kiutawala katika nchi yetu. Mipaka ya mikoa, wilaya, kata, vijiji mpaka vitogoji ina migogoro mikubwa sana katika nchi yetu. Jambo hili llinasababisha wananchi wetu wanagombana mpaka sehemu nyingine wanapoteza maisha; lakini vilevile maendeleo ya nchi yanarudi nyuma kwa sababu ya suala hili. Ipo mikoa imeanza hivi karibu kwa mfano, Mkoa wangu wa Singida ulikuwepo kabla ya Manyara. Manyara ilipoanzishwa, leo hii ukichukua *GN* ya Singida, ukichukua *GN* ya Manyara katika maeneo yanayopakana kila Mkoa unatambua eneo tofauti. Hivyo hivyo ukienda kwenye wilaya n ahata kwenye kata zetu.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi ningeshauri Serikali ifanye *program* maalum ya kuhuisha na kuangalia mipaka

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

yote ya kiutawala katika nchi hii, ili kuleta utulivu wa nchi, kuleta maendeleo ya nchi na wananchi wetu wafanye kazi zao wakiwa katika hali yenye utulivu. Kwa hiyo ningependa kuishauri Serikali yangu...

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Mtinga kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Festo Sanga.

T A A R I F A

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Spika, alolizungumza Mheshimiwa Mbunge ni sahihi kabisa. Hata kule Njombe na Mkoa wa Mbeya kuna changamoto kubwa ya mipaka ambayo imesababisha hata hili zoezi la uwekaji wa anuani za makazi kwenye nchi hili imekuwa changamoto sana maeneo ya mipakani. Kwa hiyo ni kweli anachokizungumza Mheshimiwa Mbunge, nilikuwa nataka kumpa taarifa kuhusu hilo.

SPIKA: Mheshimiwa Mtinga unaipokea taarifa hiyo.

MHE. FRANCIS I. MTINGA: Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa hii kwa mikono miwili, na ninaamini hapa hata Wabunge wote wangepata nafasi wangekubaliana na jambo hili, ni tatizo kubwa, kwa hivyo niiombe Serikali ichukulie jambo hili kwa muhimu sana kwa sababu wananchi wetu wanapata tabu sana kwa kugombania mipaka. Tunashindwa kufanya nyingi kwa kusuluuhisha migogoro hii. Kwa hivyo Serikali ilichukulie jambo hili ihuishe tu mipaka wananchi waelezwe, sisi Viongozi tuelezwe, mpaka unapita hapa, unapita pale ili kazi za nchi hii ziweze kuendelea vizuri.

Mheshimiwa Spika, mimi leo nilipenda nijikite katika maeneo hayo kwa sababu sipendi sana kupigiwa kengele. Lakini nikupongeze sana kwa jinsi ambavyo unaliongoza Bunge letu vizuri. Nilikuwa Mkoa wa Mbeya katika Halmashauri yako pale ya Manispaa hauna *double road* hata moja. Niombe Wizara ya Ujenzi pale panatia aibu, mji

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

umebanana sana ule angalau iwepo *double road* pale katikati ili Mji wa Spika wetu ufanane na Jiji la Mbeya, ahsante sana. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mtinga, na naamini Kaimu Kiongozi wa Shughuli za Serikali amesikia, na maadam tupo kwenye Bunge la Bajeti atafanya jambo. Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, nilikuwa nishamtaja pia Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava atafatiwa na Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoy.

MHE. DKT. THEA M. NTARA: Mheshimiwa Spika, na mimi nikushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nitakwenda moja kwa moja, na nitachangia sana kwenye eneo la elimu.

Mheshimiwa Spika, eneo lolote au sehemu yoyote ambayo kuna vyuo vikuu hata watu wake katika eneo lile wanakuwa na maendeleo ya kiuchumi, maendeleo ya kisiasa na maendeleo ya kijamii.

Mheshimiwa Spika, Mikoa ya Kusini kwa muda mrefu imekuwa nyuma sana katika maendeleo kwa nyanja zote. Mikoa ya Kusini wakati tumekuwa wote tukisema jamani sisi watu wa Kusini tuko nyuma. Leo hii kama Mikoa ya Kusini ya Lindi, Mtwara pamoja na Ruvuma kukiwa na Chuo Kikuu cha Serikali mambo ya uchumi yatafunguka na watu wa eneo lile wote watakuwa wanapata elimu kutoka vyuo vikuu na mambo yao yatabadilika kama ilivyo kwenye Mkoa wa Dodoma. Wagogo tulikuwa tunawasema watani zangu; zamani ukisema Mgogo wengine wanaona aibu hata kusema mimi ni Mgogo, lakini sasa hii ukisema unatoka Dodoma Mheshimiwa Mavunde anafurahi, kwa sababu Dodoma imefunguka. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na mpango wa kujenga Chuo Kikuu kishiriki cha Mkwawa, Matogoro, Songea na Mtwara, wakati ule Mheshimiwa Waziri alikuwa Prof. Msola, nimpongeze sana alikuwa mwerevu na mjanja; kikawekwa Chuo Kikuu pale Mkwawa ambacho ndicho Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu. Hata hivyo, wazo la Mtwara likafa kimya

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mpaka leo ikawa hatujui kinachoendelea, Matogoro – Songea nayo ikafa na hatujui kinachoendelea. Hizi sehemu tatu zilikuwa katika mpango wa kufanya haya maeneo yawe ni vyuo vikuu vishiriki, lakini mipango hiyo ikafa na hatujui kwa nini ilikufa.

Mheshimiwa Spika, niseme tu, kwamba Kusini tunahitaji *a Public University full flagged*. Mimi ningeomba Serikali jamani sasa hivi ijipange angalau kwa kipindi hiki waache *legacy* kama iliyoachwa hapa *UDOM* basi tuache *legacy* huko Kusini, kijengwe chuo kikuu ili watu wa Kusini nao waanze kufunguka. Tutafanya maendeleo mengine yote; tutajitahidi kilimo na mengineyo lakini bila elimu bado Kusini kule tunaonekana hatujatoka.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye suala la pili ambalo naona nilisemee hapa ndani, ni suala hili la watoto wadogo wa chekechea. Hawa watoto wadodo nafikiri na Mawaziri waliangalie. Watoto wadogo wa chekechea wanaamshwa saa kumi usiku, saa kumi na moja magari yanawapitia, wanafika kwenye gari wanazunguka mpaka wafike shulenii labda ni saa mbili.

Mheshimiwa Spika, tunajiangalia sisi kwa sababu tayari tumeshakomaa na tayari tumeshapata elimu vizuri, lakini mimi naangalia, hivi hawa watoto wadogo wanaoamshwa saa kumi wanaandalisha kwenda shulenii *is it fair?* Hiyo *cognitive development* ya hawa watoto kweli inaenda vizuri? Kwa sababu wanasinzia mpaka wakifika kule shulenii, na wakati wa kurudi wanazungushwa mpaka wanafika nyumbani kule yule wa kwanza anakuwa wa mwisho. Wakati mwingine tunasikia mambo yanayotokea ndani ya hayo mabasi wanayozungushwa.

Mheshimiwa Spika, sikatai kwamba tunafanya biashara, lakini sasa wanazungushwa na wakati mwingine wale wanaowazungusha kwenye magari mnasikia wanachowafanya hao watoto. Sasa hilo nalo tuliangalie, kwamba hivi hii *trend* ni sawa? Wenzangu wataalam wa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Saikoloji na wataalam wa *Development* ya hiyo *brain*, je, hicho kinachotendeka ni sawa?

Mheshimiwa Spika, niunganishe na moja linalotokea sasa hivi, mimi naona ni janga la Kitaifa. Kuanzia *primary* mpaka vyuo vikuu dawa za kulevyia zimekuwa ni kawaida, bangi zimekuwa ni kawaida, michezo michafu inayofanywa na watoto wa kiume kwa wakiume imekuwa ni ya kawaida. Serikali tunasema nini? Tunajenga taifa la namna gani?

Mheshimiwa Spika, kuna siku moja kuna mzazi akanipigia simu akasema alienda huko *beach*, mnaita *beach*, sijui kwa Kiswahili tunaitaje, ufukweni; kwenda kule amekuta wasichana na wavulana wanafanya vitu vya ajabu vya waziwazi huko kwenye *beach*. Sizitaji shule maana tunasema tutaharibu biashara za watu; hivi tunaharibu biashara za watu ama tunaharibu Watoto? Mambo yanayofanyika sasa hivi ni ya ajabu, Wizara ya Elimu mpo, Wizara ya Afya mpo, Wizara ya Ustawi wa Jamii upo, Mambo ya Ndani mpo mpaka Utumishi. Tunalipeka hili Taifa wapi? Hivi baada ya miaka kumi au ishirini tutakuwa na watoto au tutaongeza vituo vya Mirembe? Hilo jambo linaniumiza na ni janga la Kitaifa, ni janga. Tutakuwa na watoto wa namna gani ikiwa hata watoto wa *primary* wanazijua bangi ni za kawaida? Je, tumehalalisha hii bangi? *that a thing I want to know.*

Mheshimiwa Spika, nije kwenye ukarabati wa vyuo vikuu. Niliongea kipindi kilichopita mpaka nikawa nawaza, hii *UDOM* nililzungumzia. Waende hao Mawaziri wakaangalie kule. Niliwaza nikasema hiki chuo ninachokizungumzia kingekuwa kipo Sumbawanga au kiko kule Newala labda wangekwenda, lakini kipo hapa karibu, hivi kwa nini hawaendi? Nelson Mandela ule mgogoro wa ujenzi wa kiwanja mpaka leo unaendelea, hawaendi.

Mheshimiwa Spika, ninawatahadharisha tu, ikija hiyo bajeti yao Elimu mimi yaani Shilingi hiyo nimeshandaa na watanifuata mpaka Ruvuma kuja kuichukua. Nelson Mandela, *UDOM* hapo kuna vyuo vya Afya vya kat, nilisema

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kule Songea hali ni mbaya, hebu nendeni mkazunguke kule muangalie. Nilisema wakati ule ulipokuwa Mwalimu wangu Ndalichako nilifiki umenielewa lakini ukani-*put off* kabisa, yaani sijui ulini-*neglect* kwa sababu ni mwanafunzi wako? *I don't know.* Sasa amechukua mwingine, Professor Mkenda sitaki kuja kuniambia tuongozane, mimi sitaki kuongozana tukutane hukohuko, kuongozana sitaki. (*Makofi, Vichecho*)

Mheshimiwa Spika, jambo jingine nilizungumze kuhusu fedha za *research* katika vymuo. Nishukuru sana Serikali ni kweli sasa hivi watoto wengi wanapata mikopo, lakini kutokana na idadi kubwa ya watoto wanaopata mikopo fedha za *research* zikapungua sana. Sasa..

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. DKT. THEA M. NTARA: Mheshimiwa Spika, muda wangu umeisha?.

SPIKA: Umeisha, ahsante sana Mheshimiwa Thea Ntara kwa mchango huo; na nafikiri kwenye hii hoja ya watoto ya kuamshwa saa kumi usiku, upande mmoja ni Serikali sawa lakini upande mkubwa sana ni wa wazazi. Kwa sababu kama mzazi anakaa Kibaha anataka mtoto wake asome shule iliyopo Dar es Salaam tena mitaa ya Posta, sasa unataka mtoto achukuliwe saa ngapi? Kwa hiyo saa nyinyige mzazi mwenyewe anataka sasa basi litaenda limchukue yeye peke yake alifu litaanza kumfikisha yeye shulenii saa ngapi na wote tunajua kuna foleni.

Kwa hiyo upande mwingine ni wazani; na washauriwe, na nadhani tuchukue ule ushauri alioutoa Mheshimiwa Rais kama ni wa jumla yale mambo ambayo inabidi tuwaambie watu tunaowawakilisha ukweli, tuwaambie ukweli. Mzazi unaye kaa mbali na shule Serikali imejitahidi na haya mabasi tunayozungumza hizi siyo shule za msingi za Serikali, ni shule binafsi mzazi ameamua kumpeleka mtoto wake mbali kwa hadithi alioisikia yeye. Kwa hiyo tuzungumze na hawa wazazi pia siyo Serikali peke

yake kwenye mambo hata yale sisi tuna uwezo nayo. Tuzungumze na wazazi wasipeleke watoto mbali kule ambako uwezo wa kuwatazama inakuwa ni saa chache na mtoto ni mdogo sana. Kwa hiyo hilo nalo nazani sisi tuendelee kuwashauri pia wananchi waendelee kuyatazama hayo mambo. Mtoto wa chini ya miaka saba unataka aende akasome sijui kilomita ngapi. Mpeleke shule iliyopo pale ya Serikali ndiyo maana tunasisitiza humu Bungeni shule ziendelee kujengwa ili watoto watoshe huko, lakini anayetaka kumpeleka mbali atafute utaratibu mzuri, kwa kweli saa kumi usiku ni haifai kabisa. Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava atafatiwa na Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mhe. Yahaya Omary Massare.

MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kuweza kunipa nafasi ili na mimi nichangie katika bajeti iliyopo mbele yetu. Kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa wasilisho lake la jana kwa bajeti ambayo kwa kweli inatupeleka tunapotaka.

Mheshimiwa Spika, ninaishukuru sana Serikali kwa kuongeza kiwango cha bajeti, na kwa hivyo nitazungumzia katika masuala mazima ya kuzuia maambukizi ya UKIMWI. Kwa kipindi cha mwaka 2022/2023 Serikali imetenga zaidi ya bilioni 1.8 kwa ajili ya kutekeleza afua za kupambana na maambukizi ya UKIMWI. Hata hivyo nitoe masikitiko yangu kwa bajeti hii ambayo inakwenda kumalizika mwezi wa sita, Serikali ilitenga kutoa Shilingi bilioni moja kwa afua za kupambana na maambukizi ya virusi vya UKIMWI kwa fedha za maendeleo zinazotokana na mfuko wa ndani.

Mheshimiwa Spika, wafadhili au fedha za nje zilikuwa jumla ya milioni mia tatu themanini na kitu, na wafadhili wametoa fedha kwa asilimia mia moja. Hata hivyo, lakini kwa masikitiko makubwa fedha za ndani ambayo ni milioni moja ilitengwa mpaka Machi haikutoka hata Shilingi moja. Sasa nikifikiria juhudhi ambazo tunazo kama nchi na malengo ya Dunia ya kudhibiti maambukizi mapya virusi vya UKIMWI; na Tanzania tukiwa katika mstari wa mbele kuhakikisha kwamba

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI yanapungua. Sasa kama bajeti ya Serikali, vyanzo vya ndani fedha hazitoki, ikitokea wafadhili wameacha kutoa fedha itakuwaje? Napata mashaka sana napata uchungu sana.

Mheshimiwa Spika, tunajua kwamba kuna mkakati wa kufikisha asilimia 95 ya watu wote ambao wanapimwa virusi vya UKIMWI kujua afya zao, asilimia 95 kwa wale ambao wamegundulika na virusi vya UKIMWI kuhakikisha kwamba wanakuwa katika matibabu; na asilimia 95 ya wale ambao wapo kwenye matibabu kuhakikisha kwamba wanapima kujua wingi wa virusi. Sasa kwa *trend* hii ya utoaji fedha, napata mashaka.

Mheshimiwa Spika, suala la maambukizi ya UKIMWI naona bado ni tatizo kubwa, hasa kwa vijana wenyе umri kati ya miaka 15 mpaka 24. Vile vile kwa wananchi ambao wapo pembezoni; wako kwenye mialo, maeneo ya migodi, hasa sasa hivi kumekuwa kukizuka migodi mingi. Mfano Mkoa wa Shinyanga, maeneo ya Kahama, Mwakitolio kuna migodi mingi ambayo inaibuka. Sasa hali ya kiafya, hali ya kuzuia maambukizi ya virusi vya UKIMWI imekaaje.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Taarifa ya Takwimu ya *Tanzania HIV Impact Survey* liliyofanyika mwaka 2016/2017 inaonesha kwamba idadi ya vijana wengi wenyе umri wa miaka 15 mpaka 24 wameshajiingiza katika vitendo vya kujamiihana. Katika idadi hiyo ya kundi hilo hilo la hao vijana wa miaka 20 hadi 24, kati yao wasichana wameambukizwa zaidi kwa asilimia 3.4 ukilinganisha na wavulana ambao wameathirika, wameambukizwa kwa asilimia 1.9. Hii inaashirika nini? Ni kwamba vijana wetu wengi wameshaingia katika hili janga la maambuziki ya virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, fedha ambazo zinatolewa na Serikali, fedha za ndani hazitolewi kwa wakati. Tunategemea kwa asilimia kubwa wafadhili. Je, tutawalinda hawa vijana ambao kwa kweli wapo kwenye *risk* kubwa? Je, tutawafikia wale watu ambao wapo kwenye mialo? Kwa tabia za wavuvi, wanaondoka majumbani kwao usiku kwenda

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kutega, wanarudi alfajiri wamechoka. Inabidi sisi watoa huduma za afya ndio tufanye juhudhi binafsi kuwafuata kuwafikia.

Mheshimiwa Spika, kwa *trend* ya fedha ambazo zinatengwa na Serikali tunapitisha hapa Bungeni, lakini hazitoki kwenda kuwahudumia au kuwafikia kule. Kwa kweli bado ninaona suala zima la vita dhidi ya maambukizi mapya ya UKIMWI itakuwa ni changamoto kubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu, ukiangalia hata katika hii tafiti ya vijana iliyoanyika, wanaopima wengi ni wasichana; wavulana hawapimi. Kwa nini? Kwa sababu baba zao wenyewe hawapimi; na ukizingatia kwamba malezi yanaanza nyumbani. Baba hana *interest* ya kupima, anasubiria mke wake awe mjamzito, aende akapime kliniki, akishagundulika kwamba yupo salama, basi naye anajiaminisha kwamba yupo salama. Hakumbuki kwamba kuna maambukizi ambayo mwenza mmoja anaweza akawa na maambukizi na mwininge asiwe na maambukizi, unaona.

Mheshimiwa Spika, kama baba hana utamaduni wa kwenda kupima, huyu kijana wa kiume atakuwa na *courage* ya kwenda kupima? Jibu ni hapana. Niwasihisana wanaume, mjitokeze kwenda kupima, kwa sababu ninyi ndio mnaowafuata hata hao wasichana wadogo wenye miaka 20 mpaka 24, ambao wako Vyuo Vikuu, kwenda kuwarubuni, kuwapa vichipsi mayai, kuwanunulia vi-*IST*, ili mwarubuni wapate UKIMWI ambao tayari wanao. (*Makofii*)

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ngoja kwanza. Hii ni kengele ya kwanza au ya pili?

MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA: Mheshimiwa Spika, ya kwanza.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Mnzava kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Festo Sanga.

TAARIFA

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Spika, nataka kumpa taarifa mzungumzaji kwamba anachokizungumza kwamba wanaume hatuna tabia za kupima, siyo kweli. Wanaume tuna tabia za kupima; na hata Wabunge wanaume hapa ndani tupo tayari kwenda kupima afya zetu hapo nje. (*Makofi*)

SPIKA: Kwa hiyo, yupo sahihi basi, hamjapima ndiyo maana mnao utayari wa kwenda kupima. Mheshimiwa Dkt. Christine Mnzava unapokea taarifa hiyo? (*Makofi/Kicheko*)

MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA: Mheshimiwa Spika, silkubali hiyo taarifa kwa sababu utafiti ndivyo unavyoonesha. Ameshasema kabisa kwamba leo nje pale atakwenda kupima, kwa maana hiyo, hajapima mpaka sasa hivi. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba wanaume wengi hawapimi na wana tabia ya kufuata watoto wa shule ambao wana miaka 20 mpaka 24, lakini hata sasa hivi na sisi wanawake kuna wimbi ambalo limetokea, wanawake wengi hasa wenye uwezo wa kipato kuwarubuni watoto wetu wa kiume na kwenda kuwaambukiza virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nitoe shime kwa Serikali yetu chini ya Wizara yetu inashughulikia masuala ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI kwamba tunahitaji nguvu ya ziada kuhakikisha kwamba tunaelimisha watoto wetu, vijana wetu ambao wapo shule za sekondari na vyuo vikuu kwamba UKIMWI bado upo, ni janga kubwa sana la kitaifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niongelee suala la maambukizi mapya ya UKIMWI. Tumekuwa kwenye ziara Kanda ya Ziwa. Kwa kweli maambukizi ya virusi vya UKIMWI bado yapo juu,

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

hasa katika Mkoa wa Mwanza. Kwa survey iliyofanyika mwaka 2016/2017, maambukizi ya UKIMWI yametoka kutoka kwenye asilimia 4.7 kwenda 7.2 ambapo ukilinganisha na ya kitaifa ambayo ni 4.7 unaona kabisa bado kuna maambukizi mapya yanayokuja kwa kasi kwenye mikoa ya Kanda ya Ziwa. Hii ni kwa sababu kuna *highways*, kuna mipaka, kuna migodi mingi, kuna wavuvi na mialo. Kwa hiyo, kuna mazingira hatarishi ambayo yanapelekea wananchi wetu kupata virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, hiyo, naomba basi, kwa bajeti hii ambayo tunakwenda kuipitisha, kwenye masuala mazima ya kupambana na virusi vya UKIMWI, kama Serikali imetenga shilingi bilioni 1.8 kwa fedha za maendeleo za ndani tunaomba izitoe hizo fedha ili afua ambazo zinatolewa ziweze kutekelezeka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kusema kwamba UKIMWI upo, UKIMWI unaoua. Pamoja na kwamba sasa hivi tunajielekeza kwenye magonjwa yasiyoambukiza, kweli yapo na yanatusumbua wengi, hasa Wabunge kwa sababu muda mwangi tunakaa, wengine hatutaki kufanya mazoezi, tunakula vizuri; naomba kabisa kwamba juhudii ziongezeke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, magonjwa yasiyoambukiza ni hatari kushinda UKIMWI, kwa sababu ukiugua Kisukari hapa, ukiugua *Hypertension* na masharti ya vyakula yanabadilika, lakini UKIMWI utakula kila kitu. Kwa hiyo, magonjwa yote yanayoambukiza na yasiyoambukiza ni lazima tupambane nayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, atafuatiwa na Mheshimiwa Yahaya Omary Massare na Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, ajiandae.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia muda huu nami niweze kuchangia hoja ambayo ipo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru hoja ambayo ilitolewa na Waziri Mkuu. Zaidi namshukuru Waziri Mkuu kwa m kutano wake alioufanya Mkoani Kagera, Wilaya ya Karagwe kutoa suluhu na mweleko wa zao la Kahawa Mkoani Kagera. Nadhani tunakoelekea ni kuzuri, hasa sisi ambao tunatoka katika mikoa inayolima zao la kahawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo nitajikita kwenye migogoro ya ardhi. Ninavyoongea leo kuna watu wamelala nje jana. Tuna Kampuni yetu ya ranchi kwa jina mashuhuri, *NARCO*. Kama kuna kitu ambacho wamefanikiwa Mkoa wa Kagera, ni kutengeneza migogoro mikubwa baina ya wakulima na wafugaji. Kwa kweli, *NARCO* ni mtambo wa kufyatua migogoro kuliko ufugaji ambayo ni kazi ya msingi waliopewa na sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kagera, hususani Wilaya ya Muleba, *NARCO* wana ranchi mbili. Wana ranchi Rutoro na Mwisa, lakini wamepata hizo ardhi katika Wilaya ya Muleba kwa njia ambayo mimi kama Mwanasheria sijui walipataje. Bahati nzuri Mheshimiwa Spika ni Mwanasheria, na ninamwona Waziri wa Ardhi yupo hapa. Upatikanaji wa ardhi ya Mwisa ambayo ni mali ya Halmashauri ya Wilaya ya Muleba, hawa watu walivyoipata tuna mashaka makubwa. Nimepitia *GN*zote, tangu mwaka 1960 mpaka leo, nimetafuta *GN*ambayo inawapa uhalali *NARCO* kumiliki ardhi ya Mwisa, sijaipata. Tunapoongea, hawa watu wa *NARCO* wapo eneo la Mwisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, eneo la Mwisa katika Wilaya ya Muleba linahusisha Kata saba; tuna Kata za Kemitembe, Karambi, Kasharunga, Mbunda, Burungura, Ngenge na Rutoro. Ndani ya hizo Kata tunavyo *Vijiji* 12 na *Vitongozi* 19. Eneo lote hilo tunavyoongea wananchi hawajui kama leo watalala kwenye nyumba zao, hawajui kama kesho wataamka kwenye maeneo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba tuna wasiwaso haya maeneo waliyapataje; kwa sababu haya maeneo ni mali ya Halmashauri ya Wilaya ya Muleba, ni maeneo ambayo yanakaliwa na vijiji; na vijiji vimepimwa tangu mwaka 1975 na vingine vimepimwa mwaka 2010, lakini hawa watu wanasesma ni mali yao.

Mheshimiwa Spika, tunazo sheria za nchi hii; tunayo Sheria ya Viji (Land Village Act (No. 5) ya Mwaka 1999, lakini tulikuwa na Sheria ya Land Acquisition Act; tunao utaratibu wa kutoa ardhi ya vijiji; tunao utaratibu kwamba Rais akititaji eneo lolote atalitwaa, lakini kuna utaratibu wa kufanya hivyo. Waziri wa Ardhi ataandaa utaratibu ambao utakuwa gazetted, itatoka *GN then hilo* eneo litatwaliwa kwa matumizi mapana ambayo yana maslahi mapana kwa ajili ya uchumi na matumizi ya Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kinachoendelea, nimeangalia kote huko, hakuna kitu kinachofanyika au kilichofanyika. Watu wamekwenda wamepima maeneo ya Halmashauri, maeneo ya vijiji; na leo tunavyoongea, katika Vitongoji vya Kabwensana, Maigabili, NARCOwanahamisha watu kinyume cha sharia. Hawafuati Sheria ya Ardhi ya Viji, hawafuati sheria ya kuhamisha makaburi ya wapendwa wetu (*Grave Remove Act (No. 9)* ya Mwaka 1999, pia hawafuati mila na desturi za Wahaya. Wanakwenda pale, wanafukuza watu, wanawaambia ninyi mnahama, mnatoka hapa mnakwenda kule, hakuna notice iliyotolewa, Waziri wa Ardhi hajatoa notice kwa ajili ya kuhamisha makaburi kama ilivyo kwenye Graves Remove Act. Watu hawana amani, hakuna usalama kwenye eneo la Mwisa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hili nalisema, nashukuru umekalia Kiti, namwona Naibu wa Waziri ni Mwanasheria, naomba mtusaidie. Hatuwezi kuruhusu vitendo vya namna hii, wananchi wanateseka, wanafukuzwa kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, mbaya zaidi, naomba niliseme hili: lugha inayotumia kule, wanasesma ninyi ni wavamizi. Mimi nashangaa! Mtanzania ambaye amezaliwa Tanzania,

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

amekaa kwenye ardhi tangu mwaka 1975, leo *NARCO* anamwambia ni mvamizi. Tunalipeleka wapi Taifa? *NARCO* wanalo tatizo. Naomba, haya mambo yanayoendelea Kagera na Muleba, hayawezi kuishia Muleba tu, yatakwenda hata kwenye mikoa mingine tusipochukua hatua leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tatizo hili lilianza mwaka 2016 kwenye upande wa Mwisa. Wakavamia eneo, wakaanza kupima. Tulipokwenda kwenye uchaguzi wakanyamaza. Tumemaliza uchaguzi, wameendelea na leo wapo wanaendelea. Nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo, ndugu yangu Mheshimiwa Ndaki Mashimba. Mwaka 2021 alikuja Wilaya ya Muleba kwa ajili ya kutafuta suluhu ya Mwisa, tukakaa tukaenda *field*, tukafanya mikutano na wananchi. Tukawaambia, vijiji ambavyo vimesajiliwa pamoja na vitongoji vyake, kwenye huu mradi wa Mwisa havitaguswa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumetoka kule, hawa *NARCO* walivyo wa ajabu, wakaanza kuwaambia wananchi msiwasikilize wanasiasa. Mimi nashangaa, kama wanasesma msiwasikilize wanasiasa, Diwani ni Mwanasiasa, Mbunge ni Mwanasiasa, wewe Mheshimiwa Spika ni Mwanasiasa; na Bunge hili ni la Wanasiasa; ina maana hawatamsikiliza Diwani, hawamsikilizi Mbunge na hata Bunge lako hawatalisikia. Sasa wengine wa juu yake sitawasemea. Nashindwa kuelewa, hivi *NARCO* hawa, wanatoka Taifa gani? Wanatumikia Taifa gani? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tulikubaliana pale, tukaja na kitu tunakiita *community* ambayo ina maazimio 16. Moja ya Azimio, ambalo ni Na. 16 tukasema Ardhi ya Vijiji pamoja na Vitongoji vyake visiguswe. Tumetoka, leo tunavyoongea, wapo kwenye Vitongoji, wanawahamisha watu kwa nguvu zote. Hapo ukumbuke, hawana *GN* ya kuwapa hiyo ardhi, kwenye makaburi ya watu wanaleta mifugo kulisha pale. Sasa mila zetu ziko wapi? Sheria ziko wapi? Labda kama Waziri amewapa hiyo ruhusa jana, lakini mpaka leo naongea, hakuna taarifa ya kuhamisha makaburi ya wananchi. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Muda umeisha Mheshimiwa. Ahsante sana.

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, atafuatiwa na Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi na Mheshimiwa Nicodemus Henry Maganga, ajiandae.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi hii nami nichangie katika hotuba hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Nami nichukue fursa hii kuipongeza Serikali ya Chama change, Chama cha Mapinduzi, hususan Mheshimiwa Rais wetu, mama yetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri ambayo anafanya hasa sisi Wabunge ambao tunatoka Majimbo ya vijijini. Ametupa heshima kubwa sana, kwa fedha nydingi ambazo zimeelekezwa katika shule zetu, hasa shule chipukizi. Mimi ni mionganoni mwa jimbo ambalo ni Halmashauri na limenufaika sana kwa fedha za Mheshimiwa Rais hizi alizoenda kututafutia huko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kama kiranja wa Serikali. Amefanya kazi iliyotukuka na anakisaidia sana Chama chetu, Chama cha Mapinduzi kutekeleza llani yetu ya mwaka 2025. (*Makofii*)

Mheshimiwa spika, katika Ofisi ya Waziri Mkuu, wanashughulika na vijana ambao ndio waathirika wakubwa sana wa ajira za nchi hii. Tunategemea vijana hawa waajiriwe katika Sekta ya Kilimo. Ofisi hii ya Waziri Mkuu imekuwa inashughulika pia na vitalunyumba, wakitoa mafunzo kwa vijana ili waweze kujajiri katika kilimo hiki cha umwagiliaji wa njia ya matone kupitia vitalunyumba.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo ambalo naomba niishauri Serikali kupitia Ofisi hii ya Waziri Mkuu. Vitalunyumba

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

hivi vinauzwa ghali sana. Vifaa peke yake inafikia takribani shilingi milioni 14 kujenga kitalunyumba ambacho ni cha kawaida. Kwa wananchi wetu masikini na hasa wa vijijini ambao wamekosa ajira; na vijana hawa wamepata elimu lakini ajira hakuna, wana nia ya kujajiri.

Mheshimiwa Spika, naishauri Ofisi ya Waziri Mkuu itenye fedha kiasi kuweka ruzuku katika vitalunyumba ili vishuke bei na wananchi, wale vijana wanaopata mafunzo; ambapo wanatoa mafunzo kwa vijana 100 kwa kitalu nyumba kimoja ambacho kinajengwa katika Halmashauri moja. Sasa kitalunyumba kimoja kinaweza kuendeshwa na vijana watatu mpaka watano. Sasa wale vijana wanaobaki 97 wanakuwa wamepata elimu, lakini hakuna cha kufanya. Naishauri Serikali iweke ruzuku katika vitalunyumba, kwani itaongeza wigo wa ajira katika sekta hii ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, tumeona juzi Mheshimiwa Rais akitoa vitendea kazi zikiwemo pikipiki kwa Maafisa Ugani wetu, lakini tunashuhudia kuona nia ya kuongeza bajeti ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, tunapokwenda kuongeza bajeti ya kilimo, tuhakikishe basi kunakuwepo na matrekti na pembejeo nyingine zikiwemo *power tiller*, plau za kukokotwa na ng'ombe, lakini mbolea. Serikali inatumia fursa hii kuweka ruzuku. Juzi tumeona baadhi ya Wabunge wakichangia na kulalamika, matrekti yaliyoletwa yanakatika kwa sababu hayana ubora. Huko nyuma Serikali yetu ilikuwa na sera mbalimbali za kilimo ikiwemo siasa ni kilimo, hapa tulimsikia Mheshimiwa hapa mwandishi wa vitabu Shigongo akisema. Pia kulikuwa na kilimo cha kufa na kupona na mwisho hapa juzi juzi tulikuwa na kilimo kwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kule nyuma tulikuwa na matrekti bora sana. Yalikuwepo matrekti ya *Ford, Massey Ferguson, John Deere* lakini kuanzia kilimo kwanza tumeanza kuleta matrekti ya ajabu. Kulikuwa na matrekti ya *Farm Truck* mtu anakopeshwa trekta kabla hajalipa deni, trekta limeshaharibika na ndio maana umeona taasisi ile ambayo

ilikuwa inakopesha matrekta SUMA JKT walipotea hapa. Kwa sababu, hasara ile ili kuwa huwezi kuikamata, trekta imeshakuwa *scraper* na mtu bado ana deni. Baadhi ya vijiji vingi na wakulima wengi waliathirika, lakini hii *Ursus* ambayo imeletwa miaka hii ya karibuni ni ya hatari kweli kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa nini tusirudi tukaleta matrekta ambayo yanafaa kwa kilimo cha ardhi ya Tanzania? Matrekta ya *Ford*, *Massey Ferguson*, *John Deere*, matrekta imara ambayo mtu alinunua akiwa kijana na mpaka anafikia miaka 60 kama mimi anaweza kulitumia. Leo trekta zinazwua mpaka shilingi milioni 50, shilingi milioni 60. Kama tunataka kwenda kufanya kilimo kama ilivyo kilimo ni uti wa mgongo basi tuhakikishe Serikali inaweka nguvu kubwa katika kuleta trekta, ambazo ni imara lakini ruzuku ya Serikali iwepo ili ziuzwe kwa bei ambayo mwananchi anaona anaweza kununua. Mwananchi mmoja akinunua trekta watakaolima ni zaidi ya familia 10, kwa sababu akishamaliza kulima shamba lake atamkodisha mwengine, akimaliza atamkodisha mwengine. Hii maana yake ni nini? Tunaongeza kilimo katika fursa ambayo tunaitarajia kwamba iajiri wananchi walio wengi katika Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumeona Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini Serikali kwa ujumla imeifanya Mkoa wa Singida, Mkoa wa Dodoma na Mkoa wa Simiyu kuwa mikoa ya kielelezo, katika kuhakikisha kupunguza *deficit* hii ya mafutam ambayo tunaagiza mafuta ghafi kule nje ili yaje yachakatwe hapa ili tutengeneze mafuta ambayo hayana *cholesterol* yanayotokana na mbegu za alizeti. Serikali ilifanya jitihada sana za kusambaza mbegu japo hazikuwa bora. Dhamira yetu ni kuona sasa basi Serikali inaingia katika kusambaza mbegu bora kabisa za *Hysun* za alizeti ambazo zitakuwa na tija kubwa katika kuzalisha mazao ya kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naendelea kuishauri Serikali iongeze na iendeleesi katika kilimo cha umwagiliaji. Kilimo ambacho kitatoa ajira na ambacho kina uhakika sana na uvunaji, ukiacha kilimo cha mvua ni kilimo cha umwagiliaji. Tuna namna nyingi ambazo baadhi ya mito inapotea,

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

inakwenda kumwaga maji katika bahari na maziwa, tungeitumia ile kukinga mabwawa ya kutosha ili tuweze kupata kilimo cha umwagiliaji. Pia maji ya chini ya ardhi yakinumika yatatusaidia sana kuongeza kilimo, kama njia mojawapo ya kusaidia kilimo cha nchi hii.

Mheshimiwa Spika, ninalo jambo lingine ambalo naishauri Serikali, irudishe Tume ya Mipango ili ibuni vyanzo vingi nya mapato. Tumezoea kujikita katika vyanzo ambavyo ni vile vile miaka nenda, miaka rudi. Kama tusiporudisha Tume ya Mipango, isaidie kuchakata namna bora ya vyanzo vipyta nya mapato, tutaendelea kubaki hapa hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sidhani tunapokwenda tunaongeza shilingi trilioni tatu kwa kila mwaka au shilingi trillioni mbili kutoka 36 kuja 39 bila vyanzo vipyta nya mapato, tutaendelea kuikaba sekta ya mafuta ya petroli, ndio chanzo chetu kikubwa cha mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo hili ambalo limeanza mchakato siku nyingi, naiomba sana Serikali yangu, iikubali na imalize mchakato wa kuchakata *LNG*, gesi yetu ije katika kimiminika iweze kutumika kama mbadala wa mafuta. Magari mengi madogo yaweze kutumia *LNG* ili tutoke katika utegemezi wa kuagiza mafuta. Tumeshuhudia mafuta yalivypanda kutohana na vita ya nchi jirani zinazosakamana na kusukumana za Ukraine na Urusi. Leo dunia inahamanika kwa sababu hii. Kama tungekuwa tumeanza kuichakata gesi yetu na ikatumika kama kimiminika, leo baadhi ya magari mengi yanageanza kutumia *LNG* na tungetokana na tungepunguza kiasi kikubwa cha utegemezi wa mafuta ya petroli katika uendeshaji magari na mitambo yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na ahsante sana kwa nafasi. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi atafuatiwa na Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga na Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa ajiandae.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. IDDI K. IDDI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza kabisa nianze kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu, mama yetu kipenzi, mama Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya. Kwa ridhaa yako naomba basi nitumie *style* ya Mayele kumshangilia Mama Samia Suluhu Hassan kwani anaupiga mwingu sana. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ninavyochangia hapa nina furaha sana baada ya kumwona Mwenyekiti wa Yanga Bunge, Mheshimiwa Gulamali baada ya kunikabidhi kadi yangu sasa ya Yanga kwanza. Sasa najijua ni mwanachama halisi wa Yanga. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie katika maeneo matatu na moja nianze na suala zima la nishati. Nianze kuipongeza Wizara ya Nishati kwa kazi kubwa ambayo inaendelea kuifanya, chini ya Waziri wake Mheshimiwa January Makamba na msaidizi wake Mheshimiwa Byabato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kimsingi...

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Ester Amos Bulaya.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, nimempongeza mwanachama wa Yanga kwa kuonyesha kadi yake na sio kadi tu, ni kadi ya viwango ya timu ya wananchi. (*Makofi/Vigelegele/Vicheko*)

SPIKA: Mheshimiwa Kassim Iddi, unaipokea taarifa hiyo?

MHE. IDDI K. IDDI: Mheshimiwa Spika, ninapokea taarifa hiyo na ninaomba nimshangilie na yeye kwa *style* ya Mayele. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, taarifa.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Mheshimiwa Kassim Iddi kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, tunajua kwamba Yanga wanajitahidi kuigaiga ila tunawaomba waje na kadi za viwango. Simba ya Kimataifa tuna mpaka *VISA Card*, tuna kadi ya wanachama ya kiwango, ukiangalia kadi yao, yaani hadi wanatia huruma.

Kwa hiyo, naomba mchangaje aje achukue hizi kadi za Simba ili wakaboreshe za kwao zaidi kuitia Mwenyekiti wake wa Tawi. (*Makofii/Kicheko*)

SPIKA: Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi unaipokea taarifa hiyo?

MHE. IDDI K. IDDI: Mheshimiwa Spika, taarifa hiyo siipokei kwani Mheshimiwa Nicholaus Ngasa, Mbunge wa Igunga, ameniambia kuwa na kadi ya Yanga pia nimeanza kukopesheka kuwa na sifa. (*Makofii/Kicheko*)

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, mchango wako wa leo una taarifa nydingi sana. Mheshimiwa Stanslaus Mabula.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Spika, naomba tu kumpa taarifa mzungumzaji Mheshimiwa Iddi kwamba, wananchi wanamsikiliza na hayo sio waliyonituma, kwa hiyo aongee masuala ya wananchi. Ahsante sana. (*Makofii/Kicheko*)

SPIKA: Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi unaipokea taarifa hiyo?

MHE. IDDI K. IDDI: Mheshimiwa Spika, taarifa hiyo siipokei kwani waliyonituma hapa ni wananchi na nazungumzia wananchi. (*Kicheko/Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, basi naomba niende moja kwa moja kwenye mchango wangu. Kwanza nianze kwa kuwapongeza Wizara ya Nishati kwa kazi kubwa ambayo wanaendelea kuifanya na hapa niwe mkweli kwamba, suala zima linaloendelea kwa sasa na hasa kwenye mitandao ya kijamii na baadhi ya wachangiaji jana juu ya upandaji wa bei za mafuta katika nchi yetu hii ya Tanzania. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali kwamba katika mfumo huu ambao umeanzishwa na upo, mimi kama Mbunge wa Jimbo la Msalala, naendelea kuwaomba waendelee kuuboresha mfumo huu wa uagizaji wa mafuta. Kwani ni mfumo ambao ni bora sana na hata nchi zingine za jirani wanakuja kuiga mfumo huu hapa Tanzania. Ukiangalia Nchi za Malawi, Zambia tayari wamekuja kujifunza namna bora ya Serikali ya Tanzania tunavyofanya katika uingizaji wa mafuta ya pamoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna hoja ambazo zimeibuka kwamba soko la mafuta liwekwe huria na wapewe wawekezaji binafsi waweze kuingiza mafuta. Nataka tu niuambie umma wa Watanzania kwamba, suala zima la uingizaji mafuta kwa pamoja lina faida zake katika nchi yetu hii ya Tanzania. Moja ya faida ya uingizaji wa mafuta kwa pamoja ni *national security*. Leo hii tunaangalia Nchi za Rusia na Ukraine vita inayoendelea kule, leo kama nchi tukiiachia soko huria la mafuta, upi sasa uhai na usalama wa nchi yetu hii? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba watu tunaochangia katika suala zima hili la mafuta tuweke uzalendo mbele, kuhakikisha , kwamba tunachangia ili kuleta manufaa ya nchi yetu. Nimeona wengi katika suala hili la mafuta wanachangia kuangalia masilahi yao binafsi. Niseme tu kuanzia leo utaratibu huu uendelee kwa sababu, ni utaratibu ambao unalinda uhai na usalama wa nchi yetu. Pia, leo kama mafuta yataachiwa liwe soko huria, sisi kama wafanyabiashara... (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Cassim Iddi ngoja kwanza ni kazi yangu kuwalinda Wabunge humu ndani. Wale wenye mawazo tofauti na ya kwako umewasema hapo kwa ujumla kwamba wanachangia kwa masilahi yao binafsi; na Kanuni zetu zinasema mtu akiwa na masilahi lazima ataje na maslahi yake ya kifedha.

Sasa nataka kukurahisishia una njia mbili; moja, ni ya kusisitiza kwamba wana maslahi, kwa hiyo, sisi tutawataka wao walete hayo maslahi ambayo na wewe unayajua. Au ni kuondoa hiyo kauli ili kila Mbunge humu ndani awe huru kutoa mawazo yake, lakini kama unao uhakika huo, basi uthalisema kwa namna hiyo. (*Makof*)

MHE. IDDI K. IDDI: Mheshimiwa Spika, naomba kuondoa kauli hiyo, lakini niendelee kusisitiza kwamba, tunapokwenda kuchangia ni lazima tuangalie maslahi ya wananchi wetu ambao wametutuma.

Mheshimiwa Spika, niendelee kwa kusema kwamba upatikanaji wa mafuta kwa bei ambayo iliyopo sasa ni utaratibu ambao ni wa Serikali umeendelea kudhibiti mfumuko wa bei kupanda na kushuka na kuhakikisha kwamba, hao waagizaji wa mafuta wanaagiza kwa pamoja, sambamba na kutangazwa *tenderya* pamoja ili kuweza *ku-control/bei* ya soko la Kimataifa. Kwani tunafahamu kwamba hata visima vya mafuta vinavyouza mafuta haviuzi moja kwa moja kwa muuzaji wa mafuta ama kampuni yoyote, isipokuwa wameteua *ma-agent* kwenye nchi zao huko ambao wanaauza mafuta kwenye nchi nyingine hizi za jirani. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niendelee kusisitiza kwamba utaratibu huu Serikali iendelee kuuboresha vizuri, lakini niishauri tu kwamba hapa suala ni kuhakikisha ya kwamba wanajitahidi sasa, kuangalia zile gharama na kodi mbalimbali ambazo zimekwa waweze kuzifanyia kazi, waziondoe ili kupunguza gharama ya mafuta. Tukumbuke sakata hili linafanana moja kwa moja na sakata la vinasaba. Wapo waliokuja hapa wakasema Kampuni ya *GFI* haifai

inatunyonya na Serikali ilisikia ushauri huo ikaenda kuondoa na kuwapa *TBS*. Hata hivyo, baada ya siku tu kupita wale wale waliokuwa wanaipiga vita *GFI* walirudi wakaanza kusema kwamba sasa *TBS* haina uwezo, baada ya kuona sasa mianya ya mafuta yameanza kuingia ambayo yanachakachuliwa. Kwa hiyo, niombe tunapokwenda kujadili hili suala hasa katika kuzingatia usalama wa nchi yetu tuweke uzalendo mbele.

Mheshimiwa Spika, niendelee kuchangia sasa upande wa TAMISEMI. Hali ya barabara katika maeneo yetu ni mbaya sana na hasa nizungumzie sasa kwenye Jimbo langu la Msalala. Barabara ni mbovu sana. Leo hii tunazungumzia ukuaji wa kilimo kwenye maeneo yetu, leo hii tunazungumzia ukuaji wa viwanda kwenye maeneo yetu, lakini vyote hivi haviwezi vikaenda sambamba kama miundombinu ya barabara haitarekebishwa. Niombe Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Naibu Waziri nadhani yupo hapo ananisikia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na changamoto kubwa sana kwenye maeneo yetu haya, hasa katika usimamizi wa fedha ambazo zinakwenda kwenye kukarabati barabara. Leo hii utaona *tender* nyingi za barabara zinatangazwa wakati wa mvua. Niendelee kuwaomba Mheshimiwa Waziri na Wizara kwa pamoja waweke mkakati sasa wa fedha hizi ambazo tutakuwa tumezipitisha kwenye bajeti, ziende zikaendelee kukaa pale hata wakati wa mvua zisiende zikachukuliwa tena huko mbele. Pia, waweke usimamizi madhubuti katika kuhakikisha kwamba wakandarasi wanaopatikana kwenye maeneo yale ni wakandarasi amba moja, wana sifa za kuhakikisha ya kwamba wanatekeleza miradi ile kwa wakati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la pili, wakandarasi hao wawe *financially fit* kwa ajili ya kuhakikisha kwamba miradi ile wanakwenda kuitekeleza bila kusuasua na wala kutegemea mikopo kwenye mabenki. Kwani kuwapa wakandarasi amba moja hawana uwezo kwenye maeneo yetu ndio kunapelekea kucheleweshwa kwa barabara nyingi sana.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, leo hii nitazungumzia miradi katika eneo langu la Kata ya Jana, Kata ya Mwaruguru, Kata ya Mwanase, maeneo haya ni wakulima wa mpunga. Nimpongeze Mheshimiwa Bashe kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kugawa vitendea kazi kama pipipiki na kuendelea kuthibitisha kwamba mama yetu Samia Suluhu ametoa fedha nydingi kwenye kilimo. Matunda hayo hayawesi yakaenda kuleta matokeo kama barabara zetu kwenye maeneo ya uzalishaji zitakuwa ni mbovu. Leo hii tunaongea barabara hizo hazipitiki. Niiombe Wizara wajaribu kuangalia namna gani na njia bora ya kuhakikisha kwamba barabara hizi zinaanza kutengenezwa mapema kabla ya mvua, ili wananchi sasa wa kwenye maeneo yale waendelee na uzalishaji katika maeneo hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana muda wako umekwisha Mheshimiwa.

Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga atafuatiwa na Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa na Mheshimiwa Anne Kilango Malecelea ajiandae.

MHE. NICODEMAS H. MAGANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru kwa kunipa nafasi kwa siku ya leo tena ili niweze kuchangia kwenye hotuba ya Waziri Mkuu. Nimeisoma hotuba ya Waziri Mkuu Mpango wa Bajeti mwaka, 2022/2023 kweli imekaa vizuri sana. Hivyo sasa, nitumie nafasi hii tu kumuombea kwa Mwenyezi Mungu Mheshimiwa Waziri Mkuu, kama alivyokusudia kwenye malengo yake aweze kutufanya kazi Watanzania.

Nimeangalia katika ukurasa wa 22 amezungumzia Mahakama ambazo zinakwenda kujengwa katika Taifa letu, ikiwemo na Wilaya yangu ya Mbogwe. Kweli nauunga mkono huu Mpango kwa asilimia mia moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kukupongeza wewe kwa kuchaguliwa kuwa Spika wetu wa Bunge Tukufu pamoja na Baraza la Mawaziri wapya pamoja na Manaibu wale waliochaguliwa kwa mwaka huu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, niombe sasa kutoa mchango wangu kuiomba Serikali, wajaribu kuzingatia hao Mawaziri waliochaguliwa kufuatilia zile kumbukumbu. Wale Mawaziri waliokuwepo kwamba, kuna ahadi ambazo walizitoa kwenye Majimbo yetu kwa ajili ya kuwatumiakia wananchi wetu. Vile vile, niombe kuwasilisha mawazo ya wengi wananchi wangu wa Jimbo la Mbogwe wananipenda sana na wamenitura kuja kuyasema mahali hapa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kweli yapo mengi yanazungumzwa na hayana budi kuyakwepa kuyazungumza mahali hapa, maana sisi ndio washauri wa Serikali. Ugumu wa maisha unaongoza sasa hivi mitaani na ugumu huu wa maisha kiukweli kama alivyotangulia kusema Mheshimiwa Iddi hapa, unachangiwa na *issue* ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, naomba ku-*declare interest* tu kwamba mimi ni muuza mafuta japokuwa alitaka kuliweka vibaya sana lakini wewe ukalinyoosha vizuri, kwamba, asitunyime kutoa mawazo yetu japokuwa kwamba sisi ni wadau wa sekta hiso, tuishauri vizuri tu Serikali ili kusudi kila mmoja aweze kufaidika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini, tumekuwa tukishauri hata kwenye Kamati, kwamba, vipo vyombo vyaa Serikali ambayo vinachangia kumuumiza mwananchi. Ukiangalia *EWURA* ina masharti mengi sana na tumeshashauri huko kwamba, wabadilishe miongozo ili watu waweeze kufungua vituo vyaa mafuta vijijini. Leo kwenye Jimbo langu kuna baadhi ya sehemu mafuta yanauzwa mpaka Sh.5,000/= kwa lita moja sio Sh.3,000/= peke yake. Sh.3,000/= ni kwa wale walio na vituo vyaa mafuta, lakini yakiingia kwenye makopo kwa wananchi walio wengi ambako hakuna huduma za *petrol station* wanauza wanavyotaka wananchi hao. Kwa hiyo, kuna kila sababu

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

tuiombe Serikali iliangularie upya na ilete miongozo hiyo haraka sana, tuifanyie mabadiliko, watu waweze kufungua vituo kwenye hayo maeneo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, kwenye upande wa barabara hapa, wananchi wanatamani sana kuona barabara zinatengenezwa kila mahali. Jimbo langu la Mbogwe ni kubwa lina kata 17 na kila kata ina barabara za msingi, zinaingiza pato la Taifa pamoja na pato la halmashauri. Jimbo langu linahitaji kuongezewa bajeti ya *TARURA* ili kusudi Meneja wangu wa *TARURA*, aweze kurekebisha barabara zinazotakiwa kurekebishwa kwenye hiyo Wilaya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, wananchi wanahitaji kuona umeme unatengenezwa kwenye maeneo yao. Vipo vijiji ambavyo bado havijawekewa umeme na tumekuwa tukiongea kila wakati humu Bungeni kwamba umeme sasa hii awamu iende kukamilika.

Mheshimiwa Spika, jambo la nne, wananchi wanahitaji kuona maji kwenye maeneo yao. Wananchi kiukweli hawana mambo mengi sana pamoja na kwamba, mipango ni mingi sana ya Serikali, lakini naishauri Serikali iangularie vitu vya msingi tu vichache, vitatu ama vitano ili kuweza kuwasaidia wananchi wetu waliotuweka madarakani. Kwa sasa kwa kweli hali ni ngumu sana, uchaguzi ungekuwa ni kesho au keshokutwa, tulikuwa na asilimia chache sana ya kurudi humu Bungeni maana hali ni mbaya. Ukiangalia wananchi kiukweli mtu wa kwanza wanayemlalamikia ni Mbunge na wanatufuatilia sana na wanatuangalia kwamba, Mbunge wetu anaishauri nini Serikali.

Mheshimiwa Spika, jambo la Nne wananchi wanahitaji kuona maji kwenye maeneo yao. Wananchi kiukweli hawana mambo mengi sana pamoja na kwamba mipango ni mingi sana ya Serikali, lakini ninaishauri Serikali iangularie vitu vya msingi tu vichache, vitano ama vitatu ili

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kuweza kuwasaidia wananchi wetu walioituweka madarakani.

Mheshimiwa Spika, kwa hali ilivyo sasa kwa kweli hali ni ngumu sana, uchaguzi ungekuwa ni kesho au keshokutwa tulikuwa na asilimia chache sana ya kurudi humu Bungeni maana hali ni mbaya. Ukiangalia wananchi kiukweli wanamlalamikia mtu wa kwanza ni Mbunge na wanatufatilia sana wanatuangalia kwamba, Mbunge wetu anaishauri nini Serikali.

Mheshimiwa Spika, mimi nitumie nafasi hii kuishauri Serikali ione namna gani mwananchi anaenda kumpunguziwa ugumu wa maisha. Tukiangalia mfano Serikali ya Awamu ya Kwanza, Awamu ya Pili, Awamu ya Tatu na Awamu ya Nne tulikuwa tuna vyanzo vingi, hapakuwa na tozo lakini maisha yallienda. Hapakuwa na tozo kwenye mafuta na kwenye miamala, lakini watu wallishi kwa raha mustarehe, leo hii tuna ndege, tuna meli kwenye maziwa yetu huko pamoja na bahari yanaingiza kwenye Pato la Taifa.

Kwa hiyo, niiombe Serikali sasa ikae ifikirie wananchi hawa kulingana na kilio kwa vile ngoma ikilia sana hupasuka, maana kilio ni kikubwa sana. Kila kijiwe ukikaa unakuta watu wanaliongelea hilo tu kwamba maisha yamepanda sana, maisha yamekuwa magumu sana, nauli imeongezeka kutoka shilingi 1,000 mpaka shilingi 5,000 ukiingia kwenye huko kwenye Wilaya zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niiombe Serikali ilione hilo kama jambo la msingi sana ili kuwasaidia wananchi hawa wawzeze kuishi maisha mazuri.

Mheshimiwa Spika, jambo jingine hapa ninaiomba Serikali kwenye Wilaya yangu sina chuo cha VETA. Na ukisoma kwenye ilani ya Chama chetu cha Mapinduzi tuliinadi kwamba, kila Wilaya itakuwa na Chuo cha VETA. Niiombe Serikali sasa ione namna iweze kunisaidia kwenye Jimbo langu kupata chuo cha VETA.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, pia jambo linguine ni taa za barabarani. Kwenye kampeni tulikuwa tukinadi kila patakapojengwa lami kutakuwa na taa za barabarani. Kwangu sina taa za barabarani na Mji wangu unakua kwa kasi sana wa Mbogwe na Masumbwe. Kwa hiyo, niiombe Wizara inayohusika na haya mambo waweze kunisaidia wananchi wangu wapate umeme na waondoke gizani ili waweze kunufaika na utawala huu tulionao wa Awamu ya Sita.

Mheshimiwa Spika, jambo jingine, nikucombe wewe uendelee kutulinda tu sisi ni vijana wako ni wageni humu ndani. Twaweza kuwa tunakukosea kweli, maana hatukusoma chuo kuja kuwakilisha watu humu, kila mtu na lafudhi yake. Kwa mfano, mimi lafudhi yangu inaeleweka ninaweza nikawa ninazungumza kama kwa ukali sana, lakini kumbe ndivyo nilivyo tu. Ninaomba kwa unyenyekevu mkubwa niweze kusikilizwa na niweze kusaidiwa vizuri sana pale ninapochangia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nzungumzie kwenye hotuba hii ya Waziri Mkuu, ukurasa wa 36, amezungumzia *issue* ya pato la madini. Niiombe Serikali sasa iangalie haya mapato yanayokusanywa kwa wingi kuna sehemu Serikali haiwezeshi. Wachimbaji hawa wadogo hakuna fungu ambalo limetoka Serikali Kuu kama zinavyofanya sekta nyingine.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kilimo wanatoa matrekta, wanakopesha matrekta, lakini wachimbaji wadogo ambao hatujawasaidia hawa na wanafanya vizuri ni vyema wakatengenezewa miundombinu angalau ya barabara kwenye migodi yao.

Mheshimiwa Spika, ipo migodi inayozalisha kila siku, lakini haina miundombinu ya barabara, hakuna vituo vya afya kwenye maeneo yale. Dada pale amezungumza UKIMWI unaenea kwa kasi kubwa sana Kanda ya Ziwa, ni kweli watu wanaishi kwa shida, lakini ukiangalia tozo ambazo zinakusanywa ni nyingi na suala hili tumeshalishauri kwenye Kamati. Ninakuomba tu Mheshimiwa Waziri Kaka yangu na

umekuwa Waziri wa mfano wa kwanza, maana katika makusanyo nimeangalia kabrasha huko Mawaziri waliopita hakuna Waziri ambaye amewahi kukusanya Bilioni 528 kama mwaka jana, sasa hivi imefika Shilingi Bilioni 400.6 ina maana unaonesha jinsi gani ulivyo mwaminifu Kaka yangu, hongera sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikuombe kwa vile wewe unakaa na Rais mwambie kabisa ukweli kuanzia wewe mwenyewe unatokea sehemu za machimbo, una mgodi wa namba moja, namba saba, hakuna miundombinu ya kutosha kwenye maeneo yale, lakini wananchi hawa ni waaminifu wanaingiza patola hatari kwenye Taifa, aone fungu ili kusudi aweze kutusaidia wachimbaji wetu wapate manufaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mchango wangu leo naomba nikomee hapo ili Serikali sasa iweze kutusaidia tuweze kuishi maisha mazuri na yenye raha. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Nicholaus George Ngasa, atafuatiwa na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela. Kwa namna muda unavyoonekana pale tutakuwa tumemaliza, lakini kama michango itakuwa ni mifupi basi, tutamalizia na Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao.

MHE. NICHOLAUS G. NGASSA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rais wetu Samia Suluhu Hassan kwa kuonesha dira madhubuti katika kuongoza nchi yetu na kuna maeneo manne ambayo mpaka sasa tunasema Mheshimiwa Rais ameupiga mwingi.

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza ni kusimamia ulinzi na usalama wa nchi yetu, eneo la pili ni kusimamia maendeleo na ustawi wa Taifa, eneo la tatu ni kuimarissha utangamano na Jumuiya za Kikanda pamoja na uhusiano wa Kimataifa na eneo la nne ni kulinda tunu za Taifa letu ikiwepo umoja, amani, mshikamano, kulinda Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, lakini pamoja na Muungano wetu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Hongera sana Mheshimiwa Rais tunakuombea kwa Mwenyezi Mungu akupe afya njema uendelee kutuongoza vyema. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, nimesimama kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, pia nimpongeze Mheshimiwa Kassim Majaliwa pamoja na Wasaidizi wake kwa kuendelea kufanya vyema katika kusimamia shughuli za Serikali, pia na kuziratibu shughuli za Serikali pamoja na Bunge.

Mheshimiwa Spika, mimi nitachangia maeneo mawili ya kisera. Eneo la kwanza nitaongelea suala la usimamizi madhubuti wa fedha za umma na eneo la pili nitakalochangia ni suala la uchumi shindani, uchumi jumuishi kwa ajili ya maendeleo ya watu.

Katika mchango wangu moja utajikita kwanza katika kupitia *document* niliyonayo, llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, hotuba ya Mheshimiwa Rais ya mwezi Aprili mwaka jana 2021 na Sheria ya Fedha za Umma (*Public Finance Act, No. 6, ya 2001*), lakini pia na Sheria ya Fedha za Umma za Serikali za Mitaa (*The Local Government Finance Act*) ya mwaka 2019. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina mifumo mbalimbali ya udhibiti wa fedha za umma, mimi nitajadili mifumo miwili. Mfumo wa kwanza ni unaosimamiwa na ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Hesabu za Serikali kwa maana ya *Internal Auditor General* na mfumo wa pili ni ule unaosimamiwa na Ofisi ya Mdhibiti na Msimamizi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa maana ya *CAG*, chini ya ofisi ya *National Audit Office* ambayo ni Ofisi ya Ukaguzi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, unapokwenda kwenye Halmashauri zetu kwa sasa tunasema kwenye Majimbo, mama pochi lake limefunguka fedha nyingi zinakwenda. Pamoja na fedha hizi nyingi kwenda tunahitaji mifumo Madhubuti ili tuweze kuzisimamia fedha hizi ili ziweze kutoa matokeo kama ambavyo tunatarajia.

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza ni kuhusu ukaguzi wa ndani kwenye Halmashauri zetu. Unakwenda kwenye Halmashauri kwa mfano Halmashauri ya Wilaya ya Igunga tuna Kata 35 na tuna Vijiji 119, lakini tuna Mkaguzi wa Ndani mmoja tu. Ujisoma Sheria ya fedha ya Serikali za Mitaa na Sheria ya Fedha za Umma inataka hawa watu pamoja na majukumu yao mengine ya ukaguzi, lakini wahakikishe wanafautilia ile michakato yote ya shughuli zinazofanyika kwenye Halmashauri ambako fedha za umma zinakwenda. Kutokana na uchache wa hawa watu wanajikuta muda mwingi wanaishia kukagua risiti za manunuzi na kukagua vocha za malipo, wanashindwa kuangalia michakato ya fedha zinakokwenda kwa ajili ya kuleta mwandeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ndugu zangu, viongozi wangu na chama chetu sasa inabidi tuangalie hili suala tuweze kuongeza rasilimali watu katika hill eneo ili tuweze kusimamila vizuri rasilimali zetu za fedha. Kwa hiyo, katika hili jambo tuwe makini tuhakikishe tunaongeza watu, tuungeze rasilimali watu, tusijikite katika kuwajengea tu uwezo. Unapokuwa na mtu mmoja anasimamia ukaguzi katika Halmashauri moja ambayo ina Vijiji vingi na Sheria hii ya Fedha ya Serikali za Mitaa inasema kabisa huyu mtu anatakiwa kukagua mpaka akaunti za Halmashauri za vijiji, sasa vijiji 119 yuko mtu mmoja katika hali ya kawaida vinaweza kumzidia na asiweze kufanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mbadala wake ni nini ama *alternative?* Sheria hii ya Fedha za Umma mwaka 2010 ilifanyiwa maboresho na Bunge likapendekeza kuanzhishwe kitengo kinaitwa kitengo cha usimamizi wa vihatarishi Serikalini (*Risk Management Unit*). Baadhi ya sehemu wameanzisha idara kama Benki Kuu ya Tanzania na baadhi ya maeneo wameanzisha vitengo, lakini bado kuna changamoto kubwa kwenye Halmashauri nydingi wameweka *ma-champion* tu, ambao utendaji kazi wao pia ni mdogo.

Mheshimiwa Spika, faida ya kuwepo vitengo vyatya usimamizi wa vihatarishi ni nini? Yule mtu wa ukaguzi anapoendelea kuhangaika na ukaguzi wa vocha zile za

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

malipo, anapohangaika kukagua risiti za manunuzi huyu mtu wa vihatarishi ye ye anaangalia zile *process* na kuhakikisha anatoa *assurance* kwa hizi taasisi zetu za Serikali, Wizara, Idara za Serikali pamoja na mamlaka mbalimbali. Kwa hiyo, niwaombe Serikali kupitia Wizara ya Fedha na kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu waweze kulisimamia hili ili Idara zetu, Wizara zetu na Taasisi zetu wahakikishe vitengo vyta vihatarishi vinaimarishwa katika Taasisi zao ili viweze kutoa *assurance* ya michakato mbalimbali ya *investments* na shughuli mbalimbali za Serikali zinazofanyika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo ningependa kulichangia la kisera, linahusu uchumi wa kisasa, shirikishi na shindani. Ilani yetu ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, Ibara ya 18 imeliongelea hili, lakini pia hotuba ya Waziri Mkuu eneo la 14 imelielezea hili. Unapoongelea uchumi shindanishi maana yake lengo letu ni kufungamanisha hizi sekta za uzalishaji na mimi hapa kwa kifupi nitaongelea sekta ya kilimo, lakini pia na sekta ya viwanda.

Mheshimiwa Spika, asilimia zaidi ya 65 mpaka 70 ya Watanzania wako kwenye sekta ya kilimo, sasa kama tunavyoona Serikali imeanza kuweka mikakati mbalimbali ya kuimarisha kilimo tunachokiolomba sasa hivi hali ya hewa nchini imekuwa haitabiriki, mvua hazitoshi, pia ukijaribu kuangalia pamoja na kutoa pembejeo maeneo mengi uzalishaji unakuwa mdogo, kwa sababu gani?

Mheshimiwa Spika, hali ya hewa, kuna mabadiliko ya tabianchi, tujikite sana kuwekeza katika kilimo cha umwagiliaji. Niwaombe Wizara ya kilimo, maeneo yenye skimu za umwagiliaji kama kule kwetu Igunga tuna skimu ya Mwanzugi ni kubwa sana, tuna Bonde la Wembele ambalo maji kwa mwaka mzima yanaishia tu yamekaa hayafanyi kazi, waboreshe hizi skimu, wazihuishe ili tuweze kuongeza uzalishaji. Hii itasaidia hata kupatikana kwa malighafi katika viwanda.

Mheshimiwa Spika, naweza nikatoa mfano mdogo hapa, hapa nchini sasa hivi tuna uhaba wa mafuta ya kula,

kwa sababu mwaka jana kufika mwezi wa Tisa viwanda vingi vya uzalishaji wa mafuta ya kula vilikosa malighafi uzalishaji ni mdogo. Sisi huku tumeweka tozo za kulinda masoko ya ndani ya mafuta ya kula, tunadhibiti yale masoko ya nje, sasa yanapopungua, soko la ndani bidhaa zimekwisha, tunapoanza kutegemea bidhaa na mafuta kutoka nje matokeo yake yanakuja kama sasa hivi tunajikuta bei inaongezeka na kunakuwa na malalamiko ya wananchi kupanda kwa bei ya bidhaa, hususan mafuta ya kupikia au mafuta ya kula. Kwa hiyo, ninaomba tunapoweka hizi kanuni za kulinda masoko ya ndani, tuhakikishe kabisa tunakuwa na uthabiti wa kuhakikisha sekta ambayo inalindwa iwe na uwezo wa kujitosheleza kuzalisha, kama ni kilimo iweze kuzalisha malighafi za kutosha ziweze kwenda katika viwanda ili tuwe na bidhaa muda wote na tusijikute kwamba tunasababisha mlipuko wa bei.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ambalo naweza kulichangia kwa kifupi sana ni katika suala la uchumi shirkishi, lengo letu pia ni kuhakikisha tunaboresha mazingira ya wafanyabiashara. Niwapongeze Halmashauri ya Jiji la Dodoma wameweza kuanzisha soko zuri sana la wamachinga hapa ambalo lipo katikati ya Mji. Hii ndio namna ambayo tunaweza tukasema tunaboresha mazingira ya wafanyabisahara wadogo, huwezi ukatoka unasema unaenda kujenga soko la wamachinga kilometra 10 nje ya mamlaka ya Mji inakuwa ni ngumu. Kwa hiyo, unapoweka mazingira kama haya maana yake unaongeza mzunguko wa fedha, lakini pia ajira kwa wananchi, ajira kwa vijana zinapatikana kwa wingi, nasi kama ilani yetu ambavyo tumeahidi basi tunajikuta kwamba, tumeimarisha na tumeboresha biashara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa ni suala la urasimu. Tuombe kabisa pia Serikali sera zetu ambazo tunaenda tunapoboresha, hizi sera za kuhakikisha kwamba tunalegeza kuhakikisha kwamba tunalinda masoko ya ndani na kuongeza uzalishaji katika sekta ya uzalishaji tujikute tunapunguza urasimu. Mtu anapohitaji kuwekeza kama ni kiwanda au shughuli nyininge yoyote ya uzalishaji mali asijikute

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

anatumia muda mwengi katika kutafuta vibali na kuzungushwa makoridoni.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Naunga mkono hoja asilimia mia moja. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Anne Kilango Malecela.

MHE. ANNE K. MALECELÀ: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, mimi leo nitaongea kwa kifupi, kwanzza nianze kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi, nimpongeze Rais Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Kwanza wa Rais, Waziri Mkuu pamoja na Baraza la Mawaziri lote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya nchi yanaletwa na Serikali pamoja na wananchi. Naomba niseme kwamba, kwa kipindi hiki cha Awamu ya Sita mwaka wa kwanza, Serikali ya Chama cha Mapinduzi imefanya kazi kwa bidii zote sana na sisi tulioko huko Majimboni wananchi wanaendelea kufarijika. Mpaka hapo nafikiri nimeanza kwa kifupi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa niingie kwenye jambo ambalo nataka kulichangia kwenye hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Naomba nichangie jambo moja tu, sekta ya uzalishaji, Fungu Namba 37 - Kilimo.

Mheshimiwa Spika, nikiongea kilimo kama Mbunge wa Same Mashariki, zaidi ninakwenda kugusa kilimo cha tangawizi. Nagusa kilimo cha tangawizi kwa sababu, ndani ya Jimbo langu mimi Tarafa mbili zote, Tarafa ya Mambavunda na Tarafa ya Gonja, wananchi wanategemea kilimo cha tangawizi, lakini nikizungumza kwa Tanzania, Tanzania kuna Mikoa ambayo inalima tangawizi sana, Ruvuma inalima tangawizi, ukija Mbeya wanalima tangawizi,

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Morogoro wanalima tangawizi na Mikoa mingine imeanza kulima tangawizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi naomba kwa Tanzania niachie hapo, sasa nije kwenye tangawizi ulimwenguni.

Mheshimiwa Spika, hili zao sisi watanzania, zao la tangawizi, tunaliona kama ni zao ambalo halihitaji kipaumbele kabisa, naweza nikasema tunalipuuza. Twendeni duniani huko, tuanze na India. India kwa ulimwenguni ni Taifa la kwanza kwa kulima tangawizi, nakiri kwamba, wao hawa-*export* zaidi kwa sababu wao wenye kama India wanakula sana tangawizi, lakini ukiangalia India kwenye soko la dunia anapeleka asilimia 43.81 karibu anafikia asilimia 50. Na hizi *data* ninazungumza nazipata *August* mwaka 2021, mwaka jana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nchi ya pili ni Nigeria. Nigeria ni Taifa liko Afrika, lakini Nigeria ni namba mbili duniani kwa kupeleka tangawizi kwa wingi kwenye soko la dunia. Anapeleka asilimia 16.94 ni nchi ya Afrika hiyo. Nchi ya tatu ni Uchina.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi leo niongee kwa vivu, roho inaniuma. Ukiamuangalia Nigeria vizuri, naomba ndugu zangu mum-*google* vizuri, Nigeria analima tangawizi vizuri sana anapeleka kwenye mfuko wake wa Taifa, *GDP* anapeleka kutoka kwenye tangawizi anapeleka asilimia 23, siyo ndogo. Asilimia 23 kwenye *GDP* itoke kwenye tangawizi, siyo kidogo, ina maana Nigeria wanafanya kazi kwa bidii kuliangalia zao la tangawizi.

Mheshimiwa Spika, ukija ukimuangalia Nigeria huwezi kumtofautisha sana na sisi. Mimi nimeangalia kwa nini ye ye anapeleka asilimia 23 kwenye *GDP* ya Taifa lake, ni kwamba Serikali imesimama imara sana kwenye kilimo cha tangawizi kwenye nchi ya Nigeria, imesimama imara kwa kuboresha miundombinu ya kilimo cha tangawizi. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, sasa mimi kwa nini naongea kwa wivu? Serikali ya Tanzania inashindwaje?

Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 2000 niko humu ndani ninaongelea tangawizi, ninazungumzia tangawizi, ninazungumzia tangawizi. Serikali inasema hivi, inasema vile, naomba kipindi hiki, nazungumza kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu, lakini Waziri wa Kilimo asimame awajibu Watanzania wanaolima tangawizi kwa nini hili zao tunaliweka kama ni zao si kipaumbele?

Mheshimiwa Spika, nirudi tena niongee kwa uzito na ninyi mtani-*support*. Mwaka 2019 tulipata *Covid 19*, tangawizi ndiyo iliyotusaidia sana. Kila Daktari akisimama kuleni tangawizi, kila Dakrati akisimama tumieni tangawizi, lakini zao hili Serikali naomba nizungumze kwa uchungu, sikufurahi sana hakuna Waziri wa Kilimo, lakini hakuna hata Naibu Waziri wa Kilimo, *anyway* atasoma kwenye mitandao, kwa nini Serikali haioni umuhimu wa kuliangalia hili zao vizuri? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa huu ni mwaka wa 22 nikisimama ni tangawizi mpaka wengine wananiita tangawizi, lakini *it is fine*. Naomba Serikali kipindi hiki izungumze inaiangaliaje tangawizi kwenye nchi hii?

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Same Mashariki wanaongoza kwa kile kilimo, lakini mioundombinu ya kilimo cha tangawizi Same Mashariki inaumiza roho. Wananchi wanatengeneza wenyewe hakuna wataalam, lakini bado wanaongoza kwa kulima kilimo hiki. Serikali iseme kwa nini haipeleki wataalam wa tangawizi, zile sehemu zinazolimwa tangawizi?

Mheshimiwa Spika, nimekwenda Madaba nikalima tangawizi eka 20, nimelima kule, miundombinu ni hivyohivyo kama Same Mashariki, hapana! Upande wa kilimo, Serikali nazungumza kwa malalamiko hamjawa *serious*. Upande wa zao hili la tangawizi wala hamlijali, lakini tulipopata *Covid...*

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Anne Kilango Malecela kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mwanaisha Ulenge.

T A A R I F A

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Spika, naomba kumpa taarifa mama yangu kwamba ni sahihi kabisa anavyozungumza kwamba...

SPIKA: Ngoja, ili Taarifa Rasmi za Bunge zikae vizuri, unampa taarifa Mheshimiwa Anne Kilango Malecela.

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Nampa taarifa mzungumzaji Mheshimiwa Anne Kilango Malecela kwamba, anayoyazungumza ni sahihi kabisa, Serikali yetu siyo tu haijalipa kipaumbele zao la tangawizi, lakini hajatoa kipaumbele kwa mazao yote ya viungo nchini Tanzania ambayo yanaingiza fedha nyingi nchi za jirani. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Anne Kilango Malecela unapokea taarifa hiyo?

MHE. ANNE K. MALECELA: Mheshimiwa Spika, napokea na ninamshukuru sana Mheshimiwa.

Mheshimiwa Spika, wakati namalizia nikwambie ukweli kabisa Serikali isimame imara kuangalia haya mazao. Inachagua mazao kidogo inayafanya kazi, haya ambayo inayapuuza kwenye nchi nyingine kama Nigeria yamepeleka asilimia 23 kwenye *GDP* ya nchi. Sasa ninajiuliza aah! kwani hawa wa-Nigeria wao wakoje, sisi tukoje?

Mheshimiwa Spika, ukiangalia hali ya hewa ya Jimbo la Kaduna kule Nigeria ndiyo hali ya hewa iliyopo Ruvuma, ndiyo hali ya hewa iliyopo Kilimanjaro. Serikali imechukua

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

serious sana mazao ya viungo, lakini sisi tunayapuuza, hapana. Serikali katika hili mimi sitakubali. (Makof)

Mheshimiwa Spika, mimi nimejitahidi nilipoingia mwaka 2005 Jimbo la Same Mashariki, nilipoona wale wananchi wanalima sana tangawizi, nilianzisha ujenzi wa kile kiwanda. Naishukuru sana Serikali, nashukuru mbia aliyejuka kutuunga mkono kujenga kile kiwanda cha tangawizi pale Same Mashariki. Ukweli sasa tunagawana sisi pamoja na mshirika mwenzetu, lakini bado sasa hivi nazungumza tena nikiwa ninajivuna, Tanzania, Mamba Miamba tuna kiwanda cha kusindika tangawizi ambacho Afrika Mashariki hakipo, lakini Serikali inatusaidiaje? Tuna kiwanda, kilimo kiko wapi?

Mheshimiwa Spika, kile kiwanda ni kikubwa mno, kinahitaji tangawizi nyingi sana. Serikali isipokuwa imara kuboresha klimmo cha tangawizi hata kile kiwanda kitakuwa hakina maana. (Makof)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nasema ahsante sana. (Makof)

SPIKA: Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu mbalimbali kuhusu hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nitaje majina tutakayoanza nayo mchana, Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao, Mheshimiwa Innocent Seba Bilakwate, Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, Mheshimiwa Conchester Leons Rwamlaza na wengine tutaendelea kuwataja kadri michango itakavyokuwa inaendelea.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ndio tuko kwenye hoja ya kwanza kabisa kwenye hoja kadhaa za bajeti zitakazokuja mbele yetu, tutakuwa tunaendelea kukumbushana mambo taratibu ili michango yetu iwe inafuata Kanuni zetu. Niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge tukumbuke kujadili hoja badala ya watu kwa sababu Kanuni zetu zinataka hivyo, tujadili hoja badala ya watu. Kwa hivyo, hata kama mtu amechangia hoja fulani wewe shughulika na hoja aliyoizungumza badala ya

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kushughulika na yeye kama mtu kwa sababu itakuweka mazingira ambayo yanakuwa siyo mazuri sana kikanuni. Kwa hiyo, ukitaka kukubaliana na hoja ama kutofautiana na hoja ya mtu fulani, lakini siyo kukubaliana na mtu au kutokubaliana na mtu.

Kwa namna hiyohiyo, niwakumbushe tena matumizi ya takwimu ni zile ambazo unaweza kutuambia umefanya utafiti au kama siyo wewe umefanya basi kuna utafiti fulani umefanyika ambao unaonesha takwimu fulani, lakini usitengeneze takwimu zako za kufikirika halafu ukazileta humu ndani kwa sababu, utavyoambiwa uthibitishe utapata wakati mgumu.

Waheshimiwa Wabunge, leo nilimuacha Profesa Kishimba alisema asilimia 90 ya wasomi wanajua kusoma na kuandika, lakini hawana maarifa. Niliachache ile illi nilitumie kama mfano. Takwimu za namna ile humu Bungeni haziruhusiwi kwa sababu, hujafanya utafiti wa kujua wasomi wale ni asilimia 90 wanajua kusoma na kuandika na hawana maarifa, kwa hiyo lazima utuoneshe nani aliyefanya huo utafiti. Kwa hiyo, muelewe hiyo imepita, lakini utaratibu wa matumizi ya takwimu uko namna hiyo. Huwezi kuamka tu wewe ukaona mimi ninavyoona, mimi ninavyoona, hapana, siyo wewe unavyoona, lazima useme takwimu zile zenye uhalisia.

Waheshimiwa Wabunge, jambo lingine ambalo nataka kuwakumbusha ni kuhusu orodha ya wachangiaji. Niliwahi kusema hukonyuma, lakini niwakumbushe tena kwa sababu tutakuwa hapa muda mrefu, kama miezi mitatu hivi. Anayekuwa amekaa hapa mbele kama ni mimi au mtu yeyote atakayekuwa ananisaidia hapa mbele anayo mamlaka ya kuita mtu yeyote aliyeko kwenye orodha kuchangia au mtu mwengine yeyote aliyemuomba kuchangia ikiwa yeche ameona kuna sababu za kufanya hivyo.

Waheshimiwa Wabunge, hivyo, msiwe mnakuwa na wasiwasi, unakaa ukihesabu kwamba mimi nilikuwa namba moja mbona nimeitwa wa nne, wa tano, wa sita, wa saba,

aah! mpe nafasi aliye hapa mbele kuongoza kikao. Wale wanaoleta orodha hapa mbele siyo waongoza kikao, wao wanaleta orodha kwa maana ya wachangiaji ambao wanatakiwa kusomwa hapa. Kwa hiyo, sababu huwa ziko nyingi, mwingine Mbunge mgonjwa kwa hiyo, lazima apewe nafasi ili aweze kuwahi hospitali, mwingine Mbunge anaenda kwenye Kamati lazima apewe kipaumbele kwa sababu Kamati yake imeita Kikao, mwingine Mbunge ameitwa sehemu Wizarani kuna jambo anaenda kufuatilia, mwingine anaenda Jimboni kwake kuna changamoto. Kwa hiyo, sababu huwa ziko nyingi kwa nini hapa mbele wanaweza wakaitwa Wabunge wengine badala yako wewe uliyekuwa wa kwanza. Kwa hiyo, ile orodha unaweza ukauliza jina langu limo ama halimo?

Waheshimiwa Wabunge, ndiyo maana unaweza ukawekwa kwenye orodha leo, lakini bado yule anayeendesha hapa akasema utachangia kesho, muda umekwisha au hata wakati mwingine maswali huwa hayaishi yote, anasema tutaeendelea siku nyingine haya maswali yatapangiwa ratiba. Kwa hiyo, tutoe nafasi kwa Kiti kuongoza Kikao.

Jambo lingine ni Mawaziri. Kuna michango hapa imetoka, lakini ilikuwa inaashiria kwamba, wangetamani wawepo Mawaziri hapa kusikiliza hoja na ninyi ni mashahidi mimi nasisitiza jambo hilo siku zote. Kwa hiyo, ukiona hawapo hapa ndani na mimi sijasema jambo ujue ninazo taarifa kuhusu wao kutokuwepo hapa ndani na hizo taarifa uwe na uhakika tu Spika wako nakulinda vizuri Mheshimiwa Mbunge, hizo taarifa ujue kabisa ni taarifa muhimu na katika kupima imeonekana wawepo huko kwa wakati huu badala ya kuwa hapa, kwa sababu yote yanahitajika kufanyika. Kwa hiyo, msiwe na wasiwasi hoja zote Waheshimiwa Wabunge mnazozitoa humu ndani zitajibiwa wakati wa kujibu hoja hii ambayo iko mbele yetu, yale ambayo yanahitaji kujibiwa, lakini mengine ambayo yatajibiwa kwa maandishi mtajibiwa kwa maandishi na yale ambayo wanatakiwa wayachukue kama mawazo wakayafanyie kazi, msiwe na wasiwasi yatafanyiwa kazi.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Waheshimiwa Wabunge, hivyo Waheshimiwa Mawaziri wako wengine ambao wamesafiri kwa vibali maalum kabisa na wako wengine wameenda kumuwakilisha Rais kwenye mikutano mbalimbali huko, wengine wameenda kwenye tukio muhimu kabisa la sensa. Ninyi mnafahamu nchi yetu itakuwa kwenye sensa mwaka huu kwa hiyo, Mawaziri wengi wameenda pia kwenye Kikao hicho ambacho ni muhimu sana kwetu Wabunge ili tujue kwenye maeneo yetu wananchi wako wangapi ili tunapoleta hapa takwimu kwamba maendeleo huku mmeweka bajeti kidogo, basi unasema kwangu watu ni wengi kuliko huku.

Sasa hizi takwimu kama nilivyosema hatuwezi kuzipata kama hawa Mawaziri hawatakuwa sehemu ambayo wapo siku ya leo na wengine kama nilivyosema wamesafiri nje ya nchi kwenda kumuwakilisha Mheshimiwa Rais na namna hiyo. Hizi fursa tunazozizungumza humu ndani lazima watu wetu waende huko wawepo. Kwa hiyo, msiwe na wasiwasi Waheshimiwa Wabunge Mawaziri hawa waliopo, lakini pia utaratibu wetu wa Ofisi ya Bunge kuwapelekea taarifa zitawafikia, wala si lazima wazitafute kwenye mtandao, watafikishiwa kwa utaratibu wa kawaida.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo nasitisha shughuli za Bunge mpaka Saa Kumi kamili jioni leo.

(Saa 7.00 mchana Bunge lilitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)

(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirejea)

SPIKA: Waheshimiwa tukae, Katibu.

NDG. HUSSEIN ATHUMANI – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Ofisi ya
Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023**

(Majadiliano yanaendelea)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, na hapa wako Wabunge ambao hawakupata fursa ya kuchangia, na sasa nitaanza kuwaita ili wapate nafasi hiyo ya kuchangia mchana huu. Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao, atafatiwa na Mheshimiwa Innocent Seba Bilakwate, Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi ajandae.

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Na mimi naomba nichangie Muswada huu wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa niaba ya wananchi wa Sengerema kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, nimesikiliza Wabunge wenzangu wakichangia kuhusiana na suala la mafuta na kulalamika bei ambazo zinavyopanda sasa hivi bei zimefikia katika kiwango cha juu ambacho hakijawahi kufikiwa katika historia ya nchi hii. Naomba nirejee kidogo kwa ajili ya kuweka *hansard* ikae sawa.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1982, 1983 na 1984 Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilipata tatiozo (*crisis*) ya mafuta ikabidi kutumia mafuta ya *furnace*; lakini wakati huo yalikuwa ni masuala ya kiuchumi, ambapo Mheshimiwa Hayati Julius Kambarage Nyerere ilimlazimu sasa kwa kutumia TPDC alikwenda Algeria, Saudi Arabia na kwa wenzetu Kuwait wakakubali kutupa mafuta hali ikaja ikawa nzuri.

Sasa hali inavyokuwa mbaya kama kwa sasa hivi ambako tunakoelekea ni suala sasa la Mheshimiwa Rais tunamuomba, mama yetu Samia Suluhu Hassan sasa ni wakati wa kwenda mwenyewe mahala ambapo kuna hali ngumu kama hii mama asafiri yeye mwenyewe Rais wa nchi akazungumze na hawa wazalishaji wa mafuta ili tuweze kupata mafuta ya gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, huu mfumo wa PPBA mimi nakumbuka ulianzishwa kama si 2012 ni 2014, na leo hii mfumo huu una miaka 10. Si vibaya kama nchi kuangalia, kwamba je, mfumo huu bado uko sahihi tuendelee sisi kama nchi

kuutumia? Sisi kama nchi mfumo huu je, una madhara gani na una faida gani kwetu?

Mheshimiwa Spika, faida ya kwanza iliyopo kwenye mfumo wa *PPBA* ni kwamba tunaweza kutathmini na kutabiri kodi yetu ya mapato kwa miezi miwili, kwa sababu kuna mafuta yatakuwa yameagizwa kwa miezi miwili tunajua kodi yetu tunayokuja kuikusanya hiyo ni faida kubwa ya kwanza. Ya pili ni kupata uhakika wa kuwa na mafuta katika miezi miwili inayokuja

Mheshimiwa Spika, lakini yako madhara sasa ambayo yanaletwa na taasisi hizi mbili, *PPBA* pamoja na *EWURA*. Taasisi hizi ni kwamba ziko chini ya Wizara ya Nishati. Hawa wenzetu wa *EWURA* mguu mmoja wako Wizara ya Maji, mguu mmoja wako Wizara ya Nishati; na hao ndiyo wanaokuja kupanga bei ya mafuta, hao, kwa mamlaka ambayo iliyopitishwa na Bunge, ndio wanaokuja kupanga bei ya umeme. Sasa hii *EWURA* iangaliwe iwekwe wapi kwa maslahi mapana ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusiana na hili suala la *PPBA*, ni kwamba ye ye ndiye anayepokea zabuni za mafuta, zabuni za uagizaji wa mafuta na zabuni za utangazaji wa bei ambazo ye ye anajua sasa kwamba fulani ameshinda kutohana na hali hii.

Mheshimiwa Spika, tunalo Shirika letu la Mafuta (*TPDC*) Shirika hili a mafuta wakati wa marehemu Rais Julius Kambarage Nyerere pale *Tipper* aliwekeza ye ye pamoja na wenzetu wa *CALTEX* kutoka Italy, Tanzania ikawa na asilimia kama sijasahau 51 au 49; lakini nafikiri ni 51 *CALTEX* wana asilimia 49. Hata hivyo, Baba wa Taifa hakuishia pale, ni kwamba tukawa na shirika letu la BP. Katika BP Serikali ikawa ina asilimia kule 51 na BP wakawa na 49. Hii inaonesha namna gani Baba wa Taifa alikuwa amejiandaa kukabiliana na hii hali. Sasa kule Caltex wana 49 na huku BP wana 49 hizo ni sehemu ambazo mafuta yetu sisi yangeweza kupitia katika *angle* hiyo.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, lakini huyu *TPDC* anazalisha gesi pia. Si kwamba hana mtaji lakini pamoja na kuwa anazalisha gesi anaidai *TANESCO*. Mpaka Januari mwaka huu *TPDC* peke yake anaidai *TANESCO* billioni 502. Ukichukua mwezi huu wa Februari ukachukua na Machi na sasa hivi huu mwezi huu wa Aprili utakapoisha *TPDC* atakuwa anaidai *TANESCO* billioni 652. Huyu *TPDC* ni kwamba anayo kampuni tanzu inaitwa *TANOIL* ambayo imetengenezwa kwa ajili ya ku-supply mafuta kwa nchi kama hali ya nchi inakuwa mbaya. Tumekwenda kuanzisha *TANOIL* wakati tayari sisi kule PUMA tuna asilimia 51. Tumekwenda kuanzisha kule kwenye *Tipper* kule kuna *CALTEX* ambako kuna *storage* kubwa ya kuhifadhi mafuta; zaidi ya lita milioni 300 tunaweza tukahifadhi pale *Tipper*. Pia, bado tungeweza kujenga uwezo pale *Tipper* tukaweza kuhifadhi mafuta yetu.

Mheshimiwa Spika, sasa leo *TPDC* anadai billioni 652 na hana mtaji; sasa hili linakuwa ni tatizo kubwa sana. Mimi ushauri wangu kwa Serikali ni kwamba wamlipe, waje hapa wanatueleza kwamba wanamlipa lini *TPDC* apate pesa ya kuagiza mafuta. Mashirika kama haya yako nchi zote duniani. Ukienda Algeria, Misri nan chi nyingine zote zinazotuzunguka ina nguvu kubwa, isipokuwa sisi Tanzania hili Shirika limekuja kuonekana mfu kama halina kazi. Lakini kama tungekuwa tumeagiza mafuta yetu ikitokea shida tunafungulia mafuta yetu.

Mheshimiwa Spika, sasa nakupa mfano, *TPDC* ameshinda tenda ya Januari kwa *premium* ya kuagiza mafuta bei ya gharama ya mafuta kuyaleta hapa Tanzania kwa dola 26, amekuja kuomba mwezi wa pili amenyimwa kazi, amekuja kuomba mwezi wa tatu huu amenyimwa kazi. Uzalendo hakuna huko *PPBA*.

Mheshimiwa Spika, tunamuomba Mheshimiwa Rais tunamuomba aiangalie *PPBA* kwa haraka mno hawa ni watu ambao watamletea tatizo kubwa kwenye nchi hii. Vilevile Mheshimiwa Rais aiangalie *EWURA*; hatuwezi kukubali. Tarehe 22 imekuja meli ina mafuta, hii meli ilikuwa inaitwa *MTSL Falcon*, ilikuwa na tani 39. Watu wa *TBS* wamekwenda kuipima

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wakasema kwamba asilimia 90 ya vyumba vingine mafuta yake yako bora asilimia 10 mafuta si mazuri. Hawa *Adax* ambaao ndiyo walikuwa wamepewa *tender* wakaondoa ile meli wakaipeleka Beira.

Mheshimiwa Spika, kuagiza yale mafuta tayari Serikali imepoteza bilioni sita, sawa na bilioni 14 ilhali yale mafuta asilimia 90 yangeshushwa na asilimia 10 iliyobakia yale ndiyo yakarudishwa; lakini yale mafuta yakaachwa yote yakaondoka yakaletwa mafuta mengine na zile *LC* zilizokuwa zimefunguliwa zikabadilishwa. Uzalendo! Uzalendo ni bidhaa adimu sana katika nchi hii. Huyu Mheshimiwa Rais tutamsaidiaje kwenye hali kama hii? Hili ni tatizo kubwa sana mfumo wa *tender* wa *PPBA* uangaliwe.

Mheshimiwa Spika, na hivi tunavyozungumza na wewe leo kuna kampuni ambazo tayari zimeshinda *tender* ya kuja kuua wananchi. Leo kuna kampuni iko hapa, naangalia *Adax* huu mzigo uliokuja alikuwa na dola 28 kwa *premium* kwa usafiri wake, kuna hawa *Vitol Bahrain* wakapewa dola 72. Yaani kuna mtu amepewa *tender* ya dola 28, kuna mtu amepewa *tender* ya dola 72 kwa tani. sasa dakika hizi na jambo hili ni kubwa sijui nifanyeje nakuomba sasa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Dakika moja malizia, unaweza ukachangia kwa maandishi mchango utafika tu, dakika moja malizia.

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Amepewa Agusta kwa dola 53, amepewa *traffic* Gula kwa dola 44,000, akapewa *TPDC* kwa dola 26 inauma sana. Leo huyu *TPDC* ana kosa *tenderyuko PUMA* ndiyo mwenye hisa na sisi anakosa *tender*. Nchi hii naomba mengine yaliyobakia niyaache kwa usalama wa Taifa ahsanteni sana. (*Makofii/Kicheko*)

SPIKA: Mheshimiwa Tabasam tunakushukuru kwa mchango huo lakini naamini hapo kuna hoja za kisheria. Kwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

sababu sheria za manunuzi tulitunga sisi hapa kama zinaleta changamoto basi hizo changamoto ni sisi hapa wa kuzitatau.

Lakini kama hizo sheria hazifuatwi huko unakosema hiyo itakuwa changamoto kubwa; nadhani Serikali iko hapa Bungeni ijaribu kuyatazama hayo lakini kama wamefuata sheria kile ambacho wamekifanya hata sisi tunataka wafuate sheria. Sasa kama hawajafuata sheria hicho walichokifanya basi wafuate sheria kwa sababu kutakuwa hakuna sababu ya kutengeneza sheria halafu sheria hizo zikawa sisi wenyewe ndiyo tunataka tena zivunjwe. Kwa hiyo mlitazame hilo alilolizungumza hapo Mheshimiwa Mbunge.

Waheshimiwa Wabunge nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Innocent Seba Bilakwate atafatiwa na Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza ajiandae.

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuchangia. Awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenipa afya na nguvu ya kuendelea kuwatumikia wananchi wangu wa Jimbo la Kyerwa. Pia nichukue nafasi hii kipekee kuishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi nzuri zinazofanya chini ya mama yetu Samia Suluhu, hasa hasa kuleta pesa nyingi ya maendeleo kwa wananchi wetu. Ni ukweli usiopingika pesa inakuja na miradi inaendelea vizuri.

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa nataka nzungumzie kwanza upandaji wa bidhaa. Ni vizuri tukaeleza hapa ukweli. Nilikuwa najaribu kufuatilia taarifa za *EWURA*; ukifuatilia taarifa za *EWURA* mara nyingi Waheshimiwa Mawaziri na wengine wamekuwa wakisema bidhaa zimepanda kwa sababu ya mafuta. Hebu tuangalie taarifa za *EWURA* zinasemaje kuanzia mwezi wa 12 mpaka sasa.

Mwezi wa 12 mwaka jana bei ya mafuta kwa Dar es Salaam ilikuwa ni shilingi 2510 na kwa Kigoma kule Uvinza ilikuwa ni shilingi 2754 mwezi wa pili mwaka huu bei ya mafuta ilishuka ikawa shilingi 2480 kwa Dar es Salaam na kule Uvinza

Kigoma ikawa 2720, maana yake ilishuka kwa shilingi 30. Tukaja mpaka mwezi wa tatu bei ya mafuta ilikuwa ni shilingi 2500 kwa Dar es Salaam mpaka 2784 kwa Uvinza kule Kigoma.

Sasa Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wanaotusikiliza lazima tueleze ukweli. Bidhaa zilizopanda mimi niseme ukweli hazitokani na upandaji wa mafuta. Kwa sababu ukija kuangalia hapa hizi takwimu za *EWURA* haiwezekani hii shilingi 60 ambayo imepanda kwenye soko la mafuta ndiyo iongeze bei kiasi hiki. Mimi nitoe mfano, kule kwangu kuna sabuni mbili tunazozitumia, kule Kyerwa. Sabuni ya nyota mwezi Januari ilikuwa inauzwa shilingi 1,000 lakini mpaka sasa ile sabuni inauzwa shilingi 3,500. Sabuni ya mkwano ilikuwa inauzwa shilingi 2,000 leo hii hiyo sabuni inauzwa shilingi 5,000. Hivi hii shilingi 60 ilioongezeka kwenye soko la mafuta ndiyo imepandisha bidhaa kiasi hiki?

Mheshimiwa Spika, lakini ukija kwenye mafuta ya kula ni jambo ambalo ni la ajabu. Mafuta yaliyokuwa yanauzwa shilingi 1,700 leo hii haya mafuta ni shilingi 3,500. Yaani hii haikubaliki. Ukienda kwenye vifaa hivi vya ujenzi, mimi mwaka jana mwezi wa 12 niliagiza pale kwenye vifaa vya ujenzi vya *aluminum*; pale nilivyoagiza wakanipa *quotationya* shilingi millioni 18. Nimekwenda juzi wananiambia hivyo vifaa bei imebadilika ni millioni 35. Waheshimiwa Wabunge na Watanzania lazima tuwaeleze ukweli. Suala la kusema mafuta yamepanda tuongee tarehe sita juzi, siyo miezi hii miwili mitatu iliyopita, hili haliko sawa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi ninachokiona kwenye suala la upandaji wa mafuta tunaongelea kipindi hiki cha juzi, lakini miezi mitatu kule nyuma mafuta yalikuwa hayajapanda kiasi hiki cha kuweza kupandisha bidhaa zikapanda namna hii hili haliko sawa. Mimi nilichokiona baada ya kufutilia hawa wanaouza wameachiwa uhuru wameamua kujitawala kufanya wanavyotaka.

Mimi niombe tumsaidie Mheshimiwa Rais, tusiende na hoja ya kusema bidhaa zimepanda kwa sababu ya mafuta. Leo hii tukianza kutangaza sawa kwa sababu mafuta

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

yameongezeka takriban kwa 500 zaidi. Kwa hiyo mimi ninapิงa suala la kusema bidhaa zimepanda kwa sababu ya mafuta kupanda.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nilisemee ni kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa maamuzi ambayo ameyafanya kule Kagera kwenye suala la kahawa. Kwa uchumi wa mkoa wa Kagera tunategemea sana kahawa, na hawa wakulima wamesahaulika kwa muda mrefu. Kwa hiyo mimi nipongeza Serikali kwa hatua ambayo umechukua na kuruhusu kahawa kuuzwa kwenye *AMCOS*.

Mheshimiwa Spika, kahawa ilikuwa inauzwa kwenye Vyama Vikuu, wanakusanya na ndio wanauza, lakini Vyama Vikuu kimekuwa ni kichaka cha kuwanyonya wakulima na kuwaibia. Sasa niombe sana Waheshimiwa Wabunge wale ambao wanatoka kwenye mikoa inayolima kahawa tuunge mkono utaratibu huu. Mimi mwaka jana nilliomba Serikali, nikaomba huu utaratibu utumike angalau waangalie unaendaje. Mwaka jana tumeujaribu, utaratibu huu ni mzuri wa kuuza kahawa kwenye vyama vya msingi; kwa hiyo ninapongeza sana Serikali kwa hatua hii ambayo imefikia.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine, ili nchi hii iweze kuwa, pamoja na vipaumbele vingine, tunaona Serikali imeanza kuwekeza kwenye kilimo ambacho kimesahaulika kwa muda mrefu. Nliombe sana Serikali wampe nguvu Mheshimiwa Bashe, kazi anayoifanya ni nzuri. Serikali iongeze pesa tuingie kwenye kilimo ambacho kina tija kilimo ambacho kitakuwa na faida kwa nchi lakini pia kwa mkulima. Leo hii ukienda kwenye viwanda vyetu tunaagiza bidhaa na malighafi nje kwaajili ya kuleta kwenye viwanda vyetu.

Mheshimiwa Spika, fedha za kigeni zinaenda nje, kitu ambacho hakijakaa sawa. Hii nchi Mungu amejalia, tuna vipindi virefu vya mvua, tuna udongo mzuri, ukiingia kule kwetu Kyerwa ni raha tupu. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali, tuwekeze kwenye Kilimo ambacho mkulima akihitaji mbolea anaipata kwa wakati, mkulima akihitaji mbegu bora, azipate

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kwa wakati. Ninaamini nchi hii tunaweza tukatumia kilimo na kikaongeza fedha yingi kwenye uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine la kusemea ni hawa watumishi wanaojitolea. Juzi Serikali imetangaza kuajiri. Kuna watumishi wamekuwa wakijitolea muda mrefu. Hawa watumishi inapofika wakati Serikali inapotaka kuajiri, hao wanaojitolea huwa wanaachwa. Sasa naiomba sana Serikali, hao watumishi ambao wamejitolea muda mrefu, Serikali iwape kipaumbele ndio waanze kupewa nafasi. Kwa hiyo, hili naomba Serikali iliangularie, kwa sababu hili jambo ni muhimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo linguine, *MSD* wameshindwa, lazima tueleze ukweli. Sijui pale kuna mdudu gani? Kipindi cha nyuma alikuwepo yule kijana anaitwa Laurian, allikuwa anafanya vizuri, tunapata dawa kwa wakati. Wakaingiza fitina, sijui nini na nini, hata kesi yenye we aliyofunguliwa hatuioni, lakini madudu tunayoyaona ndiyo haya. Hakuna dawa, hali ni mbaya huko vijijini. Kwa hiyo, naomba sana Waziri anayehusika, huyu bwana waliyemweka pale, kama ameshindwa, wamweke pembedi watafute mtu ambaye anaweza akawapatia wananchi dawa kwa wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, haya mambo ya kulea watu, huko vijijini hali ni mbaya. Hili haliwezekani, ni lazima tuelezane ukweli. Mtu kama ameshindwa kazi, akae pembedi, wanaoweza kazi waendelee.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru, ahsanteni sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, atafuatiwa na Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza na Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, ajiandae.

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nami awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa mambo yafuatayo:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, kwanza kwa kuiruzuku nchi yetu kuwa hapo ilipo kwa maana ya jiografia. Nalisema hilo makusudi, kwani leo hii tukizungumzia habari ya ardhi, iwe ni ardhi nzuri; watu wanazungumzia habari ya kilimo, habari ya maziwa na vitu vingine vyote, mimi narudi kumpelekeea shukrani Mwenyezi Mungu kwa kuturuzuku hayo yote. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, *point* yangu moja ya msingi, kuna bahati moja mbaya unapokuwa na kila kitu, unaweza ukafika sehemu ukashindwa kujua uanze na kipi. Ndiyo maana nataka kuleta *point* ya kwamba pamoja na haya yote mengi mazuri, ni lazima tuwe na vipaumbele. Hatuwezi tukafanya kila kitu, lazima tuwe na vipaumbele. Nami niseme, kwa mfano, tukizungumzia habari hii niliyosema ya ardhi nzuri; ardhi nzuri ni jambo moja na matumizi bora ya ardhi ni jambo lingine. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama tutafika sehemu tukijua tu tuna ardhi, ardhi, ardhi, tukaachana na matumizi bora ya ardhi, hautaacha kuona nchi hii ikiendelea kuwa kwenye migogoro ya ardhi, hautaacha kuona nchi hii ikiwa kwenye uzalisha duni. Kwa hiyo, naendelea kushauri na kusisitiza matumizi bora ya ardhi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nikitoka hapo, najua kwa ruzuku hiyo hiyo, tunazungumzia habari ya uwekezaji katika maziwa. Ni jambo jema, lina afya. Nami ukizungumzia kule kwangu Katavi, ndiyo maana tuna uwekezaji mkubwa wa Bandari ya Karema. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, *point* ni nini? Leo hii tukifanya vizuri katika eneo hilo, changamoto tunazokutana nazo za kuhakikisha labda mizigo yetu inapita kupitia nchi nyingine, tutakwepa hilo. Tukiwekeza vizuri katika hizo bandari, nakuhakikishia tutakuwa na uchumi mkubwa. Kwa wale waliobahatika kufika *DRC*, uchumi wa maeneo yale ni mkubwa. Sasa tunafanyaje ili kuweza ku-*take* uchumi huo? Ni pamoja na uwekezaji huu katika Ziwa Tanganyika na maziwa mengineyo. Naomba nitoke hapo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nilifurahishwa kwenye hotuba ya Waziri Mkuu kuhusu Sera za Mapato na Matumizi; lakini eneo hili kwa ujumla wake, kama kila kitu kikifanyika vile ilivyotakiwa, basi kelele zingekuwa ni chache. Nalisema hilo kwa sababu gani? Pale tunaambiwa kwa maana ya Sera za Mapato na Matumizi, tumeelekezwa kwamba usimamizi madhubuti wa fedha za Umma, lakini yawepo maeneo yenye tija bila kusahau ajira na uchumi wa mtu mmoja mmoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikiyasema hayo, tafsiri yake ni nini? Leo hii tunazungumzia habari ya uwezekaji na kwa maana nzima ya uwekezaji kuvutia wawekezaji. Pale tumeambiwa, kwa kuvutia uwekezaji, tunaweza tukazalisha ajira takribani 62,301. Nasema kuvutia wawekezaji, ni jambo moja, lakini tunasemaji kuhusu Watanzania hawa?

Mheshimiwa Spika, niseme jambo moja, tukifurahi kuona wawekezaji wanakuja, nami hapa naomba ni-*declare interest*, mimi ni mchimbaji mdogo wa madini. Katika eneo hilo la uwekezaji nimeshiriki kwa kina na mafao nayapata katika eneo hilo. Kwa hiyo, hata mimi naweza nikatoa darasa kwa wenzangu.

Mheshimiwa Spika, kama nchi, wakati tunazungumzia habari ya uwekezaji, tunafanyaje kwa maana ya kumsaidia Mtanzania? Je, kama nchi, tumetengeneza mazingira ya kumwandaa Mtanzania na mikataba ya Kimataifa? Maana kuna wakati mtu anaingia kichwa kichwa katika masuala hayo. Tutafika mahali Watanzania wenzangu watabaki kuwa watazamaji. Kwa sababu wanakuja watu ambao kwanza wana-*financial muscles*. Wana msuli wa kifedha, wanamkuta Mtanzania ambaye kwa sababu hajaandaliwa kwa maana ya elimu ya mikataba na vitu vingine, unaweza ukamkuta ye ye na ardhi yake ambayo Mwenyezi Mungu amemruzuku, akaona kama haina thamani, akafikiri thamani ni kwa huyu tu anayekuja. Kumbe ye ye huyu mtu ni tajiri, lakini hajatengenezewa mazingira ya kujua kwamba ana utajiri wa kiasi hiki. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kwa eneo la uchimbaji. Bahati nzuri niseme mikakati mizuri inayoendelea katika nchi yetu, mtu mmoja anaweza akafika sehemu akaingia mkataba, kwakuwa mtu mmoja ana mashine, ana fedha, na kadhalika, yeye kama hajatengenezewa mazingira ya kujua, kuelimishwa zaidi na kupewa elimu ya mikataba, ana ardhi yake ambayo labda kama ingekuwa imethaminishwa, kwamba bwana wewe hapa tulipo mashapo ya eneo lako ni kiasi hiki na hiki. Kwa hiyo, unapokwenda kwenye meza, nenda ukiwa kifua mbele, ukijua na wewe ni kama alivyo yeye. Haya yote, naiomba nchi yangu na Serikali iendelee kufanya jambo hilo jema la kuhakikisha tunawasaidia wananchi wetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, naomba nitoke hapo kwenye eneo la elimu ya uwekezaji, kuna suala lingine la mwingiliano wa majukumu, taasisi za udhibiti na masuala mazima ya tozo. Kama hatutafika sehemu tukajaribu kuendelea kuona namna ambavyo kila taasisi inavyoingiliana na taasisi nyingine, masuala hayo ya tozo na vitu vingine vya namna hiyo, tunaweza tukakuta wakati mwингine tunarejesha nyuma ari ya watu kujituma katika maeneo hayo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kuna suala la UVIKO na athari za UVIKO. Nafarijika kuona miradi mbalimbali ambayo imetengenezwa, lakini kama nchi, tumebaki na darasa lipi? *Point* yangu ya msingi ni hiyo. UVIKO kwa ujumla wake, angalia jinsi dunia ilivyosambaratika, angalia kila mtu alivyotamani kubaki kwake. Sasa katika mazingira haya ya kubaki kwetu, iwe ni somo. Kwa maana gani?

Mheshimiwa Spika, katika mazingira ambayo mtu wetu alikuwa anatakiwa labda akatibiwe India, Marekani au Uingereza, kwa somo lile la UVIKO unafika mahali unaona kumbe kama nchi, tuna kila sababu ya kuendeleza miundombinu yetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana naishukuru sana Serikali. Leo hii ukiichukulia Jakaya Kikwete pale, hata ukija tu Benjamin, shughuli zinazofanyika pale, uwekezaji mkubwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

uliofanywa na Serikali, hata kama ilikuwa UVIKO imetufikisha mahali ambapo tumefungiwa milango, kumbe unaweza ukafungiwa milango, lakini ukawa katika *position* ya baadhi ya mambo kujihudumia *internally*. Nilikuwa nasema, tukifurahia mambo mengine kwamba tumejenga madarasa, *well and good*; vituo vya afya, *well and good*, lakini somo pana tunalolipata ni lipi? Maana yake, tuendelee kujitegemea. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza, atafuatiwa na Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu na Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, ajiandae.

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika hoja ilio mbele yetu ya Bajeti ya Waziri Mkuu. Napenda pia kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametukutanisha tena hapa leo kama ilivyo ada kila mwaka kwamba tunakaa hapa kupitisha bajeti, tunaiangalia nchi yetu, tunaipanga kwa sababu tunatafsiri mipango yetu katika fedha.

Mheshimiwa Spika, nina uhakika kwamba tunapopitisha bajeti, ni vyema pia tukapima mafanikio yake. Tunapaswa kuangalia tija iliyotokana na fedha tulizozitoa, lakini pia tunapaswa kuhakikisha kwamba tunapata muda kama huu wa kuweza kusahihihisha na kutoa ushauri kutokana na mambo mbalimbali ambayo yametekelezeka au hayakutekelezeka katika bajeti iliyopita.

Mheshimiwa Spika, nina hoja kama moja au mbili kuhusu bajeti ya mwaka huu. Nipo kwenye Kamati ya LAAC, tunakutana na Halmashauri mbalimbali, tunafanya vikao, tunahoji na tunatembelea kukagua ufanisi wa miradi. Yapo mambo mbalimbali ambayo tumeyaona, lakini mimi nitaongelea hoja moja ambayo nimeona ni kero ya aina fulani katika bajeti tunazozitoa na matumizi ya fedha za Serikali.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, katika ziara na vikao la LAAC, tumegundua kwamba kuna Halmashauri zinapewa fedha, fedha hizo zinatolewa mwishoni mwa mwaka; tuseme kama kwenye tarehe 15 mwezi wa Sita. Halafu baada ya hapo, hizo fedha kabla hazijafanya kazi yoyote, zinarudishwa Hazina inawezekana kwa kadri ya sheria ilivyo. Je, fedha hizo zinaporudishwa Hazina, Serikali inapata tija gani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu fedha zinarudishwa wakati miradi haijakkamilika, lengo linakuwa halikutimizwa, lakini fedha zinavyorudishwa kule Hazina, hazirudi tena Halmashauri. Kwa hiyo, miradi inakwama. Unaweza kukuta miradi inakaa miaka saba mpaka minane haijakkamilika.

MBUNGE FULANI: Eh!

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Spika, nitoe mfano kwenye Halmashauri ya Shinyanga, walipewa shilingi milioni 500 mwezi wa Tano mwaka 2021; tarehe 26 mwezi wa Sita, zikarudishwa Hazina. Tumekwenda kuikuta katika Halmashauri ya Mbarali, tumeikuta Busokelo na Msalala. Sasa mambo kama haya Serikali inasemaje? Kwanini itoe fedha na fedha hizo kabla hazijatumika, malengo yake hayajatimizwa, halafu zinarudishwa Hazina? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hoja yangu kubwa ni: Je, fedha hizo zinaporejeshwa Hazina, zinakwenda kukaa katika kifungu gani na katika Akaunti ipi? Fedha hizo sijawahi kuona hata CAG amekagua na kuzisemea. Nani anakuwa *accountable* wa fedha hizi? Kwa mfano, unapoenda kwenye Halmashauri wao watakuonesha kwamba tumepewa bajeti, lakini tulikuwa na fedha fulani labda shilingi milioni 500, sasa tumeongezewa shilingi milioni 500, tulikuwa na bakaa, watakuonesha; lakini kwenye bajeti kuu bakaa hii huwa hatuioni. Lazima Serikali itupe maelezo. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, tunakwenda kuitisha bajeti ya shilingi triliuni karibu 41, tunatunga sheria ya matumizi na makusanyo. Kwa hiyo, ina maana sheria hii inawezekana inaelekeza kwamba fedha za mwaka fulani zisitumike mwaka

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

huu; na nina uhakika Serikali inaweza ikanijibu namna hii. Ninajua kwamba tunapitisha *Financial Bill* kwamba sasa twende kukusanya. Tunapitisha fedha za matumizi, sasa tunakwenda kutumia, lakini hizi fedha zinapokwa kutoka kwenye Halmashauri, zinakwenda kuwekwa wapi? Nani anazisimamia? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunapenda kupata majibu. Tunapenda kuelezwa kwamba hizi fedha hazitumiki kutokana na sheria iliyopo, lakini tunaziweka mahali fulani, tunakuja kuzionesha kama bakaa katika bajeti hii ambayo tunapitisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo hili linatia wasiwasi, tunajiliza mambo mengi, tunataka majibu kutoka kwa *Pay Master General*, atuambie kwamba fedha hizi zikirudishwa, miradi haikutendeka; na yapo maelekezo. Nakumbuka mwaka 2021 katika Kamati ya Bajeti na hata Kamati ya USEMI huko walikuwa wakipambana na hili jambo. Kamati ya Bajeti ilitueleza kwamba mwaka 2021 wamesema fedha hizi zifunguliwe akaunti maalum ndani ya Halmashauri. Ukienda, huwezi kupata akaunti hiyo na huwezi *ku-trace* hizi fedha ukazipata. Kwa hiyo, inawezekana zinatoa mwanya wa kutumika ndivyo sivyo. Sijasema wizi, hapana. Nimesema zinaweza kutumika ndivyo sivyo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tupewe maelezo ili tuone Serikali inapobeba fedha hizi inapata *impact* gani? Wanaziweka wapi? Nani anakuwa *accountable*? (*Makofi*)

WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:
Mheshimiwa Spika, Taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji.

TAARIFA

WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:
Mheshimiwa Spika, naomba kumpa taarifa msemaji kwamba

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kupitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2021/2022, Serikali ilileta mapendekozo ya kurekebisha sheria iliyokuwa inasema fedha zirudi na sasa fedha hizo hazirudi. Kupitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyoitoa mwaka 2021 wakati anahitimisha Bunge la Bajeti, fedha hizo sasa zinabaki kwenye taasisi husika, wanachotakiwa ni kuleta Mpango wa Utekelezaji wa fedha hizo, kwa sababu mwaka unakuwa umekwisha na fedha hizo zinabaki ndani ya taasisi husika au Halmashauri husika. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, unapokea taarifa hiyo?

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Spika, taarifa hii siipokea kwa sababu, tumekuta jambo hili lipo ndani ya Halmashauri. Nafikiri labda tungekuwa tumeypata maelekezo mapema. Siwezi kukubaliana, inawezekana ni kweli, lakini lipo. Kama wamefanya hivyo, mbona bado linaendelea? Kwanini liendelee? Kwa hiyo, ndiyo maana nilikuwa nasema, mimi nia yangu ilikuwa...

SPIKA: Ngoja. Kwa sababu umeuliza hilo swali hapo mwisho, nadhani kwa maelezo yake, anasema ni mwaka wa fedha 2021/2022. Maana yake ni kwamba, fedha za mwaka huu wa fedha ndiyo ambazo hazitarejeshwa. Kwasababu hizo nyininge, zilikuwa ni za mwaka uliopita kabla sheria hiyo haijabadilishwa. Nadhani utakuwa umeelewa sasa.

Yaani yale malalamiko ya Halmashauri hayazihusu fedha za mwaka huu, kwa maana ya mwaka 2021/2022. Malalamiko ya Halmashauri ni ya huko nyuma yaani tuseme, mwaka 2019/2020 ama 2020/2021, lakini Mheshimiwa Waziri anachokizungumzia ni kwamba mabadiliko yemeshafanywa na Serikali. (*Makofi*)

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Spika, sawa. Kwa hiyo, tutaiona katika ukaguzi wa mwaka huu, lakini bado tujue kwamba kuna fedha za nyuma. Labda aseme kwamba Bunge chini yako, lina uwezo wa kumruhusu CAG akakagua hizo fedha zilikuwa zinakwenda wapi? Tusifunge

hoja hii kwa sababu huku nyuma kumekuwepo na fedha zilizokuwa zinakaa katika msingi huo na hazijulikani zipo wapi?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hoja yangu niipeleke hivyo kwamba tuone katika ukaguzi wa mwaka huu kama fedha zitakuwa zimeoneshwa kama anavyosema, lakini bado malalamiko yapo ndani ya Halmashauri na wanaandika barua kuomba warejeshwe, bado hawajibu huko Hazina sijui kuna kitu gani, wataendelea kuona, lakini mimi tayari nimetoa ujumbe wangu, tunapaswa nasi kama Wabunge kujua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni bajeti hii, kwa hiyo, tunajaribu kuangalia kila senti ya Watanzania inatumika vipi na kama inakuwa *shambolic*, tujue ili tuweze kurekebisha mambo ambayo tunayaona. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niongelee pia kuhusu ufanisi wa utekelezaji wa miradi hii. Ni kweli ipo miradi ambayo inatekelezwa vizuri na ipo miradi ambayo inatekelezwa chini ya viwango. Niende katika Mkoa wa Kagera huko Bukoba Vijiji, kumekuwa na maeneo mengi ambayo tumekuwa tukilalamika. Kwanza, tumelalamika muda mrefu na ninamshukuru Waziri wa Uwezeshaji umewahi kuwa Waziri wa Fedha, nimewahi kukulilia kwamba sasa huko kwetu ndiyo ukweni, vipi? Kwa hiyo, bado mambo ni mabaya namna hiyo, hatuna barabara tangu uhuru. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kama kuna jimbo ambalo limetelekezwa kabisa na sisi tuna uchungu kusema ukweli hatuna barabara pamoja na mipango hatuna barabara ya lami, hatuna barabara ya kufungua uchumi, lakini kuna maeneo ambayo yanatengezwa kwa fedha za nchi, lakini bado zinatengenezwa chini ya viwango. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, naomba niseme kuhusu maeneo ya Chabaramba na eneo la Katokoro, haya maeneo ninayoyasema ni maeneo ambayo yana matingatinga ya miaka nenda, rudi. Ina maana labda hata mimi nimezaliwa yapo, lakini wanaokwenda kutengeneza

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

inawezekana hawafanyi ule upembuzi yakinifu. Nashukuru tumelia sana hapa wametengeneza kule Katokoro lakini lile daraja nimefika mimi mwenyewe *this time* nilipoenda, limepasuka, lina nyufa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, hata lile eneo la Chabaramba limetengenezwa, hata kama mimi sio mtaalam, barabara ipo hapa na ukingo wa maji upo hapa yaani vinaenda sambamba. Sasa nikajiliza haya ni makosa ya wahandisi na wahandisi katika nchi hii wakati mwingine jamani, si wote lakini wakati mwingine wanatuharibia kazi. Wanaharibu kazi zao kwa sababu, unawezaje kwenda kwenye kazi kama hii halafu ukaandika *certificate* mtu alipwe. Kwa hiyo, kuna vitu vya namna hiyo. Tumelia kuhusu daraja la Karebe Bukoba Vijiji daraja hili linafanya kiungo na ndiyo inasaidia uchumi wa jimbo letu. (*Makofi*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana. Muda wako umeisha Mheshimiwa.

CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi na Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, ajiandae.

MHE. ISSA J. MTEMVU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie katika hotuba au bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kama waliotangulia nami nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Samia Suluhu Hassan na nampongeza wazi kabisa ndani ya sakafu ya moyo wangu kwa sababu ya kazi kubwa anayoifanya, hasa ni katika kutekeleza bajeti ya mwaka 2021/2022. Pamoja na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mambo mengine makubwa ya ulinzi na usalama, lakini kiujumla miradi ya kielelezo ameitekeleza vile ambavyo Watanzania hawakutegemea. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, miradi mingi Watanzania wanatakiwa waijue ujenzi wa reli ya kisasa kwa kiwango cha kimataifa *SGR* ilikuwa takribani asilimia sabini na kitu sasa hivi ni asilimia 95.3 inakwenda vizuri hasa katika vipande vya mwanzo kuanzia Dar es Salaam - Morogoro lakini hata Morogoro - Makutupora hiyo imeenda kwa kiwango kikubwa, lakini mikataba mingi imeendelea katika vipande vilivyobakia.

Mheshimiwa Spika, mradi wa kufua umeme wa maji wa Mwalimu JK Nyerere *Megawatt* 2,115, nikiwa Mjumbe wa Kamati ya Bajeti, tumekwenda kule na tumejiridhisha kabisa kazi inakwenda vizuri kama Mheshimiwa Msukuma asubuhi alivyooleza. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ipo miradi mingine ujenzi wa bomba la mafuta ghafi, kutoka Hoima Uganda hadi Chongeleani Tanga, tunaambiwa kazi inakwenda vizuri na tumeona ameisaini mikataba ya mwisho.

Mheshimiwa Spika, vilevile mwisho kabisa ujenzi wa madaraja makubwa na barabara, hii hata kule Dar es Salaam wananchi wa Dar es Salaam wanajua kwamba lipo daraja zuri lile la *Tanzanite* pale *Palm Beach* ambalo limekamilika na limeshazinduliwa, lazima tumpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri ambayo alianza akiwa Makamu wa Rais akaipokea vizuri na sasa ameenda nayo vizuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, leo nitajielekeza katika maeneo kama mawili hivi eneo la *TARURA*, lakini vilevile na eneo la ardhi na hasa katika ukurasa wa 142. Upande wa *TARURA* tunashukuru sana katika kipindi kilichopita tumeona hapa *TARURA* ilikuwa ina changamoto kubwa na tumelia sana humu ndani mpaka tukaenda kwenye tozo, tukaweka tozo kwenye mafuta ya *petrol/na diesel/lili* tuongeze zaidi ya bilioni 396 kwenda kwenye *TARURA*, zitusaidie kwenye majimbo yetu

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

na Mheshimiwa Rais aliongeza zaidi ya milioni 500 hadi bilioni moja, wengine bilioni moja na nusu kuweza kwenda kwenye majimbo na tumeona kazi nzuri ambayo imefanyika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hii ni tofauti sana na Dar es Salaam, Dar es Salaam kule tunalia sana na hasa kwenye Wilaya ya Ubungo. Hii Wilaya ipo pembezoni na imesahaulika kwa muda mrefu sana. Barabara kule hakuna kabisa ni vumbi, ni mchanga, vumbi na udongo. Tumelia mara nyngi viongozi wakubwa wakija tunasema lakini ukweli kama nchi inao mpango mzuri wa mradi mzuri ambao tumekuwa tukiambiwa, sisi wawakilishi na wananchi wenyewe mradi wa *DMDP III*, Dar es Salaam *Metropolitan Development Program III*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ya kwanza imekuja tunesema hapa Bungeni, hata mwaka jana nnilisema kwenye Bunge la Bajeti. Program ile imesaidia Buza, Kijichi, Sinza na maeneo mengine kuna mataa mazuri kule hadi kule Mburahati. Ya pili imeenda kwenye Mto Msimbazi, nami nafurahi kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu. Hii ya tatu tumeambiwa inakuja lakini hatuioni ikija. Bunge liliopita nilisema hapa, Waziri akisimama atuambie inakuja au haiji, lakini hakuna majibu. Sasa hivi tunaambiwa kuna mtaalam mmoja kakaa nayo zaidi ya miezi mitatu au minne kusaini tu ili tuweze kuona, barabara zaidi ya kilometra 107 za vumbi ambazo wananchi walikuwa wanaamini tukipata ile wananchi wa Jimbo la Kibamba na Ubungo wanaenda kufurahi. Tunaomba sana sana kwenye majumuisho tuambiwe *DMDP III* ipo wapi inakuja au haiji kwenye bajeti inayokuja.

Mheshimiwa Spika, lipo jambo hapa limezungumzwa kwenye ukurasa wa 42; Ujenzi wa Barabara ya Njia Nane Kimara – Kibaha nilisema juzi kwenye swali langu la msingi tunafurahi sana tunaambiwa zaidi ya asilimia 86 sasa hivi zimekamilika zaidi tu palikuwa na ongezeko la kimkataba kwenye zile kilometra 19.2 Kimara - Kibaha lakini kuna shida. Jambo hili lilitkelezeza kisheria; niliuliza hapa sheria gani ilitumika kuwaondoa wananchi wa pembezoni pale kwenye barabara ya njia nane na kuwavunja bila fidia? Leo ni kilio

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kikubwa sana tulijibowi hapa sheria iliyotumika ni ya mwaka 1932, yaani mwaka 1932 baba yangu Marehemu Mzee Mtemvu kaondoka, babu yangu kaondoka, Alhaji Zuberi Mwinyishee Manga Mtemvu kaondoka, hakuna hapa ambaye aliwahi kuwepo. Bunge hili ndiyo linatunga sheria, leo tunaishi na sheria ya mwaka 1932 kweli? Sheria ya 1932 ndiyo inavunja makazi ya watu?

Mheshimiwa Spika, naomba niwakumbushe, mwaka 1974/1975 palikuwa na *operation vijiji* ambayo ilikuwa ina lengo la kuondoa watu ndani ndani kuwaleta pembezoni mwa barabara ambaao walijengewa shule, hospitali na kadhalika na kadhalika na vile vile hizi huduma maana yake ilikuwepo ni rasmi, lakini zipo sheria nyingine ambazo zilikuwa zinatumika. Kuna Sheria ya Mipango Miji, kuna *Land Act* ya mwaka 1999 Na.5, zote hizi zilikuja na kuondoa sheria nyingine zillizopita. Hata mwaka 1989 hati ya Kiluvya illitolewa na Mheshimiwa Hayati Kawawa aliipokea mwaka 1989, Kijiji cha Kiluvya, sasa na yenye we pia ilikuwa ni ya uongo. Hii inaleta sintofahamu tunaomba sana tufahamu jambo hili ili wananchi kama kweli walikuwa wana haki na haijafanyika, basi haki yao iende na zaidi ya hili hata palikuwa na kesi...*(Makofi)*

MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

SPIKA: Nani anayo. Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo.

MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO: Mheshimiwa Spika, nataka tu nimpe mchangiaji Mheshimiwa Mbunge wa Kibamba, pacha wangu kwamba, hili suala la fidia hata wananchi wa Ubungo Kisiwani ambaao wanatakiwa wapishe Mradi wa *DART* wanatakiwa walipwe fidia, lakini hatma yake haijulikani mpaka leo.

Mheshimiwa Spika, nataka nimpe tu hiyo taarifa.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. ISSA J. MTEMVU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru naipokea taarifa hiyo na ni ukweli...

SPIKA: Mheshimiwa Mtemvu, unasuburi uitwe kwanza. Mheshimiwa Issa Mtemvu unaipokea taarifa hiyo.

MHE. ISSA J. MTEMVU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naipokea tena ukitegemea ni taarifa ya Profesa ambaye si muda mrefu anaenda kuingia kwenye kilio kingine cha bomoa bomoa kutokea Ubungo hadi pale Kimara walipoanza kwangu. Pole sana nafikiri sasa utakimbizana na hilo ili lisiwafikie wananchi wako.

Mheshimiwa Spika, kuhusu jambo la ardhi, katika ukurasa wa 42 wa bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, kuna muda wengine tunalia juu ya changamoto, changamoto ni kujenga jenga barabara zenye mabonde mabonde na kadhalika na mashimo shimo ya mvua, lakini kuna wakati mwingine ni lazima kama nchi tulilie juu ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, juzi Mheshimiwa Rais alienda kuzindua nyumba za Magomeni *Quarter*, jambo zuri, nakumbuka zamani nikiwa Diwani pale ndiyo tulianza ule mchakato wa kuvunja vile vijumba na tukaja na malengo yale au mawazo mapana au maono mapana mwaka 2012. Miaka 10 baadaye tunaona Mheshimiwa Rais anaenda kuzindua nyumba maghorofa pale ambapo wananchi na Watanzania wameona, ni leo lazima tuwe na sura hiyo. Leo tuna Tandale kongwe kabisa, leo tuna Magomeni, tuna Manzese lazima tufikie tukajenge majengo ya aina ile.

Mheshimiwa Spika, hili kwenye nchi kadhaa limeshafanyika Misri kule na nchi nyininge, ni jambo jepesi tu, waende kuingia makubaliano na wananchi ambao wanamiliki hati zile katika vile vijumba vyao, wanawapa *floor* ya chini na *floor* ya kwanza, *floor* ya tatu hadi ya kumi wanachukua kama nchi ambayo kimsingi ...

MHE. TARIMBA GULAM ABBAS: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. ISSA J. MTEMVU: Mheshimiwa Spika, ni lazima haya yote tunaweza kuyafanya...

SPIKA: Watu wa Dar es Salaam hivi na nyie huwa mna... Mheshimiwa Abbas Tarimba.

MHE. TARIMBA G. ABBAS: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nataka nimpe taarifa mzungumzaji Mheshimiwa Mtemvu kwamba yaliyowafika kwake Kibamba pamoja na Ubungo, yaliwafika wananchi wa Jimbo la Kinondoni mwaka 2015, wamebomolewa wananchi wa Magomeni, wananchi wa Hananasif jumla nyumba 94, lakini mpaka leo hajjulikani, hivyo kilio chao na sisi Jimbo la Kinondoni tunacho.

SPIKA: Sasa hicho kilio, ndiyo maana Waheshimiwa Wabunge huwa nawakumbusha siku zote, hili ni taarifa kuhusu hoja ipi, kwa sababu hoja aliyokuwa anazungumza huyu ni ya kuipongeza Serikali kwa jambo lilihofanyika kwenye nyumba za Magomeni, sasa wewe unasema kilio kilichowapata, alikuwa hazungumzii kilio hapo alikuwa ameshamaliza hoja ya kilio kashaondoka huko.

Kwa hiyo taarifa Waheshimiwa Wabunge yaani uwe unafuatilia ile hoja aliyonayo na ndiyo maana huwa nasema inabidi umsubiri kama anahamia kwenye hoja nyingine kama kuna jambo amesahau ndiyo lengo la taarifa, siyo unataka kuchangia na wewe kuhusu jimbo lako na shida yako, unasema shida hiyo inafanana. Nadhani hapo tumeelewana Waheshimiwa Wabunge. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Issa Mtemvu, malizia mchango wako.

MHE. ISSA J. MTEMVU: Mheshimiwa Spika, nilinde na ni ukweli.

Mheshimiwa Spika, kwenye hoja hii ya makazi ambayo nilikuwa naendelea kuizungumza ni lazima tuzingatia Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa ambao moja ya malengo yake karibu manne, mojawapo ni kuchochea

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

maendeleo ya watu. Unachocheaje maendeleo ya watu wakiwa maskini, wakiwa wanakaa katika makazi ambayo si bora. Kwa hiyo, nalionna hili wenzetu vizuri ni lazima wazingatia kwamba sasa tukaboreshe kama Magomeni tulivyoona twendeni Tandale, Manzese na maeneo mengine ya Magomeni ili tuweze kuukuza mji.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

SPIKA: Kengele yake ya pili imeshagonga kwa hiyo nilikuwa nasuburi amalizie sentensi ili nimwambie muda wake umeisha. Ahsante sana.

MHE. ISSA J. MTEMVU: Mheshimiwa Spika, kama dakika mbili za mwisho.

SPIKA: Sasa nikikuruhusu maana yake na yeye nimruhusu akupe taarifa kwenye hiyo hiyo dakika yako moja.

MHE. ISSA J. MTEMVU: Mheshimiwa Spika...

SPIKA: Mheshimiwa Issa Mtemvu dakika yako moja unayopewa subiri upewe taarifa. Mheshimiwa Esther Matiko. (*Kicheko*)

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Mheshimiwa Mtemvu anahoja nzuri sana ya uendelezi wa haya makazi, kwa mfano katika majiji yetu yote Mbeya, Arusha, Mwanza na baadhi ya miji ukiangalia kwa kweli makazi yapo holela holela. Kwa hiyo ana hoja nzuri nai-cement kwa Taifa ili serikali iweze kuichukua.

SPIKA: Mheshimiwa Esther Matiko, wewe ndiyo mpima hoja nzuri humu ndani na mbaya. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Issa Mtemvu malizia mchango wako dakika moja.

MHE. ISSA J. MTEMVU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru itabidi nimalizie hapa hapa tu, lakini haya yote

haya wenzetu wamewahi kusema kuna Karl Max aliwahi kueleza vizuri juu ya *relationship between population growth and economic development*. Kwa hiyo, tuweze kuona, lakini hata Mao Zedong, baba wa China alisema *country is greatest wealth is its people* tutumie idadi ya watu zaidi ya milioni sita ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam kuweza kuongeza mapato na kuweza kuongeza mchango katika pato la Taifa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja ilio mbele yetu. (*Makof!*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi atafuatiwa na Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah na Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga ajandae.

MHE. SELEMANI J. ZEDI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi hili ili na mimi kwa niaba ya wananchi ya Jimbo la Bukene niweze kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia Afya njema, lakini niungane na Waheshimiwa Wabunge wengine kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa wanayofanya na kupeleka fedha nyingi za maendeleo katika maeneo yetu kule. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia maeneo ambayo yametajwa kwenye hotuba ya Waziri Mkuu na nitazungumzia kuhusu mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa mwaka 2022/2023. Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2022/2023 ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango mkubwa wa Miaka Mitano unaoanza 2021/2022 hadi 2025/2026. Huu mpango wa miaka mitano umegawanywa katika mipango mitano ya mwaka mmoja mmoja. Mpango wa kwanza ulikuwa huu wa mwaka 2021/2022 na sasa hivi tupo kwenye mpango wa pili wa 2022/2023 ambao ndio mapendekezo yake yameletwa rasmi ili sisi Waheshimiwa Wabunge tuyajadili na kuweza kutoa maoni yetu.

Mheshimiwa Spika, sasa jambo moja kubwa ambalo nimeliona katika mapendekezo ya mpango huu wa 2022/

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

2023 ni mwendelezo wa miradi ya kielelezo na kimkakati ambayo ilianza mwaka uliopita wa mpango. Mradi mmoja wa kimkakati na kielelezo ambao umetajwa ndani ya mpango huu ni mradi mkubwa wa ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Hoima, Uganda hadi Tanga. Wote tunafahamu faida kubwa ambazo nchi yetu itapata kutokana na ujenzi wa bomba hili la mafuta.

Mheshimiwa Spika, kwetu sisi watu wa Jimbo la Bukene Mradi huu wa Bomba la Mafuta kutoka Hoima Uganda mpaka Tanga una umuhimu wa kipekee sana pale kwangu kwenye Jimbo la Bukene ndipo itajengwa *project* moja kubwa sana inaitwa *Courting Yard* ambayo itagharimu zaidi ya shilingi bilioni 600. Hii *Courting Yard* ndio *project* ambayo mabomba yote ya mradi huu, mabomba yote yatakayolazwa chini kutoka Hoima mpaka Tanga yatapakwa rangi maalum ili yaziweze kuiza hiyo shughuli yote itafanyika ndani ya Jimbo langu la Bukene eneo linaitwa Sojo ambako wananchi wameshahamishwa hekari 140 zimeshatwaliwa tayari kwa kuanza ujenzi mkubwa wa *project* hii ambayo itagharimu zaidi ya Bilioni 600. Kwa hiyo, bilioni 600 zinakwenda kuwa *injected* ndani ya jimbo langu na nina uhakika kabisa itatokea *multiplier effect* kubwa sana ya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, nashukuru shughuli zinakwenda vizuri, wale wananchi waliopisha hizo ekari 140 wote wameshalipwa fidia. Walitaka kulipwa *cash* wamelipwa, waliochagua kujengewa nyumba wamejengewa na shughuli hii imekwenda vizuri. Jambo ambalo napenda kusisitiza hapa ni manufaa ya ajira ambayo nimekuwa nikiyasema mara zote na tumekuwa tukiahidiwa kwamba upendeleo maalum kwa watu ambao wanatoka maeneo ya karibu pale waweze kupata ajira ambazo hazihitaji utaalama mkubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hata ile *local content*, makampuni ya pale yaweze kufanya *supply* kwenye makampuni ambayo yanafanya kazi pale. Hivi karibuni kuna kampuni ambayo itafanya ujenzi pale inaitwa *ISOPHimekuja* pale Nzega, imeanza vizuri imeitisha wafanyabiashara na wadau na kuwaeleza fursa ambazo zitapatikana pale.

Msisitizo wangu hapa kwa Ofisi ya Waziri Mkuu hasa sehemu ya ajira na kazi ni kama ambavyo nilikuwa nimeshaomba awali kwamba hawa wazabuni wa Tanzania, *local* ni lazima watambuliwe na wawezeshwe ili kushindana na makampuni mengine ya nje kwa sababu bila kufanya hivyo kazi zote zitachukuliwa na makampuni yale ya nje.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, haitoshi kuja tu pale kusema kutakuwa na kazi ya *ku-supply* chakula, kutakuwa na kazi ya *ku-supply* usafiri kwa maana ya kutoa mabasi, kutakuwa na kazi hizi, haitoshi kusema hivyo, lakini hawa wafanyabiashara wa ndani wazabuni wa ndani lazima watambuliwe na wasaidiwe kama wanachangamoto za kibenki wasaidiwe kupata mikopo, changamoto za kiuwezo ili waweze kushindana na makampuni ya nje yanayofukuzia kazi pale, kwa sababu bila ya kuwawezesha, bila kufanya jithada maalum za kuwawezesha, kazi zote zitakazofanyika pale zitachukuliwa na makampuni ya nje. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pale Halmashauri yangu ya Nzega kutokana na thamani ya kazi zitakazokuwa pale, tunatarajia kupata ushuru wa huduma wa zaidi ya bilioni 1.8. Hapa Ofisi ya Waziri Mkuu itusaidie kwa sababu tulikubaliana kwamba sisi kama Halmashauri ya Nzega tutawasiliana na mtu mmoja tu wa *EACOP* badala ya kuwasiliana na yale makampuni madogo madogo ili ushuru wa huduma wa kampuni zote tuupate kutoka *EACOP* tu, ambao ndio wasimamizi wakubwa wa hiyo *project* yenewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mradi mwengine ambao umetajwa katika mapendekezo ya mpango wa miaka mitano ni ujenzi wa reli ya kisasa ya *Standard Gauge*, ninafahamu kwamba vipande karibu vyote kazi zimeanza na zinakwenda vizuri isipokuwa kipande cha Tabora mpaka Isaka kilometra 165 ambako ndiyo Jimbo langu la Bukene liliipo bado hatua za kumpata Mkandarasi ndiyo zinakamilishwa, lakini kwenye eneo hili msisitizo tu ni kwamba wananchi wa Jimbo la Bukene tunasubiri kwa hamu mradi huu wa reli ya kisasa kwa sababu pale Bukene itajengwa *station* kubwa ambayo itatumika kushusha mizigo na mizigo yote ambayo

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

itahudumia Nzega na Igunga itashushiwa Bukene. Kwa hiyo, tunasubiri kwa hamu hii *lot* kipande hiki cha Tabora Isaka nacho kipate Mkandarasi ili shughuli ya ujenzi iweze kuanza kufanyika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo jingine la faraja ambalo limezungumzwa katika mpango wa maendeleo wa miaka mitano ni kufanya mapinduzi makubwa kwenye sekta ya kilimo. Kilimo katika nchi yetu kimeajiri zaidi ya Watanzania asilimia 65, kwa hiyo kwa namna yoyote ile ukitaka kufanya mabadiliko kwa Watanzania ukitaka kuinua hali zao za kiuchumi, ukitaka kuinua hali zao za kimapato basi hakuna njia nyingine yoyote zaidi ya kufanya mapinduzi kwenye sekta ya kilimo. Kwa sababu ndiyo inaa jiri asilimia 65 ya Watanzania wote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa tatizo la kilimo chetu ni tija yaani kilimo chetu hakina tija siyo kwamba watu hawalimi, wanalima lakini kilimo chao hakina tija na ili tupate tija kuna mambo ambayo huwezi ukayaepuka katika kilimo. Kwa hiyo, katika mpango zimeelezwu jitihada za kubadili namna yetu ya ulimaji kwamba tuende kwenye matumizi ya mbegu bora, tuende kwenye matumizi ya mbolea, tuende kwenye matumizi ya viuatilifu lakini na huduma za ugani.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu hapo ni kwamba, kuanzia sasa hebu tuwe na mipango ambayo inakuwa na malengo ambayo yanapimika ili kila baada ya mwaka tunakuwa na jambo ambalo tunaweza tukalipima tuepukane kuwa na malengo ya jumla tu kwamba malengo yetu ni kuongeza matumizi ya mbolea yaani sentensi ambayo *is too general*, au malengo yetu ni kuongeza matumizi ya mbegu bora lakini lazima tuwe na malengo *specific* tuseme tuwe na *base lane*, tuseme labda katika matumizi ya mbolea sasa hivi tuko wapi na baada ya mwaka mmoja tunataka tuongeze matumizi ya mbolea kutoka wapi kwenda wapi? *Then* baada ya mwaka moja tunaweza tukapima tukaangalia timesonga mbele au hatujasonga mbele. Hivyo hivyo kwa mbegu bora, hivyo hivyo kwa viuatilifu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine kubwa sana katika kilimo ambalo ni changamoto na linakosesha tija ni uhakika wa masoko na bei bora kwa mazao ambayo tunalima. Kwa hiyo, naunga mkono eneo hili kwenye mapendekezo ya mpango kutiliwa mkazo na kuongeza msukumo ili kuleta mapinduzi ya hali za maisha na kiuchumi kwa watu wetu, kwa sababu kilimo kinaajiri asilimia 65 na huwezi kuleta mabadiliko yoyote ya kiuchumi kama hujaleta mapinduzi ya kutosha kwenye sekta ya kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono asilimia 100. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, atafuatiwa na Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga, Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane ajandae.

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwa kukupongeza wewe binafsi kwa kullongoza Bunge letu Tukufu lakini kwa kuaminiwa na Waheshimiwa Wabunge tuliomu ndani ya Bunge hili na kuweza kukaa kwenye Kiti ambacho umekaa hapo mbele. Na tunafarijika ukiwa hapo unatuongoza ndani ya Bunge letu Tukufu, Mungu akubariki sana. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, lakini nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kutuletea bajeti ambayo sasa hivi tunaizungumza na tunaijadili katika Bunge hili lakini kutuletea matumaini katika uwekezaji wa uchumi wa viwanda na maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Spika, nitumie kwa dhati kabisa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna ambavyo anachapa kazi lakini kwa namna ambavyo ametupatia fedha nyingi

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

katika Majimbo yetu kutekeleza miradi mbalimbali. Tumeshuhudia miradi ya ujenzi wa madarasa katika sekta ya elimu katika madarasa ya shule ya msingi sekondari na mengineyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia kwenye ujenzi wa Zahanati, Vituo vya Afya, Hospitali za Wilaya na hata Hospitali za Mikoa pamoja na Hospitali za Rufaa. Pia tumeona namna ambavyo barabara zetu zimeendelea kuimarishwa kuboreshwa kupertia *TARURA* pamoja na mambo mengine. Pamoja na hayo yote mazuri ambayo yameendelea kufanyika katika Majimbo yetu, lakini bado tunazo changamoto mbalimbali na sasa tunaomba Serikali isimamie katika kuhakikisha kwamba changamoto hizi zinapungua ama zinaondoka kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika eneo la elimu tuna changamoto upande wa shule zetu za sekondari kukosa nyumba za Walimu, hii imekuwa ni changamoto kubwa sana na hasa kule vijijini Mwalimu anapokaa kwenye nyumba ambayo haina hata umeme namna ya kuandaa masomo yake ambayo anategemea siku ya pili aende akayafundishe darasani inakuwa ni changamoto. Ningeiomba Serikali kuhakikisha kwamba tunaboresha kuhakikisha Walimu wanapata nyumba bora za kuishi na kuwatia moyo kuendelea kusimamia masomo yao madarasani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia tunayo changamoto upande wa barabara. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais ametupatia fedha nyingi katika kuboresha barabara zetu lakini bado tunayo changamoto kubwa hasa katika eneo la Lindi mjini. Zipo barabara hizi zina miinuko na mabonde kwa hiyo, uwekekaji wa kifusi katika barabara zile upo tofauti na barabara tambarale. Kwa hiyo, gharama kubwa inahitajika ya fedha katika kuhakikisha kwamba wanaimarisha barabara zile ziweze kupertika wakati wote wa kifuku na kiangazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaiomba Serikali kuwaongezea bajeti ndugu zetu wa *TARURA* waweze

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kusimamia kuboresha barabara zetu na ziweze kutumika vizuri lakini tujipange katika uwekezaji ambao wananchi wetu wanategemea kuwekeza katika maeneo yao. Tusipoimarisha barabara zetu uwekezaji utakuwa ni mgumu sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tuna sekta ya nishati. Katika eneo la Lindi Manispaa tumeppitiwa na bomba la gesi linalotoka Mtwara kwenda Kinyerezi kule Dar es Salaam na walini wakubwa wa miundombinu ile ni wananchi katika maeneo husika ambayo bomba hili limepita. Lakini tunayo changamoto wananchi wetu wa Lindi Manispaa, Lindi Mjini na Jimbo la Mchinga unaposema upo Manispaa halafu unakosa umeme, mwananchi hakuelewi. Kwa hiyo, tunayo changamoto kubwa katika maeneo yetu ya baadhi ya maeneo kukosa miundombinu ya umeme. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tumejaribu kuongea sana na Serikali inatuambia kwamba tuna mradi wa *peri-urban* unaokuja, sasa mwaka wa tatu hatujaona mradi wa *peri-urban*. Sasa ninaomba Waziri atuambie ni lini mradi wa *peri-urban* utakuja Lindi Manispaa kuhakikisha kwamba wananchi wa eneo la Lindi Manispaa wanapata umeme. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, jambo kubwa katika vijiji ambavyo vimepitiwa na bomba la gesi, wananchi wale waliahidiwa kwamba asilimia ya mapato yatarudi kuja kuwekeza katika shughuli za maendeleo katika maeneo husika, lakini tangia bomba lile limepita wananchi tunaendelea kulinda hatujaona hata Shilingi Moja inakuja kwetu Lindi Manispaa kuwekeza katika miradi ya maendeleo, nalo watuambie ni lini watatuletea fedha hii ije kutekeleza miradi ya maendeleo Lindi Manispaa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia tuna mradi wa *LNG* ambao tunatarajia kwamba Lindi katika Kata ya Mbanja kule Likong'o utakuja kutekelezwa, lakini wananchi wanashangazwa vikao vyote vinafanyika Arusha *why* visifanyike Lindi Mjini? kuna tatizo gani wananchi wanakiu kubwa ya kuona vikao vinavyojadili suala la mradi wa *LNG* vinafanyika katika eneo la Lindi Mjini, Lindi Manispaa. Kwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

hiyo, ni matarajio yetu ya kwamba vikao hivyo vinavyoendelea Arusha sasa virudi vigeuke kuja Lindi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, siyo hayo tu tunataka mashirika haya ambayo yanakuja kuwekeza yaweke ofisi zao pale Lindi Mjini, tuone shughuli sasa zinaendelea lakini hata Shirika la *TPDC* waweke Ofisi pale Lindi Manispaa, ile kusafiri kila wiki wako Dar es Salaam wako Lindi sisi hatufurahishwi tungependa kuona kwamba Shirika la *TPDC* linaweka Ofisi Lindi majengo yapo, maeneo ya kujenga Ofisi yapo, tunawakaribisha waje Lindi kuwekeza. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nzungumzie suala la Kilimo. Nimefurahishwa sana na hotuba mbalimbali zinazoendelea hivi punde nimetoka katika kikao pale cha Bodi ya Korosho namna ambavyo Mheshimiwa Bashe anatutia moyo katika kuleta mapinduzi makubwa katika mazao yetu ya biashara hasa katika zao hili la korosho. Kwa hiyo, nishukuru sana lakini niendelee kumpongeza nimitakia kheri katika mapinduzi yale makubwa ambayo tunatarajia kuyapata. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imezungumzia suala la Benki ya Maendeleo ya Kilimo. Sasa kushuka kwa wakulima wadogo wadogo tumeona ya kwamba benki hii imewawezesha wakulima wakubwa, sasa tunahitaji wakulima wadogo wafikiwe na benki hii. Tusipomuwezesha mkulima kupata fedha ya kuwekeza kwenye mashamba yake, kilimo chao kitakuwa hakina tija miaka nenda rudi, tunajua ya kwamba Serikali inatupatia *Sulphur*, pembejeo bure lakini pembejeo ile wasipokuwa na fedha ya kuendelea kwenda kuwekeza katika mashamba tutakuwa bado hatujawasaidia.

Mheshimiwa Spika, Wakulima wetu hawakopesheki kwa sababu hawana Hati Miliki ya mashamba yao kwa hiyo, ninaiomba Serikali kuhakikisha kwamba sasa tuwarathimishe wakulima wetu waweze kupata Hati Miliki na waweze kuingia kwenye vyombo vy ya fedha waweze kupata fedha na waweze kuendelea kuwekeza katika shughuli za kilimo. (*Makof*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, nzungumzie suala la miradi ya kimkakati, muda mrefu sasa yapata miaka minne tumeomba fedha kutoka Serikali Kuu kutuwezesha kujenga soko jipy, soko la kisasa lakini kujenga stendi mpya ya mabasi ya kisasa. Katika Manispaa pekee haina stendi ya kisasa ni ya Lindi Manispaa. Inasikitisha sana mwaka wa Nne sasa tunafuatilia hakuna kinachopatikana, ninaomba wakati wa ku-*windup* Waziri husika atuambie kuna tatizo gani la kutotupatia fedha kwa ajili ya uwekezaji wa ujenzi wa soko jipy la kisasa lakini pia ujenzi wa stendi kuu ya mabasi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nzungumzie suala la Wenyeviti wetu wa Serikali za Mitaa, Wenyeviti hawa wanafanya kazi kubwa sana na wanatusaidia sana katika kuimarisha ulinzi na usalama, lakini haijatokea hata siku moja tukawanunulia vitendea kazi. Kila kazi wanafanya kwa pesa yao lakini mapato wanayoyapata ni madogo sana. Ninaiomba sana Serikali kuangalia kwa jicho la huruma Wenyeviti wa Serikali za Mitaa kuhakikisha kwamba Posho yao wanaongezewa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ninaomba kuunga mkono asilimiamia moja. Ahsante sana. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Hassan Selemani Mtenga, atafuatiwa na Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mheshimiwa Mhandisi Samweli Xaday Hhayuma ajiandae.

Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, atafuatiwa na Mheshimiwa Mhandisi Samweli Xaday Hhayuma.

MHE. FRANCIS K. NDULANE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kama walivyotangulia kuongea wenzangu napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu wa Rais pamoa na Waziri Mkuu, Bunge

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Iako Tukufu pamoja na Wabunge wote kwa namna ambavyo kwa pamoja tunashirikiana katika kuhakikisha kwamba miradi ya maendeleo inatekelezwa vizuri inasimamiwa vizuri na tunaishauri vizuri Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, namshukuru zaidi Mheshimiwa Rais kwa sababu ameweza kutenga fedha nyingi katika mwaka wa fedha huu tunaoumaliza ili kuhakikisha kwamba miradi mingi inakwenda na kwa kweli inakwenda, kwa kweli nampongeza sana Mheshimiwa Rais. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ningependa kujikita katika maeneo machache sana leo katika kuchangia kwenye bajeti hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwanza ningependa kuzungumzia miundombinu ya barabara pamoja na madaraja, ninaanza kwanza na barabara kuu.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na barabara nyingi ambazo zimefanikishwa na Serikali kujengwa na madaraja mengi kama hayo ya *Tanzanite*, barabara ya njia nane kutoka Ubungo kwenda Kimara mpaka Kibaha, lakini kule kwenye barabara ya Kilwa Serikali imefanya kazi kubwa sana kuanzia pale gerezani kwenda mpaka bandarini, kwenda mpaka rangi tatu kuna kilometri 20 pale kazi inakwenda moto moto katika kuhakikisha kwamba barabara ya mwendo kasi inajengwa kwa *speed* kubwa ili kuwaondolea adha wananchi ambao wanakwenda Mikoa ya Kusini ya Lindi, Mtwara Ruvuma mpaka Njombe siku hizi wanatumia barabara ile. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini kuna shida katika eneo la kutoka pale Rangi Tatu eneo wanaita Tanita kwenda kutokea pale Kongowe kuna shida kubwa, kuna kipande pale cha kilometri kama 12 hivi kimesahaulika, kile kipande tangu enzi za hayati Rais wetu wa Serikali ya Awamu ya Tano alipokuwa Waziri wa Ujenzi kile tayari kililengwa kujengwa kwa kiwango cha lami barabara nne mbili zinakwenda mbili zinarudi matokeo yake leo ni zaidi ya miaka 10 sasa hivi, *diversion* zimewekwa kwenye barabara ile sasa zinaota nyasi na kuota

miti bado barabara ile haijaanza kujengwa toka pale Tanita kwenda Kongowe. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninaiomba Serikali katika bajeti ya Mwaka 2022/2023 tuweze kuijenga ile barabara kwa kiwango cha lami njia nne ili kupunguza adha ambayo inawakuta wananchi ambao wanakwenda kwenye Mikoa hiyo nilioitaja.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli barabara ile ikifika asubuhi wakati watu wengi wanakwenda katikati ya Jiji au wakati wa jioni wakati watu wanarudi majumbani kwao, kwa kweli imekuwa na adha, kipande kile cha kilometra 12 watu wanatumia masaa matatu hadi manne pale foleni ilivyokuwa imekaa vibaya, kwa hiyo naomba sana Serikali iangalie ile barabara ikiwezekana kwenye bajeti ya 2022/2023 basi iweze kufanyiwa kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini nikienda kwenye upande wa *TARURA* naishukuru Serikali pia kwa kazi kubwa ambayo imefanya ya kuongeza fedha hasa zile za maendeleo kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya barabara, lakini nilikuwa na rai kwenye upande mmoja. Barabara zile pamoja na kwamba zimekuwa zikiletewa fedha nyngi na Serikali tena kwa wakati lakini taratibu za manunuzi zimekuwa zikichelewa sana kiasi kwamba hadi mvua kubwa za mwisho wa mwaka na mwanzo wa mwaka zinapoanza unakuta bado miradi hajja-*take place* kwa sababu zabuni inatangazwa katikati ya mwaka wa fedha, kwa hiyo, unakuta kipindi kama hiki sasa ndiyo wanahangaika sasa kuchakarika kuweza kutengeneza barabara wakati fedha zilishakuja muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninaomba Serikali isimamie *TARURA* ili iweze kutengeneza utaratibu ili angalau *60 percent* ya zabuni ziweze kutangazwa kipindi kama hiki ili mwaka unapoanza wa utekelezaji wa miradi mwezi Julai basi tuweze kuendelea vizuri bila shida ili hiyo asilimia 40 inaweza ikatangaza zabuni zake baadaye kama ambavyo wanafanya wenzetu wa *TANROADS*. (*Makof*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, lakini pia ningeomba Serikali itengete fedha za dharura kwaajili ya TARURA. Nchi yetu miaka ya karibuni imekuwa na bahati nzuri ya kuwa na neema ya kuwa na mvua nydingi, na matokeo yake kwa kuwa miradi inachelewa lakini vile vile kwa kuwa fedha za *emergency* hazipo basi inapofika mahali imetokea mvua kubwa, madaraja, makalavati yamebomoka inakuwa shida kupata fedha za kurekebisha hali inayojitokeza kwa haraka ya uvunjifu makalavati na madaraja hayo.

Mheshimiwa Spika, kwahiyio ningeomba Serikali itengete pia fedha za dharura ili ikitokea *emergency* basi mara moja fedha ziweze kwenda na TARURA iweze kuchukua nafasi na kufanya kazi yake sawasawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lingine, ningeomba Serikali itengete fedha kwa ajili ya miradi maalum. Kama waliviotangulia kuongea baadhi ya Wabunge wenzangu siku ya leo, kwamba kuna baadhi ya maeneo kwenye baadhi ya majimbo kuna mabonde makubwa. Mimi pia pale kwangu, katika Jimbo langu, kuna bonde la Mto Hanga kutoka Kinjumvi kwenda Mtialambuko, lina urefu wa zaidi ya kilometra tano, ambapo wakati wa mvua maji yanajaa sana. Kwahiyio katika miradi kama ile unaweza ukakuta ukitegemea ile bilioni 1.5 ya maendeleo unaweza ukajikuta hela yote inazama kwa ajili ya kujenga tuta na kujenga daraja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwahiyio nilifikiri kwamba Serikali itafute vyanzo vya ziada ili tupate hela za ziada kwa ajili ya kutekeleza miradi mikubwa kama ile ambayo inahitaji fedha nydingi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni la pembejeo. Kumekuwa na shida katika mwaka uliopita, lakini nimefurahi Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Naibu wake hivi karibuni walikuja na ajenda ya 10/30 ambayo inaonekana itakuwa muarubaini sasa kwenye mambo ya pembejeo na miundombinu mingine ya uendeshaji wa shughuli za kilimo. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, lakini kwa kwakweli hali ilikuwa mbaya kutokana na changamoto ambayo imeelezwa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya uwepo wa *COVID 19*. Hata hivyo bado Serikali inatakiwa iweke mkakati wa kudumu wa kuhakikisha kwamba changamoto ya upatikanaji wa mbolea pamoja na pembejeo isiwe endelevu ili tutatue hii changamoto. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano mwaka jana msimu uliopita tulikuwa na ununuzi wa mbolea aina ya *urea* ambayo ilifikia wastani wa shilingi 104,000 kwa pakti moja, mbolea ya aina ya *sulpheriliuzwa* mpaka shilingi 86,000. Wakati huo huo kwa wakulima wa mahindi walio wengi, Serikali ilinunua gunia moja kwa shilingi 55,000. Kwahiyoo unawenza ukaona namna ambavyo wakulima wetu wanavyoumia, hasa wale ambao hawapewi ruzuku za bure. Tunaishukuru Serikali msimu uliopita kwa zao la korosho walltoa ruzuku ya bure, lakini kwa mazao mengine ilikuwa shida. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini tumejata *promise* ya Mheshimiwa Waziri kwamba mazao mengine ya kimkakati nayo yatasaidiwa. Basi pale ambapo itashindikana tujitahidi kudhibiti hizi bei za pembejeo, hususani mbolea, kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wakulima wetu wanalima kilimo chenyetija ili kuusukuma mbele uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini nikienda kwenye uvuvi na mifugo; tumeanza kupata ahueni kuitia ajenda 10/30 kule kwenye kilimo. Wataalam wetu wa mifugo na uvuvi wamekuwa na shida ya vyombo vya usafiri. Wale wa kilimo tayari wameshapewa pikipiki 6,704. Naomba Serikali ielekeze jicho lake sasa kwa wataalam wetu wa mifugo na uvuvi ili nao waweze kupatiwa vitendea kazi hususani hivi vitendea kazi vya usafiri na hizo *kits* za kufanya kazi katika maeneo yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vile vile ningependa niiombe Benki yetu ya Maendeleo ya Kilimo na benki nydingine ambazo zinatoa mikopo ziwafikie wakulima, wavuvi na wafugaji wadogo kwa sababu wakulima, wavuvi na wafugaji

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wakubwa ndio wamekuwa wakipata mikopo hii kwa wingi. Na kwa sababu wao wana mitaji, wana uwezo wa kuajiri mtu wa kuandika maandiko; na kwa sababu masharti ni magumu na *very complicated* kiasi kwamba hayawezhi kuwa attained na wale wafugaji, wakulima wadogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba tuwe na *special funds*. Kwamba, tunaweza tukaanzisha mfuko maalum wa maendeleo kwa ajili ya wakulima, wavuvi pamoja na wafugaji wadogo ili hata yule mkulima mwenye heka tatu aweze kunufaika na mikopo hii. Kwa sababu kwa hali iliyopo sasa hivi ni ngumu, kuna taratibu nyingi ambazo zinawafanya wale wakuliwa wasiweze kupata mikopo hiyo. Kwa hiyo ningeomba kwamba turekebishe, tushirikiane na watu wa vyama vya ushirika, tushirikiane na watu wa halmashauri; na ikiwezekana taratibu zake zifanane fanane na zile asilimia 10 zinatolewa na halmashauri ili kuwarahisishia...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Haya, ahsate sana.

MHE. FRANCIS K. NDULANE: ...wakulima, wavuvi na wafugaji kupata hiyo mikopo ili waweze kuboreshewa zana zao za kufanya kazi, waweze kuchakata mazao vizuri, lakini vile vile waweze kuongeza thamani ya mazao yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mhandisi Samwel Xaday HHayuma.

MHE. ENG. SAMWELI X. HHAYUMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Awali ya yote mimi nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, tarehe 23 alitutembelea sisi Wana-Hanang' na alikuwa kwetu mpaka tarehe 26 akijaribu kuhamasisha maendeleo ndani ya Mkoa wa Manyara. Akiwa kule aliletta salamu za Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Mheshimiwa Makamu

wa Rais Dkt. Philip Isdori Mpango. Hakuja hivi hivi, alikuja kueleza zile neema ambazo zimekuja kwenye mkoa wetu na kwenye Wilaya yetu, ya madarasa kwenye shule shikizi pamoja na shule za sekondari, kwenye sekta ya afya pamoja na sekta ya maji.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati alipokuwa Hanang' aliwaahidi Wana-Hanang' mambo kadhaa. Ninachoomba tu mimi nilivyo simama hapa salamu zile za shukurani za Wana-Hanang' lakini kukumbusha tuu mambo machache kati ya yale ambayo Wanahanang walimuomba.

Mheshimiwa Spika, Hanang' ni Wilaya kongwe; Mji wa Katesh ni Mji wa muda mrefu lakini changamoto kubwa ni ya maji. Tunashukuru tangu tumeanza na watu wa *BAWASA* wanafanya kazi nzuri sana; kabla tulikuwa tulikuwa na *KAWASA*. Hata hivyo wanayo changamoto, fedha za mabomba zilizoahidiwa hazijafika; bado fedha za kutekeleza ule mradi hazijafika. Tunaomba sana hizo fedha zitolewe kwa wakati ili Mji wa Katesh uweze kupata maji ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mradi wa Maji wa Gehandu ulioahidiwa na Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni. Mheshimiwa Rais wetu wa Awamu ya Sita, Mama Samia Suluhu Hassan alisema kwamba ye ye akisema inatekelezwa na kweli imetekelizwa. Mkataba wa bilioni 2.8 umeshasainiwa. Tunachoomba; mwaka huu maji ni changamoto kubwa, mvua ni chache wananchi wa Gehandu wako milimani. Ili wapate nafuu huu mradi uliosainiwa wakandarasi waende kwenye *site* kwa wakati ili waweze kuwasaidia wananchi hao wasipate changamoto kubwa ya maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tuna mradi mkubwa wa maji kutoka katika Ziwa Basutu. Kwenye eneo hili, niwapongeze na kuwashukuru sana wadau wa maendeleo wa *Water Aids* walitoa milioni 500. Serikali kupitia fedha hizi tulizozikopa kupitia *World Bank* milioni 550 zimeenda pale, lakini kabla

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

zilienda milioni 70; ni mradi wa bilioni 12 kwa vijiji zaidi ya 9. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali yangu iuangalie mradi huu kwa jicho la kipekee. Lakini na hao wadau wanaotusaidia waweke nguvu zaidi ili tuhakikishe kwamba wananchi wale ambao bado hawajafikiwa wawe wamefikiwa.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Mji wa Katesh wakati ule wa kampeni tulishaahidi kilometra 10 za lami. Nilimuomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati alivyokuja kwenye jimbo letu, kwamba, kwenye bajeti hii tunayoenda 2022/2023 atupe angalau, au atupiganie kupata kilomita nne za lami ili tupunguze ile 10 aliyoahidi mama tukiwa tunaelekea kwenye 25 wakati wa kuomba kura, Wanahanang tumewaaahidi lami kidogo kidogo kwa kipindi kirefu. Tukiwapa nne halafu tukaanza kidogo kidogo, kama tukienda na mbili mbili tutakuwa tumeenda zaidi. Ukifikia asilimia 70 utakuwa umefaulu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninachoomba sana, kwenye eneo hili ni kwamba, tupate hizo kilometra nne kwenye bajeti hii ya 2022/2023 ili tuendelee na hizi ahadi ambazo zimetolewa tangu mwaka 2010 ili zianze kutekelezwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vilevile tuna barabara yetu ya Katesh - Masatu - Haydom. Ukifika Mlima Chavda pale changarawe ile inatereza, tunamwaga ngano nydingi sana pale. Tusaidiwe kwenye eneo hilo, barabara ile iwekwe lami, ni kilometra 70 tu.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana Mheshimiwa Flatei alitaka kupiga sarakasi kwenye eneo hili. Ninaomba tusifike kwenye hatua ya kupiga sarakasi, kazi hii ifanyike kwa sababu ni ahadi ambayo imetolewa wakati wa uchaguzi na tumeihaidi kwenye llani yetu ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2020/2025. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vilevile tuna barabara ya Nangwa – Gisambalang – Kondoa. Kwa sasa barabara ile imekatika kabisa, mvua ikishanyesha haipitiki kabisa. Hakuna shughuli inayoendelea kwenye kata zaidi ya sita. Barabara hiyo ndiyo inayounganisha Wilaya ya Hanang na Wilaya ya Kondoa. Tunazo Kata za Gisambalang, Dirma, Simbay, Sirop, Kata ya Wareta pamoja na Kata yenewe ya Nangwa. Kote huko wananchi wangeweza kupita katikati tu hapo ambapo ni kilomita kama 50, lakini wanalazimika kutembea zaidi ya kilometra 200 kufanya shughuli zao za kiuchumi. Tunaomba Serikali itusaidie kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, katika barabara hiyo daraja limeondolewa na mafuriko ya mvua ya 2019/2020. Tuliamini lingekuwa ni suala la dharura, lakini mpaka sasa Daraja la Munguri B halijatengenezwa. Ukitaka kupita pale mvua ikinyesha uombe Mungu upite. Tumekuwa tukipata changamoto kubwa kwaajili ya eneo hilo, tunaomba tupate usaidizi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nisemee kidogo uchumi wa Wilaya ya Hanang'. Sisi tunategemea kilimo na ufugaji. Kwenye eneo la mifugo kwa kipindi kirefu tulikuwa na malambo ambayo yamejengwa kwa ajili ya kusaidia kunyweshea mifugo, ikiwa ni pamoja na changamoto nyingine ya malisho. Malambo yale yaliyojengwa mengi ni ya muda mrefu, yamechakaa, ni ya tangu mwaka 1980. Serikali iangalie namna ya kukarabati na kujenga.

Mheshimiwa Spika, tunalo Lambo la Gidahababieig ambalo Serikali kwa kipindi kirefu imeahidi kwamba lile lambo litaboreshwu kwa sababu mkondo ule una maji mengi. Kwamba watajenga bwawa kubwa ambalo pamoja na mifugo kupata maji, vilevile litasaidia wananchi kufanya umwagiliaji. Tunachoomba kwenye eneo hilo Serikali sasa itupie jicho la ziada.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye hotoba yake, ukurasa wa 24, amesitisiza sana suala la kilimo. Kwamba kilimo chetu ili kiende tunahitaji mbolea, mbegu za

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kisasa pamoja na viuatilifu. Ninachoomba kwenye eneo hili, tuwasaidie wananchi wa Hanang'.

Mheshimiwa Spika, kwenye hotoba ya Mheshimiwa Rais wakati anazindua Bunge hili la 12 alisema tuna nakisi ya tani laki nane mpaka milioni moja za ngano; na Hanang' ilikuwa maarufu sana kwenye kilimo cha ngano. Tuliangalie eneo hili ili tuboreshe kilimo cha ngano, tuache kuagiza ngano kutoka nje ya nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tulikuwa na mashamba yale ya *NAFCO*. Mashamba yale mpaka sasa kwenye yale maeneo ambayo yamemilikishwa kwa wananchi, wakulima wakilima wanapata kati ya gunia nane mpaka 12. Sasa, tunazo ekali zaidi ya 42,000 tumemmilikisha mwekezaji. Mwekezaji huyu ye ye akijitahidi sana ye ye anapata kati ya gunia tano mpaka sita. Mwekezaji huyo, si wananchi wa kawaida ambao hawatumii mbolea, wananchi wa kawaida ambao wanalima kwa njia za kawaida za asili. Sasa naomba tufanye tathmini ya kina kwenye eneo hilo. Je, mwekezaji huyu bado tunahitaji kuwa naye?

Mheshimiwa Spika, kwa hekari 43,000, kwa hesabu za kawaida ambazo mimi nimezifanya, ye ye akilima kwa namna ambayo analima kwa sasa, tunapata kati ya gunia 219,800 mpaka 263,000. Lakini wangepewa wananchi wa kawaida wa Hanang' wangeweza kuzalisha kati ya 351,000 mpaka 439,000, wananchi wa kawaida ambao hawatumii mbolea, ambao wanatumia kilimo chao cha asili. Ukienda kwenye vyama vya ushirika ambao wanapata misaada mbalimbali kutoka maeneo kadhaa ikiwepo benki yetu ya kilimo wanaweza kuzalisha kati ya gunia 527,000 mpaka 659,000. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna kazi ya kufanya kwenye eneo hilo. Ninachoomba ndugu zetu wa Wizara ya Kilimo, hao wenzetu ambao wamepewa haya mashamba, wapewe shamba moja tu kati ya mashamba yale ambayo wamepewa, yale mengine wapewe wananchi hao wa kawaida ili waweze kulima kwa namna ambavyo wanaona

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

au vinginevyo wapewe vyama vya ushirika ili tuzalishe kwa tija na ili waweze kusaidia Wilaya ya Hanang' kiuchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushuruku sana. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge orodha ambayo Waheshimiwa Wabunge walikuwa wameomba kuchangia siku ya leo imekamilika, na kwa hivyo upande wa Serikali wamezisikia hoja zenu na ushauri wenu Waheshimiwa Wabunge.

Niwakumbushe tuu kuhusu matumizi ya neno maslahi. Kanuni yetu ya 68 inazungumzia kutozungumzia jambo ambalo lina maslahi binafsi ya kifedha. Waheshimiwa Wabunge tuizingatie hii kanuni ili tunapoitumia basi tuweze kufikia mwisho wa hiki kinachosemwa kwenye hii kanuni. Ukishaanza kwa kusema unayo maslahi inabidi utoe maelezo ya yale maslahi yako kifedha halafu ukimaliza ndipo tunaanza kupima kama uchangie hiyo hoja au hapana. Hii ni kwa sababu inawezekana mawazo yako yakaathiri mawazo ya Waheshimiwa Wabunge humu ndani halafu wakafanya maamuzi fulani kwa kukusikiliza wewe kumbe una maslahi ya kifedha kwenye jambo hilo.

Na hayo maslahi ya kifedha kanuni yetu inataka uyataje. Kanuni yetu inataka uyataje hayo maslahi yako binafsi ya kifedha kwenye hoja unayotaka kuchangia. Kwa hiyo tukaipitie hii Kanuni ya 68 na masharti yaliyowekwa hapo kwa sababu ndio kwanza tumeanza kuchangia.

Kwa hiyo huko mbele watu watakuwa na maslahi na maslahi kwenye jambo hili na lile, lakini inabidi ukishasema tuu una maslahi binafsi na jambo hilo inabidi ututajie ni maslahi gani na ni fedha kiasi gani ili maamuzi ya Bunge usije ukayapelekea sehemu ambayo tunataka kuamua jambo kwa sababu wewe jambo hilo una maslahi nalo. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Baada ya kusema hayo, Waheshimiwa Wabunge ninaahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya Jumatatu, saa tatu Asubuhi.

*(Saa 11:35 Jioni Bunge lilahirishwa hadi siku ya Jumatatu,
Tarehe 11 Aprili, 2022 Tatu Asubuhi)*